**6 NOVEMBA, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Sita – Tarehe 6 Novemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc*. – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante. Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa niaba yake, Mheshimiwa Omar Omar.

**MHE. OMAR ALI OMAR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Omar.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa natafakari hapa, kumbe napungiwa mkono kuonesha kwamba Yanga jana wameshinda magoli Matano! Haya, sawa. Tunawapongeza sana Yanga kwa mpira mzuri waliocheza jana. Sasa si mnajua kanuni zetu nikishasema hapa mbele, nimeshasema kwa niaba ya Bunge. Ndiyo kanuni zetu zinavyosema, kwa hiyo, msianze kuleta fujo humu Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc*. – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, sasa aulize swali lake.

Na. 69

### Mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Jimbo

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, Serikali inazingatia vigezo gani kugawa fedha za Mfuko wa Jimbo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Jimbo la Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Jimbo umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 16 ya mwaka 2009 kwa lengo la kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuchochea maendeleo ya Jimbo. Aidha, vigezo vinavyotumika kugawa fedha za mfuko wa Jimbo ni pamoja na idadi ya watu Jimboni asilimia 45, mgao sawa kila Jimbo asilimia 25, kiwango cha umaskini asilimia 20 na ukubwa wa eneo asilimia10, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali ilifanya tathmini kwa kuzingatia vigezo hivi sambamba na mgawanyo wa fedha za majimbo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunashuhudia baadhi ya majimbo yakipata fedha kidogo ukizingatia kwamba vigezo alivyovieleza Mheshimiwa Waziri ni vikubwa zaidi ukilinganisha na Majimbo mengine na hata hali ya umaskini ni kubwa zaidi. Mfano mzuri ni Jimbo langu la Wingwi: Je, Serikali haioni iko haja ya kufanyia tathmini vigezo hivi, kwa kuzingatia sensa ya mwaka 2022? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Spika, ahsante sana, ni kwamba Serikali inafanya tathmini ya vigezo hivi mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba vinakidhi uhitaji wa fedha za Mfuko wa Jimbo katika Majimbo yetu na pia kuona namna nzuri ya kuendelea kuboresha *formula* za hivi vigezo ili kuweza kutoa fedha kwa ajili ya maendeleo ya Mfuko wa Jimbo kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kufanya tathmini mara kwa mara, na mara itakapoona kuna maeneo ambayo vigezo vinahitaji kuongezwa au kupitiwa upya, basi suala hilo litafanyika.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kwamba fedha za Mfuko wa Jimbo zinatofautiana kutoka Jimbo moja na Jimbo lingine kwa kuzingatia vigezo hivi. Kama nilivyosema, asilimia 45 ya idadi ya watu katika Jimbo husika; kwa hiyo, Majimbo yenye idadi kubwa ya watu *automatically* yatakuwa na fedha nyingi zaidi, lakini kiwango cha umaskini kwa asilimia 20 pia na ukubwa wa eneo la kijiografia kwa asilimia 10, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga sasa aulize swali lake.

Na. 70

**Ujenzi wa Stendi ya Kisasa Mwanga**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Stendi ya kisasa katika Mji wa Mwanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Jimbo la Mwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya ufinyu wa stendi ya magari katika Halmashauri ya Mwanga. Halmashuri imeandaa andiko lenye thamani ya shillingi bilioni 3.2 kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa na kuliwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI mwezi Agosti, 2023 ambapo wataalam wanaendelea na mapitio ya andiko hilo kulingana na vigezo kwa ajili ya utekelezaji, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja tu la nyongeza. Andiko la mradi liliwasilishwa tarehe 28 Desemba, 2021. Mwaka 2022 nilikumbushia kwa njia ya swali la nyongeza, nikapewa majibu kwamba mchakato unaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwezi Julai, mwaka huu 2023 Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Naibu Waziri, TAMISEMI, alitembelea Jimboni kwangu, tulipomkumbushia hilo ndiyo akashauri kwamba tufanye wasilisho la kukumbusha. Kwa hiyo, wasilisho analoli-*refer* Mheshimiwa Waziri hapa ni la kukumbusha ambalo limewasilishwa mwezi Agosti mwaka huu 2023 na ninalo hapa, limefanya *reference* kwa andiko la msingi ambalo ni la mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, swali langu: Kwa kuwa hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na ni ya muda mrefu: Je, Mheshimiwa Waziri sasa yuko tayari kutuambia ni lini kazi hii itaanza ili wananchi wa Mwanga waanze sasa na wao ku-*play their party* kwa kuanza kukusanya *material site* kama sehemu ya mchango wao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba Halmashauri ya Mwanga iliwasilisha andiko awali mwaka 2021, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilipitia na kuwarejeshea kwa ajili ya kuboresha maeneo ambayo yalihitaji maboresho zaidi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge

kwamba, ahadi za viongozi wetu wa Kitaifa, ahadi za Mheshimiwa Rais ni kipaumbele chetu na ndiyo maana tayari tumeingiza kwenye mpango, tunafanya tathmini ya mwisho wa vigezo na wakati huo huo tunatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi katika Halmashauri hiyo ya Mwanga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mwanga wawe na imani kwamba Serikali kuna hatua za mwisho za tathmini na mara fedha zikipatikana tutakwenda kuanza ujenzi wa stendi hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mwaka 2022 niliuliza swali hapa ndani ya Bunge nikajulishwa kwamba nilete andiko kwa ajili ya ujenzi wa Stendi ya Wilaya ya Biharamulo. Pia kwenye miradi ya kimkakati wa Mkoa wa Kagera kwenye bajeti ya mwaka huu 2023 tuliwasilisha pia. Sasa, naomba kujua ni lini ujenzi wa Stendi ya Wilaya ya Biharamulo utaanza ili wananchi wa Biharamulo waweze kupata huduma hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Biharamulo kwa kuwasilisha andiko la maombi ya Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Halmashauri na nimwambie tu kwamba baada ya mawasilisho hayo Serikali inaendelea kupitia maandiko yale kufanya tathmini ya vigezo. Pia sambamba na hilo, kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, mara fedha zikishapatikana na baada ya kupitia andiko hilo na kujiridhisha na vigezo, fedha itatafutwa kwa ajili ya kujenga stendi hiyo ya Biharamulo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana 2022 niliuliza swali na Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu kwa kutushauri kwamba tuandike andiko na tuwasilishe katika TAMISEMI kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Mabasi Wilaya ya Namtumbo: Je, Serikali nayo iko tayari au inaweza kutueleza ni lini nasi tutapata fedha kwa ajili ya kujenga stendi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha. Nafahamu Jimbo la Namtumbo na majimbo mengine yote kwa Waheshimiwa Wabunge, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa awamu, pia kupitia maandiko hayo ili baada ya hapo tuanze ujenzi wa vituo vya mabasi kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwakumbusha Wakurugenzi wa Halmashauri kwamba pamoja na Serikali Kuu kutafuta fedha, lakini fedha za Serikali ni pamoja na fedha za mapato ya ndani. Kwa hiyo, ni wajibu wao kuanza kutenga fedha angalau kwa awamu, kujenga kila mwaka wa fedha wakati Serikali Kuu inatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa stendi hizo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, nadhani hili ni eneo mojawapo ambalo ofisi yako inabidi ilifanyie kazi, kwa maana ya mipango nchi nzima; wapi panahitaji stendi na wapi panahitaji soko? Kwa sababu bila hivyo, uwekezaji wa hizi kila halmashauri mpaka ilete andiko, kila halmashauri itafakari, inakuwa kidogo changamoto, lakini kama Serikali ikiwa na mpango wa kujua wapi panahitaji kwa sasa, inakuwa rahisi hata fedha zikipatikana mnaelekeza nguvu huko, siyo kwa sababu halmashauri imeomba, halmashauri imeleta andiko, ila mpango wa Serikali kupeleka huko stendi, mpango wa Serikali kupeleka huko masoko.

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana hapa wakati mwingine vituo vinaanzishwa, mabasi hayapo; masoko yanaanzishwa, watu hawapo. Kwa hiyo, nafikiri ofisi yako sasa kwa sababu ndiyo imeanza kazi, mtatusaidia kwenye kuifanya nchi yetu isonge kwa pamoja na hizi halmashauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

Na. 71

**Mchakato wa kuanzisha Halmashauri – Sumve**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. KASALALI E. MAGENI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuanzisha Halmashauri ya Wilaya ya Sumve ili kusogeza huduma kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Jimbo la Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala upo kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, maombi ya kuanzisha Halmashauri mpya yanatakiwa kujadiliwa, kuridhiwa na kupitishwa kwenye vikao vya kisheria ngazi ya Vijiji, Kata, Baraza la Madiwani, Kamati

ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa kisha kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa tathmini ya vigezo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu msingi kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Busokelo ukizingatia mpaka sasa ni miaka 10 imepita? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala katika halmashauri zetu. Nawapongeza Halmashauri ya Busokelo kwa kupokea fedha za Serikali Kuu, lakini jengo halijakamilika kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema. Naomba nilichukue hilo nilifanyie kazi tuweze kuona kiasi gani cha fedha hakijapelekwa kwa ajili ya ukamilishaji na tuweze kuweka mpango kazi kuhakikisha kwamba sasa fedha hiyo inapatikana lakini jengo hilo linakamilishwa kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa Busokelo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Charles Muguta Kajege Mbunge wa Mwibara sasa aulize swali lake.

Na. 72

**Kuachwa kwa Wananchi Wenye Sifa za Kunufaika na *TASAF***

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali imewaacha wananchi wengi wenye sifa na vigezo vya kunufaika na *TASAF* katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Jimbo la Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mwibara lipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na lina jumla ya walengwa 5,320 ambao walipatikana kwa mujibu wa taratibu zinazotumika kuwapata Walengwa. Taratibu hizi zinatoa nafasi kupitia Mkutano Mkuu wa Kijiji au Mtaa au Shehia ambapo wananchi wenyewe wanapata nafasi kupendekeza, kuchuja na kuamua juu ya nani wawepo kwenye mpango kwa mujibu wa Mwongozo wa Utambuzi wa Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Toleo la mwaka 2019 na marejeo yake ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, iwapo bado kuna wananchi walipendekezwa kuwa wanufaika ila hawakuingia kwenye mpango, wawasilishe rufaa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na rufaa hizo zitaletwa kwenye Ofisi za *TASAF* Makao Makuu kwa ajili ya mapitio.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa vile mfumo

wa *TASAF* katika Jimbo la Mwibara umekufa, matatizo ni mengi, malalamiko ni mengi; je, ni lini Serikali itafanya upya zoezi la kuwatambua wanufaika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumjulisha Mbunge na pia kulijulisha Bunge lako kwamba mfumo wa *TASAF* haujafa. Tunazo changamoto katika maeneo mbalimbali ambayo kweli yako matatizo hasa katika eneo la utambuzi na uandikishaji wa wanufaika hao.

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie tena kuendelea kuwasisitiza Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako kwamba kama liko tatizo lolote, ofisi zetu zipo kwa ajili ya kusikiliza na kama taratibu zetu zinavyoeleza, kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri yeyote, basi rufaa zitapelekwa hapo na taratibu kwa ajili ya kutatua matatizo au changamoto zinazotokea yatafanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki Mbunge wa Nungwi sasa aulize swali lake.

Na. 73

**Ujenzi wa ukuta maeneo yanayoathiriwa na Bahari Nungwi**

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI** aliuliza:-

Je, sababu zipi zimekwamisha ujenzi wa ukuta maeneo yanayoathiriwa na Bahari Nungwi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mbunge na Mtumishi wa Wananchi wa Jimbo la Nungwi, najibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo mbalimbali ya ukanda wa fukwe wa Bahari ya Hindi. Lakini kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha zoezi la ujenzi wa ukuta wa Nungwi umechelewa lakini kwa sasa Serikali imepata fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imetenga fedha jumla ya shilingi milioni mia sita na hamsini kwa ajili ya kufanya tathmini ya awali ili kuwa na usanifu wa miundombinu itakayosaidia kurudisha ufukwe katika hali ya awali.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwahimiza wananchi wa maeneo ya Pwani kuongeza jitihada za kupanda mikoko, kutofanya uchimbaji holela wa mchanga lakini pia kuhamasisha ulimaji na uvunaji wa mwani usiyoharibu fukwe. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar zitaendelea kushirikiana katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto za uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, swali la nyongeza.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Serikali, ikumbukwe ya kwamba mwaka 2020/2021 niliuliza suala hili hili. Mwaka 2021/2022 nikauliza tena suala hili hili na nikajibiwa kwamba katika bajeti ile litatengwa Fungu Maalum kwa ajili ya kwenda kujenga ukuta ule. Mwaka 2022/2023 nimeishauliza tena suala hili ndiyo kwanza milioni mia sita zimetengwa kwa ajili ya utafiti. Ninachotaka kujua ni lini Utafiti huu utaanza wakati ambapo milioni sita hiyo inauwezo wa kutosheleza kujengea huo ukuta? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili. Kwa kuwa Wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, harakati zao za kiuchumi zimeegemea zaidi katika shughuli za uvuvi na utalii. Mambo ambayo yamekuwa yakitaja ni miongoni ambayo yanapelekea kuharibu na kupelekea athari za mabadiliko ya tabiachi. Je, Serikali ina mpango gani ya kuokoa mazingira ya bahari yaliyosababishwa kutokana na athari za uvuvi na utalii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Simai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, changamoto yetu kubwa katika ujenzi wa ukuta huu ulikuwa ni kuweza kuanza kupata fedha za kuanza kufanya tathimini ya awali. Kwa kuwa sasa fedha zimeishapatikana, tulichokifanya tayari tumeishawasiliana na tumeishawasilisha andiko letu kwa wenzetu Wakala wa Majengo. Kwanza kwa ajili ya kutufanyia Michoro ama Ramani kwa ajili ya aina ya ukuta ambao unatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna kuta za aina nyingi, kuna *gabrion wall*, kuna zile *slope*, kuna zile *vertical*, kuna *blocks*. Sasa tunataka tufanye utafiti tujue ni aina gani ya ukuta ambao wananchi wa pale utaweza kuwasaidia lakini pia umesema tuwatengenezee ukuta ambao utaweza kuwasaidia kuzuia maji lakini pia waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi kama ambavyo Wananchi wako hivyo. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa kwa kuwa taratibu tumeishazianza sasa hivi tunakwenda kuanza hii tathimini ili lengo na madhumuni tuwapelekee ukuta utakao wasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli shughuli zetu za uvuvi lakini na shughuli za utalii zimekuwa zikiathiri mazingira hasa maeneo ya bahari na maeneo ya fukwe. Tayari tumeona kwamba shughuli za uvuvi haramu, shughuli za uvuvi usiyokuwa rasmi lakini shughuli za ulimaji wa mwani na shughuli nyingine zinazofanyika pembezoni ama ndani ya bahari zinaathiri

mazingira. Lakini la kwanza tumeanza kutoa elimu kwa Wananchi ili lengo na madhumuni Wananchi wafahamu ni aina gani ya uvuvi ni aina gani ya shughuli ambazo wanatakiwa wafanye kwenye bahari?

Mheshimiwa Spika, lakini tumeanza kufanya doria, tunashirikiana na wenzetu wa Thumka, wenzetu wa Mji Mkongwe, wenzetu wa Mlemba *Conservation* na wenzetu wengine kupitia Wizara ile ya Uchumi wa Bluu. Lakini kikubwa zaidi tumeanza kuchukua hatua zikiwemo za kuangamiza nyavu na vifaa vyote vinavyoweza kuweza kuathiri mazingira ya bahari, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, sasa aulize swali lake.

Na. 74

**Kutokamilika ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Mwagwila – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, kwa nini ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Kijiji cha Mwagwila haukamiliki ingawa Serikali imetuma fedha nyingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali kupitia Mradi wa *DASIP* ilipeleka fedha za ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Mwagwila yenye ukubwa wa hekta 250. Kazi iliyofanyika ni ujenzi wa banio na sehemu ya mfereji mkuu. Hata

hivyo, kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha mradi huo haukuweza kukamilisha ujenzi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha eneo lote linalofaa linamwagiliwa. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga bajeti kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu wa mradi huu ili kubaini gharama halisi ya kukamilisha ujenzi wa skimu hii. Aidha, ujenzi wa mradi huu utaanza mara baada ya kazi ya mapitio ya usanifu kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa mradi huu ulitumia shilingi bilioni 1.2 na haukukamilika; je, Serikali haioni haja ya kuangalia kilichosababisha kutokukamilika ikiwemo halmashauri kutohusishwa kusimamia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili kwa kuwa Wilaya ya Meatu hatujanufaika na Miradi ya Umwagiliaje je, Serikali pia ipo tayari kutupatia eneo la umwagiliaji katika Kata ya Mwamalole na Mwabuzo eneo moja ambalo tumelipa kipaumbele kama wilaya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba tu nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na changamoto ambazo zilijitokeza awali na mapendekezo ambayo ameteyatoa sasa hivi tu miradi yote tunahakikisha kwamba inashirikisha watu wote ikiwemo halmashauri, Wabunge wa maeneo husika pamoja na Sekretarieti za Mikoa ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika kutekeleza. Kwa hiyo, tumelipokea hilo jambo na tutalifanyia kazi na hata hivyo karibuni tulikaa na Wabunge kuanisha kwenye maeneo ya miradi hiyo kuona namna gani watashiriki katika miradi yao.

Mheshimiwa Spika, la pili, kutoa kipaumbele katika maeneo ambayo ameyataja hapa ikiwemo Mwamalole. Kata ya

Mwamalole nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imepanga kwamba maeneo yote yanayofaa kwa ajili ya umwagiliaji tutayafikia na tutajenga miradi kwa ajili ya Skimu za Umwagiliaji na Mabwawa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwakunipa nafasi niulize swali. Naomba niulize swali moja ni lini Skimu ya Usense itakamilika Kata ya Ulurwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba tu nimuhakikishie Mheshimiwa Anna Lupembe kwamba kwa kuwa ujenzi unaendelea. Sisi tutakachohakikisha ni kum-*push* Mkandarasi aweze kukamilisha kwa wakati mradi huo kama ulivyopanga, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 75

**Kuongeza bei ya zao la chai – Rungwe**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuongeza bei ya chai Wilayani Rungwe kutoka shilingi 340 hadi shilingi 700 kwa kilo hasa ikizingatiwa kupanda kwa gharama za mbolea na madawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha mkulima wa chai anapata bei nzuri Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imedhamiria kuanzisha mnada wa chai nchini ili kupunguza gharama za usafirishaji na uhifadhi wa chai kwenye maghala katika mnada wa Mombasa. Mnada utasaidia upatikanaji wa soko la uhakika kwa wakulima na kuimarisha bei ya chai nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kuchanganya na kufunga chai nchini ili kupunguza utegemezi wa soko la nje. Hatua hii itaendelea kupanua soko la ndani na kuimarisha bei ya chai nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri suala la bei ya chai tumekuwa tukilisemea kwa muda mrefu sana ni kweli katika jibu lako la msingi mnasema kuna mnada wa chai kule Mombasa. Sisi kama Taifa tunajitosheleza kwa chai ya Rungwe, chai ya Njombe na kule Lushoto kwa nini msiweke mnada katika Taifa letu kwa sababu tunao wateja wa kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Umehamasisha Wawekezaji kuwekeza katika chai lakini wapo wawekezaji ambao hawaendi sawa na wakulima maeneo ya Rungwe kwa kutokuwapa pesa zao kwa wakati lakini tu si hivyo wanajiita Wakulima *Estate* lakini wakulima kama wakulima wahausiki ni mradi wa mtu binafsi. Serikali mtachukua hatua gani kuhakikisha jina hilo litumike sawa sawa na wakulima wanavyohitajika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimpongeze Mheshimiwa Mwakagenda kwa kufuatilia suala hilo

la chai na kama tulivyojibu katika jibu letu la msingi, kwamba mkakati wa sasa wa Serikali ni kuhakikisha tunakuwa na mnada ndani ya nchi na kama alivyoainisha yale maeneo yote kwamba tuna maeneo mengi na chai inatosheleza na huo mkakati na ndiyo njia pekee ambayo itatusaidia kuongeza bei na kuimarisha soko la ndani la chai. Kwa hiyo, tumelipokea na tunalifanyia kazi na tutapata majibu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, hukusu hawa wawekezaji ambao hawaendi sawa na Wakulima nitoe tu rai kwamba sisi kama Wizara tutakwenda tutakaa nao ili kuhakikisha kwamba hizi changamoto ambazo zinajitokeza haziendelei tena, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene sasa aulize swali lake.

Na. 76

**Eneo Kisasiga kutumika kwa *Block Farms* – Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutumia eneo la uwekezaji la Kisasiga – Bukene kutengeneza miundombinu ya *Block Farms* kwa kilimo cha alizeti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kutambua na kupima mashamba makubwa mapya 30 yenye jumla ya hekta 200,000 kwa ajili ya uwekezaji likiwemo eneo la uwekezaji la Kisasiga-Bukene, Wilayani Nzega.

Mheshimiwa Spika, eneo la uwekezaji la Kisasiga-Bukene lina jumla ya ekari 48,000 zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za uwekezaji. Aidha, Timu ya Wataalam kutoka Wizara ya Kilimo iliungana na Watalaam wa Halmashauri ya Nzega kufaya upembuzi wa awali pamoja na tathmini ya kina ya udongo katika eneo hilo ili kupata taarifa za kina za afya ya udongo iwapo eneo hilo linafaa kwa kilimo cha Alizeti pamoja na kutengenezwa miundombinu ya *Block Farms.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza. Shamba hili la Kisasiga lenye ukubwa wa ekari 48,000 zoezi la kupima udongo lilishafanyika na lilifanywa na watalamu wa Taasisi ya Kilimo ya *TARI* Mlingano tangu mwezi Agosti, 2021 na majibu yakaja kwamba shamba lile linafaa kwa Kilimo cha Alizeti. Kwa hiyo upimaji umeishafanyika, majibu yameishakuja.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu ni Serikali haioni kwamba sasa hivi kinachotakiwa ni kupeleka Watalam wa Miundombinu ya Ujenzi wa *Block Farm* ili washirikiane na Watalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kufanya tathimini ya Ujenzi wa Miundombinu ya *Block Farm* ili mwaka huu wa fedha unaokuja ibaki tu kutafuta fedha ili kazi ya ujenzi wa *block farm* ianze kwa sababu ekari 48,000 zimekaa *idle* na majibu tangu mwaka 2021 yameishapatika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kama ambavyo tumejibu katika jibu la msingi kwamba kuna Timu ya Watalam wa Wizara na yenyewe imefika katika eneo la Nzega na baada ya hiyo taarifa hatua zote ambazo Mheshimiwa Mbunge amezisema Wizara itazifanyia kazi. Bahati nzuri sana katika kipindi ambacho Serikali ya Awamu ya Sita imewekeza msukumo mkubwa katika kilimo ni kipindi cha Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nimthibitishie tu kwamba shamba hilo litajengwa na Watalam watapelekwa kwa ajili ya kufanya hiyo tathimini ya

miundombinu na katika mwaka wa fedha tutaliweka katika bajeti, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 77

**Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa kuwa Chuo Kikuu kamili**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza

Je Serikali inampango gani wa kupandisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa kuwa Chuo Kikuu kamili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa mujibu wa Sheria ya Vyuo Vikuu vya Tanzania na Mwongozo kuhusu Vyuo Vikuu Tanzania uliotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kukiimarisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa kama Taasisi ya Elimu ya Juu chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kukifanya kuwa Chuo Kikuu kinachojitegemea. Serikali itakipandisha hadhi kitakapokidhi taratibu tulizojiwekea kama nchi na kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili. Kwa kuwa Chuo hiki tayari kina *technical* na *academics staff* zaidi ya 231 wakiwemo zaidi ya Maprofesa 70. Pia huduma mbalimbali toshelezi wapo mpaka wanafunzi wenye mahitaji maalum. Ni kwanini sasa Serikali isitoe kibali chuo hiki kijitegemee na muda maalum wa uwangalizi wa vigezo hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wetu alipokuja katika Mkoa wa Iringa alipoongea na Wazee aliahidi kutoa fedha kupitia Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali ya chuo.

Je, ni lini sasa Serikali itatimiza ile ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa sababu hiki Chuo kinatakiwa kiwe fanisi katika Nyanda za Juu Kusini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika ni kweli Chuo chetu kina Watumishia hao aliowataja Mheshimiwa Mbunge zaidi ya 231 wakiwepo Maprofesa hao 70 lakini kwa vigezo hivi siyo vigezo pekee ambavyo vinatumika kwa ajili ya kupandisha hadhi chuo hiki na naomba nimpe taarifa tu Mheshimiwa Mbunge, Maprofesa hawa waliopo wengi wao ni wale ambao wameazimwa kutoka katika Chuo Mama kile Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Kipekee wale ambao walioajiriwa na Chuo Kikuu cha Mkwawa pale kwa upande wa Maprofesa hatuna hata Profesa mmoja ambaye ameajiriwa kama Mwajiriwa wa chuo kile pale.

Mheshimiwa Spika, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwanza tumebeba ushauri wake, lakini naomba nimuhakikishie Serikali hivi sasa tumepata Mradi wa *HEET* ambao unakwenda

kusomesha Maprofesa na Maprofesa wasaidizi zaidi ya 100 ambao tutahakikisha sasa baada ya mafunzo yao hawa, chuo hiki kinaweza kupandishwa hadhi kuwa Chuo Kikuu kinacho jitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili la upande wa majengo. Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais lakini tumshukuru vilevile Waziri wa Fedha kwa upande wa mapato yetu ya ndani mwaka uliopita wa fedha na mwaka huu wa fedha tumeweza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi pale wa majengo na mpaka hivi ninavyozungumza Wakandarasi wawili wako pale *site* ambae ni SUMA JKT pamoja na Salimu *Construction*. Salimu *Construction* anafanya ujenzi pale wa *hostel* na SUMA JKT wanafanya ujenzi wa *library.*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Mradi wetu wa *HEET* tumeishapeleka pale jumla ya dola za kimarekani milioni nane kwa ajili ya kuongeza miundombinu pamoja na majengo mbalimbali kukifanya Chuo kile kiwe na hadhi ya kupandishwa kuwa Chuo Kikuu kamili, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda.

Na.78

### Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa - Kanda ya Magharibi

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA K.n.y. MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza: -

Je, lini Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, wa Afya Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuanza Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Magharibi ambapo ujenzi utaanza na jengo la huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)*.

Mheshimiwa Spika, ujenzi huu utaanza mwezi Januari 2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Mkoa wa Kigoma uko pembezoni na Hospitali za Rufaa za Kanda zote, ambazo ni za Bungando na Benjamin Mkapa, zipo mbali; Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza kasi kubwa katika kujenga Hospitali hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili; Wakati tukisubiri hospitali hiyo ya Kanda, Je, Serikali haioni umuhimu wa kuimarisha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Maweni, hasa kukamilisha Jengo la Wagonjwa wa Nje *OPD*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba yeye ni shahidi kwa kasi kubwa inayofanyika pale. Leo tumekwenda mimi na yeye kwenye Hospitali ya Mkoa, ameona baadhi ya kliniki sasa zinatoa huduma za kitaifa ambazo zilitakiwa zitolewe Muhimbili, lakini zinatolewa pale kwa sababu ya alichokisema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, pia ameona kiwango ambacho lile Jengo la *OPD* limefika, nakuhakikishia litakwisha. Na kama ambavyo tumesema hapa Mwezi Januari ujenzi wa Hospitali ya

Kanda unaenda kuanza, utaenda kuanza kama tulivyosema hapa na tutahakikisha inaenda kwa kasi kwa kuzingatia uhitaji wa watu wa Kigoma na umbali kutoka kwenye Hospitali za Taifa na zingine za Kanda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kumuuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri;

Je, ni lini Zahanati za Jimbo la Lushoto zitapata vifaa tiba vya kutosha?

**SPIKA:** Hilo ni la kwako au la TAMISEMI? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge, swali lake zuri. Kama ambavyo alishuhudia wiki mbili zilizopita, Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua vifaa mbalimbali. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge nikienda kukaa kwenye kiti changu, aje hapa tuwasiliane na *DM* wake aorodheshe vinavyohitajjika, ili tuweze kupeleka mahitaji *MSD* mara moja, vifaa vianze kupelekwa kwenye Zahanati zake za Lushoto.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Hospitali wa Mkoa wa Simiyu haina uzio kabisa na hospitali ikikosa uzio ni hatari sana;

Je, ni lini Serikali itajenga uzio katika Hospitali ya Mkoa wa Simiyu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimepokea ombi lake la uhitaji wa uzio; lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu kwanza, Hospitali hiyo ya Simiyu ni mpya na iko bado kwenye ujenzi, Tukamalizie kwanza majengo ya kimkakati ambayo bado yanahitajika kujengwa kwenye eneo hili. Tukimaliza tutaelekea kwenye eneo la uzio kama ambavyo yeye Mheshimiwa Mbunge ameshauri, ahsnate sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji; Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Hitaji la Maji Kata za Nalasi – Tunduru Kusini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza: -

Je, lini wananchi wa Kata za Nalasi Tunduru watapata maji ya uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu,

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kata mbili za Nalasi Mashariki na Nalasi Magharibi zenye jumla ya ya wakazi 21,989; na vijiji saba vya Nalasi, Wenje, Lipepo, Mkapunda, Lukumbo, Nasomba na Chilundundu zinapata huduma ya maji kupitia Skimu ya Maji ya Nalasi na Nasomba zilizojengwa mwaka 2012. Katika kuboresha huduma ya maji kwenye kata hizo, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 itafanya ukarabati wa miradi hiyo ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma ambapo utekelezaji wake unatarajiwa

kuanza mwishoni mwa mwezi Novemba, 2023 na kukamilika Februari, 2024.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia katika mwaka huu wa sedha 2023/2024, itafanya utafiti wa maji chini ya ardhi pamoja na kuchimba visima virefu vya maji katika Vijiji vya Nalasi, Wenje na Mkapunda ili kupata vyanzo vya uhakika vitakavyosaidia kujenga mradi mkubwa wa usambazaji maji utakaoweza kuhudumia vijiji vyote vya Kata zote mbili za Nalasi Mashariki na Nalasi Magharibi. Kazi ya utafiti wa uchimbaji visima hivyo, inatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Novemba, 2023 na kukamilika Februari, 2024.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti kidogo. Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Skimu ya Nalasi iligharimu zaidi ya milioni 800 na ilifanya kazi kwa mwezi mmoja, na sasa haifanyi kazi kutokana na matatizo ya kiufundi. Katika kampeni tuliahidi kwamba Skimu hiyo itafanyiwa matengenezo, lakini mpaka sasa hii ni mara ya pili nauliza swali hili naambiwa litafanyiwa maboresho;

Je, ni lini Serikali itafanya maboresho makubwa kwenye skimu ile ambayo imegharimu pesa nyingi na haifanyi kazi, ili wananchi wa Vijiji vya Nalasi, Lipepo na Chilundundu vipate huduma ya maji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mwaka jana mwezi Agosti *RUWASA* Mkoa waliingia makataba na Kampuni ya Chikwale *Company Limited* wa uchimbaji visima 18, pamoja na kisima kimoja kirefu katika Kijiji cha Nalasi na Vijiji vingine vya Azimio, Semeni, Angalia na Mwenge ili kuboresha upatikanaji wa maji, lakini mkandarasi yule mpka sasa hajafanya kazi ya aina yoyote;

Je, ni lini Serikali itapeleka Mkandarasi mwingine mwenye uwezo wakuchimba visima vile ili kuwapatia maji wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Daimu Mpakate, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali linalosema ni lini tutafanya ukarabati wa Skimu hii ya Nalasi; kama nilivyiojibu kwenye jibu langu la msingi; Mheshimiwa Mbunge naomba uamini kwamba sisi tutakuja kukamilisha ukarabati huu kadiri ya muda huu tulioahidi hapa na nitasimamia. Mheshimiwa Mbunge tutafika pamoja katika mradi huu na kuhakikisha unafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali namba mbili, kwamba ni lini Mkandarasi mwingine apatiwe aweze kuchimba visima hivi; naomba niwe nimelichukua tukalifanyie mchakato kuona kwa nini huyu ameshindwa na kuona namna njema ya kuhakikisha visima hivyo vinachimbwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote mliosimama nawaona. Muda wetu hautatosheleza kwenu nyote lakini hao wachache watakaopewa nafasi, usinishukuru nimeshapokea shukarani. Nenda moja kwa moja kwenye swali bila historia.

Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Naibu Waziri, kwanza kwa kuwashukuru namna ambavyo wanatatua kero ya maji katika Jiji la Mwanza hususani Wilaya ya Ilemela. Wamekuja na mkakati wa matokeo ya muda mfupi, wameanza kusambaza *sim tank* katika maeneo yenye changamoto.

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa, mmesimama Wabunge wengi.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba walishafanya *survey* katika maeneo ambyo wanaweza kuchimba visima kwa ajili ya ku-*save* maji hapo;

Je, ni lini visima vitajengwa katika Kata ya Kayenze Mtaa wa Lutongo ambako tayari *feasibility study* imeshafanyika na maji yalipatikana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Angeline Mabula kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumeshafanya *survey* na baadhi ya maeneo katika vijiji hivyo alivyovitaja tumepata maji. Katika eneo la kata aliyoitaja tumepata maji kidogo lakini maji hayo tutahakikisha tutayatumia kujenga vichotea maji vichache ili wananchi wale waweze kupata huduma ya maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya Mradi wa Maji katika Wilaya ya Monduli ambao utapita katika Vijiji vya Mbuyuni, Makuyuni, Losimingoli na Naiti? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa eneo la Monduli kazi mbalimbali zinaendelea kwenye mradi huu na niseme katika mwaka huu wa sedha, tutahakikisha tunakamilisha wananchi waweze kupata maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa wananchi wengi Wilaya ya Nyang'wale wamefungiwa mita za maji na kushindwa kuendelea kutumia maji yale kwa ajili ya mita zao kwenda *speed* sana na kuwa bili kubwa;

Je, Serikali ipo tayari kutuma tume kwenda kuchunguza mita hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'wale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tutatuma wataalam waweze kwenda kuchunguza mita hizo ili wananchi waweze kulipia bili kulingana na matumizi yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa maji wa Ziwa Madunga ulitakiwa usainiwe tangu 15 Oktoba, lakini mpaka leo haujasainiwa;

Je, ni lini mkataba huu utasainiwa ili wananchi wapate maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sillo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa Ziwa Madunga tunatarajia wiki hii Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo tumeweza kuwasiliana ofisini, tutahakikisha mkataba huu unasainiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara sasa aulize swali lake.

Na. 80

**Ujenzi wa Mradi wa Maji - Ngara Mjini**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi mkubwa wa bilioni 41 wa kupeleka maji safi Ngara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu,

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge Jimbo la Ngara Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji inatarajia kutekeleza wa mradi mkubwa wa maji Ngara Mjini kwa gharama ya Shilingi bilioni 41. Usanifu wa mradi huu umekamilika na na unatarajiwa kuhudumia wananchi wapato 170,678 waishio katika Kata ya Ngara Mjini, Kanazi, Kibimba, Nyamiaga na Murukulazo. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha ili utekelezaji wa mradi huo uanze.

Mheshimiwa Spika, kwa mpango wa muda mfupi wa kupunguza kero ya maji katika Mji wa Ngara na viunga vyake, Serikali katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 imetenga kiasi cha fedha shilingi milioni 600. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na uchimbaji wa visima viwili ambapo kisima kimoja kimekamilika, ujenzi wa tanki la ujazo wa lita 250,000 na ulazaji wa mtandao umbali wa kilometa 12 na ufungaji wa pampu mbili za kusukuma maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kwanza turekebishe taarifa kidogo. Jimbo la Ngara linaitwa Jimbo la Ngara na siyo Jimbo la Ngara mjini, naomba turekebishe taarifa.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba wananchi 170,000 wa Ngara Mjini, Kanazi, Kidimba, Nyamiaga na Murukulazo hawana huduma ya maji; na kwa kuwa visima viwili vya milioni 600 vinavyojengwa sasa haviwezi kutekeleza mahitaji ya maji ya wananchi wote hawa.

Je, Serikali ipo tayari kuanza kujenga mradi huu mkubwa wa bilioni 41, kwa kutumia mapato ya ndani yanayotoka Serikali, wakati ikiendelea kutafuta fedha kutoka nje?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Maji alifika Ngara na kuahidi kumlipa Baraka Makogwe hela yake ya fidia ya shilingi milioni 104, ambye bwana huyu ardhi yake uimechukuliwa na Wizara ya Maji nae neo lake limejengwa tenki kubwa la maji na huyu bwana hajalipwa kwa muda mrefu sana;

Je, ni lini, Serikali italipa fedha ya bwana Baraka Makogwe? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mnaozungumza na simu Bungeni; katazo hili nimseshalirejea mara kadhaa. Waheshimiwa Wabunge, msizungumze na simu Bungeni. Heshimuni sehemu yenu ya kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndaisaba, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuweza kutumia mapato ya ndani kuanza mradi wa bilioni 41; Mheshimiwa Mbunge ushauri umepokelewa kwa sababu tumekuwa tukifanya hivi kwenye miradi mingi naamini na hili nalo tutalitupia jicho la ziada.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kulipa fidia, Mheshimiwa Mbunge ahadi ni deni kwa sabbau Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ameweza kuahidi; nikuhakikishie huyu mwananchi atalipwa fidia kadiri ambayo inatakikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa amjibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda sasa aulize swali lake.

Na. 81

**Wananchi wa Namajani kurejeshewa eneo lao - Masasi**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kurejesha kwa wananchi eneo la Namajani - Masasi kwa vile Jeshi la Magereza limeshindwa kuwalipa fidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu,

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wananchi Serikali iliwaelekeza wataalam wa ardhi wa Jeshi la Magereza na wataalam wa ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kupima eneo lililovamiwa na kubaini kuwa na ukubwa wa ekari 2,054 na eneo ambalo halikuwa limevamiwa na wananchi lilikuwa na ekari 1,696.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza kwa sasa linaendelea kumiliki eneo la ekari 1,696 ambazo hazikuwa na mgogoro. Kama hatua ya muafaka wa kumaliza mgogoro, Serikali ilikubali kuwaachia wananchi eneo lenye ukubwa wa ekari 2,054 lililokuwa tayari linatumiwa. Mwafaka huo ulifikiwa kwa kuwashirikisha wananchi wa Kijiji cha Ngalole, uongozi wa wilaya na Mkoa wa Mtwara, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, pamoja na Wizara ya Ardhi kwa kuhakikisha jambo hili limekwisha kwa sababu lilikuwa ni

la muda mrefu. Hata hivyo tunao mgogoro mwingine kwenye Kijiji cha Chingulungulu kati ya Hifadhi ya Misenjesi pamoja na Wanakijiji. Jambo hili nitalileta kama swali la msingi kwa Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sina nyongeza kwenye Wizara hii na niwashukuru kwa kumaliza mgogoro huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stansalaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki sasa ulize swali lake.

Na. 82

**Ukarabati wa Jengo la Mahabusu Gereza la Maswa**

**MHE. STANSALAUS H. NYONGO** aliuliza: -

Je, lini jengo la Mahabusu katika Gereza la Maswa litakarabatiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu,

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Gereza la Maswa ni miongoni mwa magereza makongwe yaliyojengwa tangu kipindi cha ukoloni ambapo miundombinu yake inahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Jeshi la Magereza inaendelea kuyafanyia ukarabati mdogo magereza nchini likiwemo Gereza la Maswa kwa kutumia fedha zinazotokana na vyanzo vya ndani. Gereza la Maswa limepangwa kuanza kufanyiwa ukarabati katika mwaka huu wa fedha 2023/2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stansalaus Nyongo, swali la nyongeza.

**MHE. STANSALAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Gereza la Maswa kama majibu ya Serikali yanavyosema ni Gereza kongwe la siku nyingi na ukarabati inawezekana ukatumia gharama kubwa, na Magereza hii ipo katikati Maswa Mjini;

Je, Serikali ipo tayari tuwapatie kiwanja nje ya mji na lile gereza mkabadilisha ikiwezekana na magereza mengine, yale magereza ya mjini mkayafanya kuwa *business complex* mkapata vyanzo zaidi vya ndani?

Je, mna mpango gani na zile nyumba za wafanyakazi pale Maswa ambazo nazo nazo zina hali mbaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nikiri, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, Magereza ya mjini hasa ile ya Maswa ni kongwe na limechakaa sana. Nikubaliane na yeye tu baada ya Bunge hili ninatarajia kufanya ziara Mkoani Simiyu.

Pamoja na mambo mengine nitatembelea eneo la Maswa. Kama atakuwa na nafasi tukaenda wote tuone namna ambavyo tunaweza tukalifanyia ukarabati Gereza hili au kukubaliana mpango wake wa kupata eneo jingine la kujenga magereza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba tunavyofanya ukarabati wa magereza ni pamoja na majengo yenyewe ya magereza, kwa maana ya mahabusu na vyumba wanavyokaa wafungwa, pamoja na nyumba za watumishi wakiwemo askari. Kwa hiyo, tutakapofanya ukarabati maeneo yote mawili yatazingatiwa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo sasa aulize swali lake.

Na. 83

**Mapitio ya viwango vya malipo ya ujira kwa wapagazi, wapishi na waongoza watalii Hifadhi ya Taifa Mlima Kilimanjaro**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya mapitio ya viwango vya malipo ya ujira kwa wapagazi, wapishi na waongoza watalii Mlima Kilimanjaro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu,

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya viwango vya malipo ya ujira kwa wapagazi, wapishi na waongoza watalii katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Aidha, katika kutatua changamoto hizo, Wizara kwa kushirikiana na vyama vya mawakala wa utalii yaani waajiri imeanza kutekeleza mikakati mbalimbali kwa ajili ya kufanya maboresho ya viwango hivyo vya malipo ya ujira.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo, Wizara imefanya kikao na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na kujadili kuhusu viwango vya ujira kwa wapagazi, wapishi na waongoza watalii.

Mheshimiwa Spika, hatua inayofuata ni Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kufanya kikao kazi baina ya wadau hao na waajiri wao kwa lengo la kupendekeza viwango stahiki, ili viweze kuwasilishwa katika Bodi ya Utatu yenye dhamana ya kumshauri Waziri mwenye dhamana ili makubaliano hayo yawe ya kisheria. Kikao

hicho kinatarajiwa kufanyika katikati ya Novemba, 2023 kule Arusha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, naomba niulize swali moja la nyongeza, ila niruhusu nijieleze kidogo.

Mheshimiwa Spika, wakati kunatokea moto kwenye mlima watu wanaokimbizana kuuzima ni wale wanaoishi kandokando ya ule mlima; pale Marangu wanabebwa, wanasombwa, wanalazimishwa kwenda kuzima moto. Sasa tulikuwa tunaomba Serikali itoe kauli kuhusiana na uwezekano wa kutoa mwongozo ili wale *tour operators* wawe na uwiano fulani tuseme asilimia 70 ya wahudumu wanaopandisha watalii wawe wanatoka kwenye eneo lile la pale Marangu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tunaenda kuufanyia kazi tuone ushauri wa kitaalam utatuelekeza vipi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 84

**Mgogoro wa ardhi Shamba la Malonje – Kwela**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji wa Shamba la Malonje na wananchi wa Kata ya Muungano na Mollo Kwela?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dues Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Malonje linalojulikana kama Shamba Namba 48/1 Malonje katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Manispaa ya Sumbawanga lenye ukubwa wa hekta 10,002 liliuzwa na Serikali kwa mwekezaji ambaye pia ni Bodi ya Wadhamini wa *Efatha Ministry*. Mgogoro wa ardhi katika shamba hili unasababishwa na baadhi ya wananchi kutoka katika vijiji vya Msanda Muungano, Sikaungu na Songambele Azimio katika maeneo ya shamba hili yaliyo ndani ya mipaka kutwaliwa kinyume cha utaratibu.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia suala hili, Serikali iliwasilisha maombi kwa mwekezaji kumega sehemu ya shamba ili igawiwe kwa wananchi na vijiji vinavyozunguka shamba hilo kwa ajili ya shughuli za kilimo. Pamoja na mwekezaji kuridhia kumega sehemu ya shamba lenye ukubwa wa ekari 3,000 ili angalau kila kijiji kipate ekari 1,000 bado wananchi wameendelea kuvamia shamba la mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa uongozi wa Mkoa na Wilaya kusimamia upangaji na ugawaji wa ardhi iliyotolewa na mwekezaji kwa vijiji hivyo ili kuondoa mgogoro uliopo. Aidha, uongozi wa Mkoa na Wilaya uwaelimishe wananchi juu ya kuheshimu mipaka ya ardhi ya mwekezaji kwa kuwa anamiliki eneo hilo kisheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Clement Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa ya swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Bajeti lililopita Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata aliuliza swali juu ya mgogoro huu na ulitoa maelekezo kwamba Waziri afanye utaratibu wa kuja kuangalia mgogoro huu na umalizike. Hata hivyo, nashukuru Naibu Waziri alikuja, jambo lililofanyika ni kutoa maelekezo kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wahakikishe wanashughulikia tatizo hili. Mheshimiwa Naibu Waziri hakupata fursa ya kwenda *field* kuona tatizo na uhalisia wake.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nirudie, naomba tena kupitia Bunge lako, niombe Waziri aje Mkoa wa Rukwa, aende akafuatilie aone uhalisia wa tatizo hili kwa sababu suala la kumuachia Mkuu wa Mkoa limekuwepo tangu miaka 13 iliyopita ambapo Mkuu wa Mkoa, mama yangu Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya analijua vizuri. Ninataka Waziri aje na timu ya wataalam wajifunze vizuri kuliko haya majibu ambayo yanaweza yakachochea hasira na mgogoro zaidi, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini niungane na Mheshimiwa Mbunge kwa *concern* yake ya kupambania wananchi wake.

Naomba nimuahidi tarehe 17 Novemba, baada tu ya Bunge hili nitafika jimboni kwake, nikiambatana na timu ambayo tumeunda *task force* ya wataalam kwa ajili ya kutatua migogoro mikubwa kama hii, kwenda uwandani kuona hali halisi na kutatua tatizo hili mara moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Sengerema, sasa aulize swali lake.

Na. 85

**Ukarabati wa viwanda vya kuchambua pamba – Sengerema**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati viwanda vya kuchambua pamba vya Nyakarilo, Nyamirilo na Buyagu vilivyopo Sengerema?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu la Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, Mbunge wa Jimbo la Sengerema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kuchambua pamba vilivyo na usajili wa Bodi ya Pamba hadi kufikia mwishoni mwa msimu 2022/2023 vilikuwa 92, na kati ya hivyo viwanda 57 vinamilikiwa na kampuni binafsi na 35 ni mali ya Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha viwanda vyote vya kuchambua pamba vinafanya kazi. Serikali kupitia Bodi ya Pamba *(TCB)* mwaka 2020 ilifanya tathmini ambayo imewezesha baadhi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika kupata mikopo kupitia Benki ya Kilimo iliyowezesha kukarabati viwanda vyao. Kupitia utaratibu huo, Serikali itahakikisha pia viwanda vya Nyakarilo, Nyamirilo na Buyagu vinakarabatiwa ili kuongeza tija katika mnyororo mzima wa sekta ya pamba. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwa kuwa viwanda vya Nyakarilo, Buyagu na Nyamirilo havifanyi kazi leo, takribani miaka 21. Huu mpango unaopangwa na Serikali hauoni kama ndio unafifisha zao letu la pamba kwa kuwa Chama Cha Mapinduzi katika Ilani yake imesema ya mwaka 2025 tunakwenda kuzalisha pamba tani milioni moja na tutaboresha viwanda. Leo tunakwenda mwaka wa tatu hakuna kiwanda chochote katika Wilaya ya Sengerema kilichoboreshwa.

Mheshimiwa Spika, haoni kwamba Serikali tayari tena ina mpango wa kupingana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali letu la pili ni kwamba kwa kuwa, viwanda hivi vipo na vinasimamiwa na vyama vya ushirika chini ya Wizara ya Kilimo na ninyi Wizara ya Viwanda ni sehemu ya Serikali. Mko tayari kufuatana na mimi kwenda Sengerema kukagua hivyo viwanda na kuwaeleza wananchi, lini mtaviboresha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ni kweli kabisa kwamba, kumekuwa na changamoto katika sekta ya viwanda hasa viwanda vya pamba katika maeneo mengi kwamba ni viwanda vya siku nyingi na hivyo vimechakaa, na kama alivyosema Mheshimiwa Tabasam, ni kweli Serikali imeshaweka mkakati maalum.

Mheshimiwa Spika, kwanza changamoto iliyokuwepo kabla ilikuwa ni changamoto ya malighafi kwenye viwanda ambavyo vinafanya kazi, lakini sasa kwa sababu ya uzalishaji mkubwa ambao Mheshimiwa Rais ameshaweka fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo, tunaamini kweli kutakuwa na uzalishaji mkubwa kulingana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo sasa pamba hii inatakiwa kulishwa kwenye viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi kama Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tutahakikisha tunapitia na kuona viwanda hivi viaenda kufufuliwa na kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu ziara, ni kweli nitafanya ziara ili nijionee na mimi kama Wizara ya Viwanda tunaoratibu viwanda, lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, ili tuhakikishe sasa mkakati tuliouweka wa kupata mitaji kupitia Benki ya Kilimo, viwanda hivi viweze kufufuliwa ili wananchi wa Sengerema na wengine wanaofanya kazi waweze kunufaika na uwepo wa viwanda hivi, lakini pia kuchochea kilimo cha pamba, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake.

Na. 86

**Hitaji la Minara ya Simu – Msalala**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Msalala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Jimbo la Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imepata mtoa huduma wa kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata ya Ntobo yalipo Makao Makuu ya Halmashauri ya Msalala. Kampuni ya Simu ya Vodacom ndiyo ilishinda zabuni ya kujenga mnara huo kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Vodacom inaendelea na hatua mbalimbali za utekelezaji wa ujenzi wa mnara huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni lini sasa mtaanza ujenzi wa minara hii kwenye maeneo ambayo umeyataja?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwenye maeneo ambayo huduma ya *5G,* naomba nirudie.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo ambayo huduma ya *5G* inapatikana kumekuwa na malalamiko mengi ya juu ya uwekaji wa *bundle* kwisha haraka. Sasa nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanatatua tatizo hili la kwisha *bundle* mapema? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipengele cha kwanza, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi kwamba tayari Vodacom wako katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa ujenzi wa mnara huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kipengele cha pili, naomba nielezee kidogo; ni kweli kabisa, kwanza niseme jambo moja, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali yake inawapenda sana

Watanzania, na kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambayo ndio mlezi wa sekta ya mawasiliano nchini, kazi yetu ni kuhakikisha kwamba tunalinda na kutetea maslahi ya watoa huduma na watumiaji wa huduma. Hivyo, hatutapuuzia wala Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan haijawahi kupuuzia malalamiko ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, nitumie Bunge lako Tukufu kuwaagiza taasisi zetu mbili, taasisi ya kwanza ambayo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* iliyoanzishwa kwa Sheria Namba 12 ya mwaka 2003 kwa kutumia kifungu cha 40 wakashughulikie malalamiko haya ya wananchi kuhusu changamoto za kuongezeka kwa malalmiko ya uongezaji wa *bundle,* lakini linaisha bila kuwa na taarifa rasmi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine, tuna *TCRA CCC;* hii ilianzishwa pia kwa Sheria Namba 12 ya mwaka 2003 ambapo kupitia kifungu cha 37 inampa mamlaka ya kuhakikisha kwamba inalinda haki na maslahi ya watumiaji kwa huduma ya mawasiliano. Hivyo, wakalifanyie kazi hili na watoe ripoti Wizarani, ili sasa kama kutagundulika kwamba kuna changamoto za kiufundi, basi *TCRA* wakafanye kazi kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali kwa kifupi.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kata ya Kikonda, Kinampundu na maeneo ya Kata ya Ilunda yana shida sana ya mtandao. Ni lini Serikali inaenda kujenga mnara katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, changamoto katika jimbo lake ilikuwa kubwa sana, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo tunayaingiza kwenye utekelezaji wa Mradi wa Tanzania ya

Kidijitali, lakini katika kata hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, naomba niipokee ili tukaiingize katika utaratibu wa hatua zinazofuata kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nilete matangazo niliyonayo hapa mbele, tutaanza na tangazo la wageni.

Kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika, wapo wageni wangu ambao ni Balozi Fahad Rashid Al Marekhi, ambaye ni Balozi wa Qatar nchini Tanzania. *(Makofi)*

Karibu sana Mheshimiwa Balozi, lakini ameongozana na Bwana Leonce Ephraim Bilauri ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mashariki na Kati, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Bi. Salma Suleiman Othman ambaye ni Afisa Dawati wa nchi ya Qatar, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Bwana Fawaz Argof Buda ambaye ni Mkalimani, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia, wageni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambao ni Ndugu Tausi Kida ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, karibu sana. *(Makofi)*

Ameongozana na Ndugu Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni mbalimbali pia ambao wako hapa Bungeni ikiwa ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika.

Tunao wageni 30 wa *Pamoja Youth Group* kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Kassim Mpeta, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 29 wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), *Senate* ya Vyuo na Vyuo Vikuu Tawi na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Bony Edward, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 86 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na Mheshimiwa Issa Mtemvu; na hawa ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 27 wa Mheshimiwa Balozi, Dkt. Pindi Chana ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria, na hawa ni watumishi kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ambao ni Kwaya ya Muhubiri KKKT Iguguno, kutoka Mkalama Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Waheshimiwa Mawaziri, nimesimama.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ambayo ni Kwaya ya Muhubiri KKKT Iguguno kutoka Mkalama, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ambaye ni jamaa yake kutoka Shirika la Maendeleo *(RTI),* karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Masache Kasaka kutoka Ofisi ya Mbunge, Lupa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Cecil Mwambe ambao ni viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kutoka Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Ally Kasinge ambao ni wapiga kura wake kutoka Kilwa, Mkoa wa Lindi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Pallangyo ambaye ni mpigakura wake kutoka Kata ya Leguruki, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Jimboni Segerea, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Zulfa Omar ambao ni wamiliki wa maduka ya *Men Destination* kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Kepteni Abbas Mwinyi ambao ni Wanachama wa CCM kutoka Jimbo la Fuoni, Mjini Magharibi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja ambao ni Madiwani kutoka Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dorothy Kilave ambao ni wanachuo wa Chuo cha Diplomasia kutoka Temeke, Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wafanyakazi wa *Royal Massage* kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine hapa na linahusu michezo ambayo timu yetu ya *Bunge Sports Club,* natamani leo nifanye mfano wa kuwatoa nje kidogo Mawaziri ambao hawawezi kunyamaza nikiwa nimesimama, kama wawe wa mfano vile, maana narudia jambo moja wakati huo huo jambo hilo hilo linarejewa sana tena, sasa sijui kama ni mimi sieleweki au ni wao hawaelewi. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ni wao. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa linalohusu michezo; *Bunge Sports Club* na *MATI Super Brands* kutoka Karatu Mkoa wa Manyara. *Bunge Sports Club* ilipata

magoli mawili na timu ya *MATI Super Brands* ilipata goli moja. Kwa hiyo, timu yetu ilifanya vizuri sana na hapa naambiwa wafungaji wa magoli walikuwa Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Festo Richard Sanga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na ratiba yetu kuna mambo nilisema tungeyashughulikia leo. Kwa hiyo, nitawapa dakika chache chache hawa Wabunge halafu nifanye maamuzi ya hayo mambo wawili. Kwanza, tutaanza na hoja ya Mheshimiwa Kasalali Mageni, dakika tatu.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kama ambavyo nilizungumza katika kikao chako kilichopita, kuhusu mchakato wa Serikali wa kuhamisha Kituo cha Maendeleo ya Michezo pale Malya kukipeleka Ilemela na ukirejea kumbukumbu za majadiliano yaliyopita, nilisimama baada ya Mheshimiwa Waziri kuonekana anataka kulipotosha Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nilisema hivyo, nilisema hivyo baada ya kauli ya Mheshimiwa Waziri ya kusema kwamba, namnukuu; "Malya tayari ni *Center for Sports Excellence*." Kwa hiyo, wanataka kujenga *center* nyingine. Waziri huyu alikuwa anazungumza wakati huo huo akijua kabisa kwamba, katika Wizara yake kumekuwa na mchakato wa kuhamisha mradi wa ujenzi wa hiyo *sports excellence* kutoka Malya kwenda Ilemela.

Mheshimiwa Spika, Waziri huyu akiwa anajua kwamba, walisaini mkataba Tarehe 06/07/2023, Wizara yake ilisaini mkataba na Kampuni ya *CRJE* wa kuijenga hiyo *Center for Sports Excellence* Malya. Wakati huo Waziri huyo akiwa anajua kwamba aliandika barua Tarehe 02/06/2023 kwenye Halmashauri ya Ilemela, akiomba eneo kwa ajili ya kuhamisha *sports for excellence*, kutoka Malya kuipeleka Ilemela. Nilizungumza hayo …

**SPIKA:** Ngoja tuelewe vizuri. Barua imeombwa na Ilemela ama imeombwa na Wizara?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Wizara iliiandikia …

**SPIKA:** Samahani, yaani eneo la Ilemela limeombwa na Wizara au ni Ilemela wameomba kituo kijengwe kwao?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, hapana. Tarehe 02/06/2023, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo aliwaandikia Manispaa ya Ilemela kuwaomba eneo kwa ajili ya kuhamishia mradi wa *Sports for Excellence* kwenda Ilemela. Ilemela walimjibu barua hiyo Tarehe 27/07/2023. Ukiangalia hapa ni muda mrefu kidogo tangu aiandike lakini ilikuwa ni siku 21 tu baada ya mkataba kusainiwa. Yaani Katibu Mkuu huyu anaonekana aliomba eneo kabla hata hajasaini mkataba.

Mheshimiwa Spika, alipomaliza kuomba eneo na kuna taarifa zao zinaonesha kwamba, Katibu Mkuu huyu ameandika aliomba eneo Tarehe 02/06/2023 lakini taarifa yake ambayo alimpa Waziri Tarehe 03/06/2023, akionesha kwamba ndiyo yuko kwenye majadiliano ya kuomba eneo Ilemela. Kwa hiyo, ukiangalia mazingira haya yote, inaonekana kulikuwa kuna dalili za kufanya ujanja ujanja.

**SPIKA:** Mkataba umesainiwa tarehe ngapi?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, barua?

**SPIKA:** Mkataba tarehe ngapi?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, mkataba umesainiwa Tarehe 06/07/2023 kati ya Katibu Mkuu na *CRJE*.

**SPIKA:** Huu mkataba umesainiwa na Wizara ikiwepo?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu mwenyewe.

**SPIKA:** Haya, kabla sijamruhusu Waziri, barua ya Tarehe 02 imeandikwa na Katibu Mkuu?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu mwenyewe mwezi wa Sita.

**SPIKA:** Barua ya Tarehe 27 imeandikwa na Mkurugenzi Ilemela?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, imeandikwa na Halmashauri ya Ilemela kuwapa eneo.

**SPIKA:** Sawa. Tarehe 06 mkataba ameingia Katibu Mkuu wa Wizara?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, *yes*. Tarehe 06/07/2023.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana umeeleweka.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo kwa hiyo naweza kuendelea?

**SPIKA:** Umeeleweka.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, *okay* nashukuru.

**SPIKA:** Hoja yako imeshaeleweka. *(Makofi)*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, sawa.

**SPIKA:** MheshimiwaWaziri, dakika tatu.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Kasalali, amesema Wizara iliandika barua kwenda Ilemela tarehe 2 Juni. Wizara hiyo hiyo pia ilisaini mkataba tarehe 6 Julai, kwa hiyo, barua hiyo ambayo anasema Wizara iliiandika ambayo ni sahihi kweli iliiandika, iliandikwa kabla Wizara haijasaini mkataba. Baada ya Wizara kusaini mkataba tarehe 6 Julai, takribani mwezi mmoja na siku nne, Wizara haijaandika barua nyingine.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Kasalali ana barua nyingine ambayo Wizara iliandika baada ya kusaini mkataba, napenda niione. Hivyo, *position* ya Wizara na *position* ya Serikali na ndiyo ambayo niliisema juzi Ijumaa ni kwamba tutaendelea na ujenzi tulioupanga Malya na tutaendelea na ujenzi tutakaoufanya Ilemela na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, barua alizozisema umekubaliana nazo. Tarehe 2 Juni barua ilitoka kwenye Wizara yako, tarehe 06 Julai Wizara yako iliingia mkataba. Tarehe 27, Ilemela ndiyo wamejibu Wizara. Kwa maelezo kama nimeelewa vizuri na utanirekebisha kama sijaelewa. Kwa hivyo, Wizara inasema hivi, Ilemela barua yao ilipochelewa wakaamua kuendelea kuingia mkataba kwenda kujenga Kwimba. Kama hivyo ndivyo, nimekuelewa pia umesema, hakuna barua nyingine iliyoandikwa ya kukana ule mkataba kwamba hamtaendelea kujenga Kwimba. *(Makofi)*

Sasa, jibia kwenye kisemeo ili tuende sawa sawa.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, uko sahihi.

**SPIKA:** Sema tu hiyo hiyo *yes* ili taarifa iingie kwenye *Hansard*.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli baada ya Wizara kusaini …

**SPIKA:** Mkataba.

**WAZIRI UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, Mkataba.

**SPIKA:** Utekelezaji unaendelea.

**WAZIRI UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, bado hatujaenda *site* kwa sababu tunafanya *mobilization* ya fedha lakini utakelezaji utaendelea.

**SPIKA:** Kwa hiyo, kama nimeelewa vizuri, hoja ya Mheshimiwa Kasalali inakuwa haipo kwa sababu Serikali itaendelea na utekelezaji wa mkataba kama ambavyo imeingia Julai mwaka huu. *(Makofi)*

**WAZIRI UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali, hoja yako imekwisha, Hakuna kinachohama kwa sababu Wizara haijasema kwamba inahamisha huo mradi. Kwa hiyo, mradi wako utaendelea. Hili limeisha Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Husna Sekiboko, dakika tatu.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa sababu hoja yangu ilishaingia kwenye *Hansard* tangu Jumamosi, kwa ufupi sana, ilikuwa kuhusu nyimbo za muziki kupigwa kwenye taasisi za elimu kwa maana ya shule za msingi na sekondari na hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa kutokana na jambo hilo. *Case Study* ya jambo hili ni tamko la Serikali au hatua iliyochukuliwa dhidi ya walimu wawili Tunduma, baada ya kupiga muziki kwenye eneo la shule na watoto wadogo kutumbuiza nyimbo ambazo zilikuwa hazina maudhui ya kujifunza shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la hoja hii, Serikali itoe mstari au tamko au kauli kwamba ni nyimbo zipi ambazo zinaruhusiwa na ambazo haziruhusiwi kupigwa kwenye taasisi za shule, kwa maana ya shule za msingi na sekondari na ni hatua zipi ambazo zinaweza zikachukuliwa kama mazingira hayo yakitokea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, dakika tatu ufafanuzi juu ya jambo hilo.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo mafupi sana kuhusu suala la maadili shuleni na haswa suala la nyimbo na miziki inayopigwa shuleni na hatua ambazo Serikali inaweza kuzichukua.

Mheshimiwa Spika, tunalo jukumu la kusimamia malezi shuleni, tunalo jukumu la kudhibiti aina ya miziki inayoruhusiwa shuleni na kukataza miziki ambayo inakiuka maadili ya Kitanzania. Kwa mfano, mtu kupiga miziki ambayo inachochea mambo ya ngono au ku-*promote* pombe au sigara na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo tunalifahamu na tumeshalifanyia kazi na waraka wa mwisho wa Kamishna wa Elimu alisisitiza vilevile, kwa mfano hata kwenye mabasi ya shule, miziki inayopigwa izingatie maadili hayo. Sasa, ni muhimu sana kujua kwamba, siyo kila kitu kinachokubaliwa uraiani kinakubaliwa shuleni. Kwamba, pombe inaruhusiwa uraiani haina maana kwamba pombe itaruhusiwa shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana kuna miziki mingine uraiani imeshaonekana ni ya kawaida, haina maana kwamba itaruhusiwa shuleni. Sisi tuna wajibu huo wa kusimamia mambo hayo na wazazi wanatutaka tufanye hivyo. Natoa wito tena kusisitiza kwamba, wote ambao wanasimamia shule wahakikishe kwamba wana-*vet* kile ambacho kinatumia kama mziki shuleni ili tusikiuke suala letu la maadili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, wale Walimu Wakuu taarifa zilizopo kama ni kweli wewe utatusaidia kufafanua, ni kwamba hawakuwepo shuleni hiyo siku ya tukio. Walikuwepo ama hawakuwepo?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, hilo ni suala la kinidhamu. Kama hawakuwepo wana uwezo wa kukata rufaa kwa Mkurugenzi ambaye ndiye amewaondoa katika mamlaka kwa sababu, hili ni suala la kinidhamu na kama mtu amechukuliwa hatua kinyume na taratibu, kwa mfano hakuhusika moja kwa moja, kuna fursa ya kukata rufaa. Sisi tulitoa

wito kwa Mkurugenzi ambaye ndiye mamlaka yake ya nidhamu pale, achukue hatua. Sasa kama hawakuwepo shuleni wana uwezo wa kukata rufaa kwa Mkurugenzi kwa ajili ya kuchukua hatua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa, Mheshimiwa Waziri, hatua za kinidhamu zina pande mbili. Huyu aliyekosea ana haki ya kusikilizwa. Amesimamishwa kabla hajasikilizwa ama utaratibu ukoje? Kama taarifa za kusema walikuwepo ama hawakuwepo, mimi na wewe tunao uwezo wa kuthibitisha basi tuziseme sasa, lakini kama mamlaka ya nidhamu imechukua hatua kabla ya kujua kuhusu hilo, ilipaswa iwasikilize na walimu. Mheshimiwa Waziri mimi najua ndivyo mnavyofanya huo utaratibu au mnachukua hatua bila kuwasikiliza? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano tu. Kuna *clip* ilikuwa inazunguka watoto wanachapwa vibaya sana kwenye nyayo na sisi tuliagiza Mkurugenzi achukulie hatua. Sisi hatuwezi kwenda kule kumuita Mwalimu na kuangalia nini kinachofanyika. Wale wanajua kabisa mamlaka ya nidhamu, kama unachukuliwa hatua za kinidhamu kuna taratibu za kukata rufaa na kwa haki kabisa na kusikilizwa.

Kwa hiyo, sisi tulitoa wito kwa Wakuu wa shule ile, kwa sababu tukio lenyewe lilitokea Tarehe Sita Mwezi wa Kumi, kulikuwa na muda mrefu umeshapita. Natoa wito kwa Mkurugenzi, kama kweli hawakuwepo shuleni na walikuwa hawana taarifa kilichotokea pale shuleni, wana haki ya kukata rufaa. Nadhani ndiyo utaratibu mzuri sana wa kushughulikia masuala kama hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Sasa, lile la kupigwa nadhani hili limeshaeleweka Waheshimiwa Wabunge. Kama Walimu hawakuwepo shuleni na Mamlaka ya Nidhamu imechukua hatua kabla, basi iwarejeshe kwenye nafasi zao. Ndiyo maana yake. Kama walikuwepo, basi mamlaka iendelee na utaratibu wake kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri hapo kama nimemwelewa vizuri. Kwa sababu, huwezi kuwasimamisha halafu ukataka wakate rufaa ndiyo wajieleze kwamba hatukuwepo. Ilipaswa hizo hatua zichukuliwe kabla. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna hoja nyingine, Mheshimiwa Waziri pale kulikiwa na hoja mbili. Hii ilikuwa ni moja kama mfano. Nafikiri zile hatua mlizozichukua katika mfano uliousema, ule ambao watoto walikuwa wanachapwa bila kuzingatia utaratibu. Mkatoa msimamo ambao ulionesha namna ambavyo utaratibu uko hivi na ndiyo unaotakiwa kufuatwa. Kwa hiyo, hata katika jambo hili mfanye vivyo, kwa nini? Wako Mawaziri humu ndani, tuko na sisi Wabunge, huwa tunacheza mziki na hao wanafunzi, na hizo *clip* zipo. *(Makofi)*

Sasa, kama tutarudi nyuma au tutaanzia hapa tulipoanza ili watu wajue nini cha kufanya. Kwa sababu, la sivyo tutaendelea kucheza huo mziki na watoto wakiwepo shuleni, halafu tunawaponza wale ambao watatakiwa kuchukuliwa hatua. Kwa hiyo, ni muhimu muende hatua zaidi ya hapa ili watu wote wawe wanaelewa ni miziki gani inachezwa, ipi haichezwi itasaidia sana. Kwa hiyo, hilo nadhani ni ile hatua ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Husna Sekiboko, uzuri jambo hili liko chini ya Kamati yako. Kwa hiyo, na ninyi huko mjiridhishe lakini tusiingize huko hisia za dini, tusichanganye imani ya dini na maadili ya Mtanzania, tusivichanganye. Kwa hiyo, Kamati na ninyi kwa sababu ndiyo mnamshauri Waziri, muendelee kushauriana huko namna bora ya kulifanya hili kwa sababu wageni tunaowapata shule ni wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, muangalie nyimbo gani zinapigwa ili mtu ajue anaenda shuleni hizo haziruhusiwi, zipi zinaruhusiwa ili tusiingie mtego kwamba aliyecheza siyo Mbunge, kwa hiyo anaadhibiwa Mwalimu, aliyecheza akiwa Mbunge Walimu hawafanywi chochote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mazingira hayo yataleta mkanganyiko. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, naona ulisimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, tumekusikia kama Serikali na tumesikia *feelings* za Mbunge aliyeleta hoja lakini na za Wabunge. Tunaomba tu sasa agizo lako hili likutanishe taasisi zinazohusika, zilizopewa mamlaka ya kusimamia masuala yote ya nidhamu kwa watumishi na kwa sekta hiyo ya elimu ili waweze kulihitimisha kwa

kutumia taratibu tulizonazo na kila mmoja aweze kutendewa haki inayotakiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nadhani hizo hoja mbili tutakuwa tumezimaliza kwa sura hiyo. Serikali haijahamisha ujenzi wa kituo cha michezo kutoka Kwimba kuelekea Ilemela. Haijahamisha, itaendelea na utekelezaji wa mkataba. Pia, hoja yako Mheshimiwa Husna Sekiboko ambayo ilikuwa na sehemu mbili, sehemu ya kwanza inawahusu wale walimu wawili, ikiwa Mkurugenzi amejiridhisha kwamba hawakuwepo shuleni warejee. Kwa sababu, ukiwaambia wakate rufaa ni jambo ambalo hawajalifanya, kwa hiyo, mamlaka ilipaswa kujua kabla ya kuwasimamisha. *(Makofi)*

Hili la pili kama maelezo tulivyoyasikia ya Serikali, watalifanyia kazi ili taasisi zote ziweke huo utaratibu mzuri ambao kila mtu atakuwa anaujua na sisi Wabunge pamoja na hayo ili tusiwaingize walimu wetu kwenye changamoto, huko tunapoenda kwenye hizo shule.

Jambo lingine ambalo nilisema tutalifanyia kazi leo lakini muda wetu kidogo umetutupa mkono tutalifanyia kazi siku ya Alhamis, ilikuwa ni hoja ya Mheshimiwa Ole-Shangai kuhusu changamoto ambayo ilijitokeza Jimboni kwake, tutaifanyia kazi wakati huo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo anaingia Mheshimiwa Naibu Spika kwa ajili ya kuendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc.* – KATIBU MEZANI:**

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye Kamati ya Mipango. *(Kicheko)*

Waheshimiwa tukae. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaanza na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kanuni ya 113(1) na ya (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2023, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea, kujadili na kushahuri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na kwa namna ya kipekee, naomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua nimsaidie kazi tena katika ofisi yake, katika nafasi hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Imani hii ni kubwa na imenilemea, na iwe deni kubwa kwake. Kupitia Bunge lako tukufu, ninamwahidi Mheshimiwa Rais, utumishi wenye weledi, maarifa, bidii na utiifu kwake, Serikali yake na Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutunukiwa *degree* ya heshima ya Udaktari wa Falsafa, kutoka Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru, mnamo tarehe 10 Oktoba, 2023. Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru ni moja ya vyuo vikuu maarufu India. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kiongozi wa pili katika nchi yetu kutunukiwa *degree* hii baada ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyetunukiwa *degree* hiyo mwaka 1985. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la *The Citizen* lilieleza kuwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametunukiwa *degree* hiyo kwa kutambua mchango wake mkubwa katika kuleta mapinduzi katika sekta za elimu, uchumi, demokrasia na

maendeleo ya wanawake. Kwa mujibu wa mtandao wa *CNBC 18.com*, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni mwanamke wa kwanza kutunukiwa heshima hii na Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru. Mimi naamini kwa kasi ya mageuzi anayoweka katika nchi yetu, tutashuhudia *degree* nyingi zikimiminika siku za usoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani, katika Mkutano mkuu wa 147 wa Umoja huo uliyofanyika Luanda Angola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa na Mwenyekiti wa *IPU*. Mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Spika ametuheshimisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kazi zao njema katika kumshauri na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake na kwa miongozo na maelekezo yao muhimu wanayotupatia sisi wasaidizi wao.

Mhesimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussen Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuiongonza Zanzibar na utekelezaji makini wa Ilani ya CCM kwa upande wa Zanzibar. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussen Ali Mwinyi kwa kutimiza miaka mitatu madarakani kwa mafanikio makubwa yanayoonekana, kushikika na kupimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini (CCM) na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa

Kilindi (CCM) kwa maoni na ushauri wakati wa vikao vya Kamati. Maoni na ushauri wa Kamati umezingatia katika kuboresha mapendekezo ya mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji; Ndugu Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na watumishi wote Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Tume ya Mipango kwa uchapaji kazi wao na ushirikiano wanaonipatia katika kuendesha Ofis ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inawasilishwa katika sehemu kuu sita na kwa sababu ya muda, naomba hotuba yangu pamoja na kitabu viingie katika *Hansard*. Kwa ujumla wake tathmini ya muda mrefu ya uchumi wa nchi yetu inaonesha kuwa, uchumi wa Tanzania umekuwa ukikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia sita kwa mwaka katika kipindi cha miaka 20 mfululizo. Aidha, uchumi wa Tanzania unaonesha hali kubwa ya ustahimilivu katika kipindi cha misukosuko mikubwa ya kiuchumi duniani, ikiwemo ugonjwa wa UVIKO pamoja na vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, bidhaa tunazouza nje na nchi ambazo tunafanya nazo biashara zimebadilika kwa kiasi kikubwa. Miaka 20 iliyopita tumeuza zaidi mazao ya kilimo, wakati sasa mauzo yetu ya nje yanatawaliwa zaidi na mauzo ya madini. Aidha, miaka 20 iliyopita Tanzania tuliuza zaidi bidhaa zetu katika masoko ya Ulaya, Marekani na Afrika, lakini kwa sasa masoko makubwa ya bidhaa zetu yapo nchi za Asia, Afrika na Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake kama ambavyo Benki ya Dunia imeeleza katika taarifa yake ya Septemba mwaka huu 2023 kuhusu uchumi wa Tanzania, Uchumi wa Tanzania unaendelea kuhimili vyema athari za UVIKO-19 na changamoto nyingine za dunia zilizojitokeza katika miaka mitatu iliyopita. Kwa

mujibu wa taarifa hiyo ya Benki ya Dunia, pamoja na changamoto hizo, uchumi wetu umeendelea kuimarika kutokana na sababu kuu tatu. Mosi, utekelezaji wa mageuzi makubwa yanayolenga katika kuchochea na kuimarisha ushindani katika uchumi; pili, kuendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; na tatu, kuendelea kuaminiwa na taasisi za fedha duniani pamoja na wadau wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, imeoneshwa katika sura ya pili ya kitabu ambacho tumewasilisha, lakini niruhusu kwa muhtasari niainishe mafanikio 10 yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/2023 na Robo ya Kwanza ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilitokana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19 na vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine. Viashiria vya uchumi wa nchi yetu vinaendelea kuwa tulivu; pili, kuongezeka kwa matumizi ya mbolea katika kilimo kwa asilimia 46, kutoka tani 393,599 mwaka 2021/2022 hadi tani 503191mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi hiki, eneo la umwagiliaji limeongezeka na kufikia hekta laki nane, ikijumlishwa na lengo la kufikia hekta milioni 1.2 ambalo tumejiwekea. Hatua hii imesababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 17.2 mwaka 2021/2022 hadi tani milioni 20.4 mwaka 2022/2023. Kwa hatua hii utoshelevu wa chakula umefikia asilimia 124 ikijumlishwa na lengo la kufikia asilimia 130 ifikapo mwaka 2025/2026.

Mheshimwa Mwenyekiti, tatu, kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa *SGR* na bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere. Kwa mfano, mwezi Aprili mwaka 2021 wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani, ujenzi wa reli hii ulikuwa katika vipande viwili vya Dar es Salaam mpaka Morogoro, na Morogoro mpaka Makutupora, ikiwa ni asilimia 83.5 na asilimia 57.6 mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Septemba mwaka 2023 ujenzi wa kipande cha kwanza umefikia asilimia 98.6 na kipande cha pili umefikia asilimia 95.4. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imeanza ujenzi wa vipande vingine vipya vitano; Makutupora - Tabora, Isaka - Mwanza, Tabora - Isaka, Tabora - Kigoma, Uvinza - Kitega ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kukuza biashara na uwekezaji ambapo jumla ya miradi 883 ya uwekezaji imesajiliwa; tano, kiwango cha wananchi wanaopata maji safi na salama kimeongezeka kufikia asilimia 88 mijini na asilimia 78 vijijini; idadi ya watalii imeongezeka kutoka watalii milioni 1.7 mwaka 2021 na kufikia watalii milioni 3.8 mwaka 2022; saba, kuongezeka kwa fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini kutoka Dola za Kimarekani bilioni 3.1 mwaka 2021 hadi Dola za Kimarekani bilioni 3.4 mwaka 2022; Nane, tumevuka malengo katika uandikishaji wa wanafunzi katika elimu ya msingi na sekondari hata kabla ya kufika mwaka 2025/2026 katika mpango wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, kiwango cha uandikishaji kwa wanafunzi wa elimu ya msingi kimefikia asilimia 108.5 ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2025/2026. Aidha, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa sekondari, kimeongezeka kutoka asilimia 47.4 mwaka 2021 hadi asilimia 48.2 mwaka 2022 ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia asilimia 48 ifikiapo mwaka 2025/2026; vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 36 kutoka vifo 67 hadi vifo 43 kati ya vizazi 1,000 mwaka 2022; na kumi, idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 hadi kufikia vifo milioni 1.4 kwa kila vizazi 100,000 mwaka 2022. Ikiwa tumevuka lengo la kupunguza vifo kufikia 180 ifikapo mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili tumepiga hatua kubwa sana. Pongezi za kipekee ziende kwa akina mama wawili shupavu. Kwanza ni kwa Rais wetu, mwanamama shupavu sana, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye maelekezo yake na uwekezaji wake mkubwa katika sekta ya afya ndiyo umeleta matunda haya. Pili, pongezi imwendee Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kwa uhodari wake wakuyaelewa na

kusimamia vyema maelekezo ya Mheshimiwa Rais, katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezoea kusema mzigo mzito mpe Mnyamwezi. Kwa mafanikio haya, mimi nasema mizigo mizito wapeni akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niwasilishe mapendekezo ya mwelekeo na maeneo ya kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka ujao. Kama nilivyosema awali, tathmini ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa katika kipindi cha muda mrefu, inaonysha kuwa uchumi wa Tanzania umeendelea kukua mfululizo kwa takribani 6% katika kipindi cha miaka 20 iliyopita. Katika kipindi chote hicho mfumuko wa bei umeendelea kuwa stahimilivu. Aidha, mauzo ya nje ya nchi yameendelea kuongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 975 mwaka 2000 hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 5.91 mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika kipindi chote hiki, mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi yametawaliwa na usafirishaji wa malighafi bila kuyaongezea thamani. Kwa sababu hii, kasi ya ukuaji wa uchumi imekuwa haiendani na kasi ya kupunguza umaskini na kuzalisha ajira, hususan katika maeneo ya vijiji. Kwa sababu hii, tunapendekeza kuwa shabaha kuu ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka ujao na miaka ijayo iwe ni kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi ambayo ni jumuishi, unaopunguza umaskini, unaozalisha ajira kwa wingi, unaotengeneza utajiri na unaochochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufikia shabaha hii, msukumo utawekwa katika kuongezea tija ya uzalishaji na uongezeaji thamani katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini; kuchochea na kuboresha ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote, kuongeza na kuimarisha matumizi zaidi ya teknolojia hususan teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); kuongeza uzalishaji viwandani na kuimarisha huduma bora za jamii kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya jumla ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 ni saba yafuatayo: -

(1) Kuendelea kulinda mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano;

(2) Kuendeleza juhudi za kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula nchini kwa kuendelea kuongeza matumizi ya mbolea, mbegu bora za kilimo na umwagiliaji;

(3) Kuongeza uzalishaji na uuzaji wa bidhaa pamoja na huduma nje ya nchi kupitia sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini;

(4) Kuweka mkazo wa pekee katika kuongeza thamani katika mazao yaliyozalishwa kupitia sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini;

(5) Kuendelea kuongeza, kuboresha na kuimarisha ubora wa huduma za jamii ikiwa ni pamoja na elimu, afya, maji na umeme;

(6) Kuendelea kutanua na kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara, reli, anga na majini na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(7) Kujielekeza kwenye kufungua fursa katika sekta za madini ya kimkakati, *(critical minerals),* uvuvi wa bahari kuu *(deep sea fishing)*, uchumi wa kijani *(green economy)* na uchumi wa kidigitali *(digital economy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya manne ni maeneo yanayokamata kasi duniani kwa sasa na ambayo kwa upande wetu hatujavuna ipasavyo. Izingatiwe kuwa wananchi wetu wengi wanaishi vijijini. Tunazungumzia asilimia 95.1 na kwamba shughuli nyingi za uzalishaji zinategemea kilimo. Aidha, sekta ya kilimo imeajiri asilimia 91 ya nguvu kazi na kwamba kasi ya ukuaji wa uchumi vijijini haiendi sambamba na kasi ya ukuwaji wa uchumi mijini. Ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani

unategemea malighafi kutoka maeneo ya vijijini. Izingatiwe pia kwamba mifumo ya ugharamiaji wa shughuli za kiuchumi hapa nchini haishikamani na shughuli za kilimo vijijini, ambapo mikopo yote ya kibiashara nchini ni shilingi trilioni 22 wakati mikopo inayokwenda katika sekta ya kilimo ni asilimia saba pekee yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, inapendekezwa kuwa katika mipango yetu ijayo ya maendeleo tuweke mkazo maalum katika kuhakikisha kuwa uchumi wa vijijini unakuwa sehemu muhimu ya uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchochea na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii vijijini *(Rural social economic development)* napendekeza kuchukuwa hatua saba zifuatazo: -

(1) Kuendelea kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwapatia wakulima wadogo *(small scale farmers)* mbegu bora na mbolea kwa bei ya ruzuku na kuendelea kupanua na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji; na

(2) Kuweka mazingira maalumu katika kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani *(primary processing)* katika sekta za kimkakati ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatumia sera za kifedha na kikodi ili kuvutia wawekezaji katika maeneo ya vijijini. Ili mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu yatoke vijijini yakiwa yameanza kufanyiwa uchakataji wa awali *(semi-processed)*. Viwanda vya vijijini vitabakisha thamani kubwa kijijini na kutoa nafasi ya ajira kwa vijana na wanawake ambao wengi wao sasa wana elimu ya sekondari. Katika hatua hii, tutahitaji kulipanga upya Shirika la Viwanda Vidogo *(SIDO)*.

(iii) Kuendelea kupanua na kuboresha miundombinu ya huduma za jamii hususani afya, Elimu. maji na umeme;

(iv) Kuhakikisha kuwa angalau asilimia 30 ya wananchi vijijini wanakuwa na Bima ya Afya ifikapo mwaka 2025; *(Makofi)*

(v) Kuweka mkazo wa pekee katika kuimarisha ubora wa Elimu hususani katika kuhakikisha kuwa shule za vijijini zina walimu wa kutosha na bora na kuunganishwa katika miundombinu ya kidigitali; *(Makofi)*

(vi) Kwa kuzingatia umuhimu wa kidigitali katika kuleta mapinduzi ya uchumi vijijini. Ninapendekeza kujenga Mfumo wa Digitali *(Rural Broad Band)* ili kuwaunganisha wananchi vijijini katika uchumi wa Taifa na kuongeza matumizi ya *TEHAMA* katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, hatua hii itawezesha Serikali kuwa karibu zaidi na wananchi kusaidia katika mapambano ya rushwa na kuimarisha Demokrasia na Utawala Bora. *(Makofi)*

(vii) Kupitia upya Sera za Fedha Sheria na Kanuni zinazosimamia mikopo kwa lengo la kuzisukuma Taasisi za Kifedha kuelekeza mikopo katika sekta ya kilimo, ufugaji uvuvi na wachimbaji wadogo wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao Serikali itaweka mkazo katika kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza na kuimarisha ujazo wa fedha za kigeni ili kufikia azima hii njia sahihi na endelevu ni kuhakikisha kuwa tunabadili mwelekeo kutoka kuuza bidhaa ghafi kwenda kuuza bidhaa zilizoongezewa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali ya ushindani duniani katika kuvutia wawekezaji, ninapendekeza kuchukua hatua zifuatazo katika kuvutia uwekezaji wa kimkakati katika uongezaji wa thamani wa mazao mbalimbali:-

(i) Kuweka mkakati wa kulenga masoko makubwa ya nje ili kuwezesha uzalishaji wa bidhaa kwa tija na ushindani kwa lengo la kuimarisha uwezo wa kuuza nje *(Export Led Economy)*. Katika kufikia azima hii tutafanya uchambuzi wa kina ili kuyabaini na kuyaelewa masoko haya ili kujua kwa dhati tunazalisha kwa ajali ya nani na kuzingatia malengo yetu ya muda mrefu; *(Makofi)*

(ii) Kwa kutambua nafasi ya uzalishaji wa nguo na mavazi katika kuzalisha ajira na umuhimu wa zao la pamba nchini katika maisha ya wananchi wetu. Tutatoa msukumo wa pekee katika

kuvutia wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya nguo. Aidha, kwa kutambua kwamba soko la nguo na mavazi ni soko lenye ushindani mkubwa dunia likitawaliwa na majina makubwa katika soko *(brand)* zilizokomaa na kudumu katika soko kwa miaka mingi na kwa kutumia fursa ya wawekezaji wengi wa nguo na mavazi kuanza kukimbilia Afrika kwa sasa. Tutaweka mazingira maalumu kwa lengo la kuvutia kampuni zenye majina maarufu *(brands)* kushirikiana na wazalishaji wa ndani nchini katika kujenga viwanda vya nguo na mavazi hapa Tanzania; *(Makofi)*

(iii) Kuanzisha mtaa wa Sayansi, Teknolojia na Digitali *(Science Technology and Digital Park)* kwa ajili ya kuchochea na kuibua ubunifu na ugunduzi unao hitajika katika mapunduzi ya nne ya viwanda *(Fourth Industrial Revolution);*

(iv) Kwa kuzingatia nafasi ya madini katika kuendelea kukuza ujazo wa mauzo ya nje na kwa kuzingatia umuhimu wa madini ya kimkakati (*Critical Raw Materials)* katika kutimiza azima ya Dunia ya kuzalisha nishati safi na salama kwa mazingira. Tutaweka mazingira mahususi kwa lengo la kuvutia wawekezaji watakao kuwa tayari kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya madini hapa nchini hususani katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha betri za magari na mitambo; *(Makofi)*

(v) Kuweka mkazo katika utekelezaji wa miradi ya kieleezo yenye manufaa na matokeo makubwa katika ukuaji wa uchumi pamoja na ile inayowezesha nchi kutumia fursa ya wakati *(Opportunity of Time)*, miradi hii ni pamoja na;

(i) Kuhakikisha kuwa mradi wa uchimbaji wa Makaa ya Mawe Chuma na madini (*critical minerals)* katika eneo la Liganga na Mchumuma unaanza kutekelezwa;

(ii) Ni kuhakikisha kuwa nchi yetu inaimarisha matumizi ya gesi *(CNG)* katika uendeshaji wa magari ili kuanza kupunguza utegemezi wa mafuta ya kuagiza nje ya nchi;

(iii) Kuweka msukumo maalumu katika miradi ya kuzalisha nishati ili kukabiliana kikamilifu na ongezeko mitaji ya kiuchumi na

kijamiii ikiwemo kukamilisha miradi ya umeme ya Bwawa la Mwalimu Nyerere na Kinyerezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo imejengwa katika nguzo kumi. Tunadhani tunahitaji kuweka nguzo imara ili kusimamia utekelezaji wake tunapendekeza nguzo kumi zifuatazo: -

(i) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi katika nchi yetu na Dunia kwa ujumla; *(Makofi)*

(ii) Kuendelea kudumisha Utawala Bora na Utawala wa Sheria nchini; *(Makofi)*

(iii) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini; *(Makofi)*

(iv) Kuendelea kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara. Katika kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika biashara na uwekezaji tutahakikisha kuwa Serikali inaendelea kujitoa katika kutekeleza huduma na miradi ambayo sekta binafsi inaweza kutekeleza kwa ufanisi zaidi ama kwa uwekezaji wa kawaida ama kwa utaratibu wa ubia. Lengo nikuhakisha kuwa rasilimali za Serikali zinaelekezwa kwenye maeneo ambayo kwa asili yake sekta binafsi haiwezi kutekeleza kwa ufanisi au pamoja na umuhimu wake yanaweza yakawa hayana tija ya biashara; *(Makofi)*

(v) Kuendelea kuhimiri athari za mabadiliko ya tabia ya nchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili;

(vi) Kuwa na rasilimali watu wakutosha na ubora inayokidhi matakwa ya wakati;

(vii) Nidhamu katika matumizi ya fedha za umma;

(viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hususani kwa wafanyabiashara na wawekezaji wadogo na wa kati nchini; *(Makofi)*

(ix) Kuongeza tija ya uzalishaji *(labor productivity)* miongoni mwa watumishi wa umma na wafanyakazi kwa ujumla;

(x) Muhimu kabisa, kuwa na nidhamu ya utekelezaji wa mambo tuliyoyapanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; ninapohitimisha ninaomba kusisitiza mambo matatu. Mosi, ni umuhimu wa kupanga vipaumbele vyetu vyema, suala hili pia liliwahi kusisitizwa na Mheshimiwa Rais, wa Awamu ya Kwanza wa nchi yetu Mheshimiwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika hotuba zake, kwa mfano, akihutubia Mkutano Mkuu wa TANU Tarehe 28 Mei, 1969, ambao ulikuwa mahususi kwa ajili ya kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo pamoja na mambo mengine Mwalimu Nyerere alieleza umuhimu wa kuchangua katika kupanga akisema naomba kunukuu " kupanga ni kuchangua kuweka mpango maana yake ni kuamua jinsi ya kutumia rasilimali iliyohaba maana yake ni kuchagua kutimiza baadhi tu ya shughuli nyingi na zote nzuri kwa sababu haiwezekani kutimizwa zote mara moja. Katika hali zao mbalimbali kila nchi ulimwenguni ina kikomo cha rasilimali inayoweza kuzitumia na ikitumia rasilimali nyingi katika shughuli moja basi italazimika kupunguza rasilimali inayotumika katika shughuli nyingine."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa sisi kama nchi tuna mahitaji mengi lakini rasilimali tulizonazo zina kikomo, kwa sababu hii tunawajibika kuchagua tufanye lipi leo na lipi tufanye baadaye. Hii ndio maana ya "kupanga ni kuchagua" katika kupanga tutazingatia vipaombele vya kimakakati kwa kuzingati dunia inakataka nini na sisi tunaweza kutoa nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni umuhimu wa kujenga maridhiano *(consensus)* ya Kitaifa katika mipango tunayopanga maendeleo ni mchakato endelevu wenye kushirikisha wadau wote katika nchi. Tunachopendekeza hapa ni Mpango wa Maendeleo wa Taifa, siyo Mpango wa Serikali. Hivyo, ni muhimu kuwa na maridhiano ya Kitaifa kuhusu mwelekeo wetu kisera ili sote tushirikiane katika kujenga Tanzania ambayo tunaitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ni umuhimu wa kuwa na watu makini wenye weledi na uzalendo katika utumishi wa umma. Suala hili la kuweka kipaombele kwa rasilimali watu limekuwa likitiliwa msisitizo na viongozi mbalimbali ulimwenguni akiwepo Mheshimiwa Rais wetu. Lee Kuan Yew aliyekuwa Waziri Mkuu nchini Singapore inaaminika ndiye kiongozi aliyeleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi nchini Singapore.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lee, anaamini kuwa kitu cha cha kwanza kinachohitajika katika nchi kuendelea ni watu wazuri ndani ya Serikali. Akihutubia Bunge la Singapore Tarehe 01 Novemba, 1994, kuhusu Mapendekezo ya Mishahara kwa Mawaziri na akieleza umuhimu wa kuwa na viongozi wazuri Serikalini alisema naomba kunukuu" *My experience in Aisa has led me to a different conclusion, to get good governance you must have good men and women in charge of government. I have observed that last 30 years that even with a poor system of government but with good strong men and women in charge people get passable government with decent progress. (Applause)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Lee ni kuwa kuwepo na mifumo na Taasisi nzuri ni muhimu lakini muhimu zaidi ni kuwa na watu wazuri katika kuendesha mifumo na hata Serikali. Ndio kusema hatuwezi kuwa na Serikali nzuri bila ya kuwa na watu wazuri wanaoendesha Serikali. Utawala bora unahitaji Serikali bora na ili uwe na Serikali bora unahitaji watu bora wanaoendesha Serikali. Kwa kuzingatia hili Serikali itaendela kuwekeza katika kuwa na idadi sahihi ya watumishi na umma wenye weledi maadili na uzalendo kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama nchi tunaye Kiongozi Mkuu wa nchi makini anayeonesha weledi na uthibitisho wa uadili wa hali ya juu. Zaidi ya yote amethibitisha kuwa ni kiongozi muugwana na mpenda haki kupitia falsafa yake ya *4R* amejenga maridhianao mapana ya kijamii na kisiasa na kuweka mazingira sawia ya kufanya siasa kwa vyama vyote nchini *(Reconciliation)*. Ametoa uhuru wa kutosha wa kutoa maoni bila uoga wala vitisho hukuakionesha uvumilivu na ustamilivu wa hali ya juu *(resilience)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi wetu ameleta mageuzi makubwa katika kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji *(reform)*. Amefufua sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini na kuwapa matumaini mapya mamilioni ya wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wadogo wa madini. Hakika anaijenga upya nchi yetu *(rebuilding)* na kupitia uongozi wake, Serikali na nchi yetu ipo salama. Naam, hapa ninamzungumzia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, "*Kuzeeka peke yake ndio inaweza kutokea bila kupanga*" lakini maendeleo ya kweli yatatokana na mipango mizuri na nidhamu ya utekelezaji wa mipango hiyo. Akihutubia katika Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM, Dodoma, tarehe 25 Agosti, 2004, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa, alisisitiza umuhimu wa mipango mizuri kwa kusema: "Kuongoza ni kupanga kwanza. Mipango mizuri huleta maamuzi mazuri kimkakati na kiutendaji". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, sisi ndio viongozi wa nchi hii. Tuna wajibu wa kupanga na kupanga vizuri ili mipango yetu hiyo ituongoze kufanya maamuzi sahihi na ya kimkakati. Inawezekana, tutekeleze wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomalizia najua mdogo wangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakuja kueleza Habari za za Bajeti ninaamini yeye atamalizia shukurani ambazo sijazisema kwa kuwapongeza wale jamaa wetu wazuri walioshinda jana. Kwa hiyo, naomba niachie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ninaomba sasa Kamati yako ipokee na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/2025. Mungu Ibariki Tanzania; Mungu Ibariki Afrika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Waziri wa Fedha. Kuna vitu tunaweza kuvitoa toa kwenye Hansard huko mbele. *(Kicheko/ Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa ili kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa uongozi wake mahiri wa kuwatumikia Watanzania. Kazi yake ni yakutukuka na kila mwananchi ameguswa na kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninatambua umahiri wake katika kusimamia utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ili kuboresha huduma za jamii kama ilivyoainishwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Ndio maana wananchi wa Tanzania wanasema mitano tena kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na wamesema mitano tena kwako Mheshimiwa Naibu Spika na wamesema mitano tena kwenu nyinyi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa busara, hekima na weledi katika kazi zake za kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa letu. Kadhalika, nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa - Lindi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi zake za kusimamia shughuli za Serikali hapa Bungeni. Vilevile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb) Naibu

Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusimamia Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Rais wa 31 wa Mabunge Duniani *(Inter Parliamentary Union)* na Rais wa kwanza mwanamke kutoka Bara la Afrika na Tanzania kushika wadhifa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi pamoja na Kamati nzima kwa maoni yao na maoni yao na ushauri wao umezingatiwa katika kuboresha Mapendekezo ya mwongozo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika napenda kutoa kumpongeza Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb) Naibu Waziri wa Fedha na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 ni ya tatu kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama amabvyo maelezo mengine yametolewa na Waziri wa Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yanaakisi juhudi ambazo Serikali ya Awamu ya Sita inachukua katika kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuendelea: kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; kutoa fursa za ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yameainisha masuala mbalimbali, ikiwemo: mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi; vipaumbele vya mpango na bajeti kwa mwaka 2024/2025; usimamizi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti; mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka

2022/2023; mapitio ya utekelezaji wa mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024; na maelekezo yanayotakiwa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na upande wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti: kwa upande wa Mwenendo wa Viashiria vya Uchumi; pamoja na changamoto zilizojitokeza katika kuathiri uchumi wa dunia, uchumi wa Tanzania uliendelea kuimarika kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita ikiwemo utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine; na utoaji wa ruzuku ya mbolea na mafuta ya petroli. Uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.7 kwa Mwaka 2022, na unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.2 Mwaka 2023 na asilimia 5.8 Mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022, na unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.2 kwa mwaka 2023 na asilimia 5.8 mwaka 2024. Aidha, kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2023, Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.3 ikilinganishwa na asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, ukuaji wa uchumi ni matokeo ya uwekezaji wa kimkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita katika miundombinu ya nishati, usafirishaji, huduma za kijamii, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini na shughuli za utalii. Shughuli za kiuchumi zilizochangia kwa sehemu kubwa katika ukuaji wa pato hilo ni kilimo, ujenzi pamoja na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4.6 katika mwaka ulioishia Juni 2023 na umebakia kuwa ndani ya lengo la mtangamano wa nchi za kiuchumi za *EAC* pamoja na zile za *SADC*. Aidha, mfumuko wa bei kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2023 ulikuwa kwa wastani wa asilimia 3.3, ikiwa ni sawa na mfumuko wa bei ambao ulikuwepo kabla ya kuingia kwa mlipuko wa UVIKO 19, ambao upo chini

ukilinganishwa na asilimia 4.7 uliorekodiwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 22.2 kwa Mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na lengo la ukuaji la asilimia 10.7. Ukuaji huo umeongezeka ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.9 tu kwa mwaka 2021. Ukuaji huo unaakisi ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya kwa sekta binafsi kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa baada ya janga la UVIKO–19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Juni 2022 akiba ya fedha za kigeni imeendelea kukidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia Juni 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa ni Dola za Marekani bilioni 5.45 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani bilioni 5.11 za Juni 2022. Kiasi hicho kinatosheleza kuagiza bidhaa za huduma nje kwa kipindi cha takriban miezi 4.9. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi 4.0 na zaidi ya kiwango cha 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na akiba hii ni kubwa kuliko nchi za hapa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2022/2023, kampuni za *Moody's Investors Service na Fitch Rating Services* ziliifanyia tathmini ya uwezo wa nchi yetu wa kukopesheka *(Credit Rating)* na kuchapisha matokeo ya daraja *B2+* na *B2+,* mtawalia. Matokeo haya yanaashiria kuimarika kwa hali ya uchumi, usimamizi wa deni la taifa na uwekezaji pamoja na hatua za Serikali ya awamu ya sita inazochukua katika kufungua shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Aidha, tathmini hii itaiwezesha nchi kutambulika zaidi katika masoko ya fedha ya kimataifa na kuongeza sifa za kuvutia uwekezaji na kupanua wigo wa kupata mikopo kwa Serikali na sekta binafsi ya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya kiuchumi yanapatikana katika Kiambatisho Namba 1 cha Mwongozo wetu; na ninaomba Taarifa yote iingie kama Taarifa Rasmi katika kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/2023 Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya

shilingi bilioni 41,480.6. Hadi Juni 2023 Serikali imekusanya jumla ya shilingi bilioni 38,977.0 sawa na asilimia 94.0 ya lengo. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 26,277.9 mapato ya ndani sawa na asilimia 93.8 ya lengo la mwaka na shilingi bilioni 3,562.9 ni misaada pamoja na mikopo nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/2023 ni pamoja na kupanda kwa bei ya bidhaa mbalimbali, ikiwemo bidhaa za petroli, mbolea na chakula kutokana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine, kudorora kwa uchumi duniani hususan katika masoko ya fedha, uwepo wa baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa kodi kwa kuingiza bidhaa nchini kupitia njia za panya na udanganyifu, ikiwemo magendo. Pia, ukiwemo mwitikio mdogo wa kutoa na kudai stakabadhi za kielektroniki za *(EFD)* wakati wa mauzo; mwisho, mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na changamoto zilizotajwa hapo juu ni pamoja na kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza makali ya bei ya bidhaa za petroli na bei ya mbolea ili kupunguza gharama za uzalishaji na kudhibiti mfumuko wa bei. Serikali ya Awamu ya Sita ni Serikali inayowajali wanyonge na ndiyo maana ilitoa ruzuku katika bidhaa hizo muhimu za mbolea pamoja na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuimarisha doria katika maeneo ya mipakani, kutoa elimu kwa mlipa kodi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki za *(EFD)* na kuanzisha tuzo ya uzalendo kupitia mfumo wa risiti za kielektroniki inayotarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni ili kuendelea kuwavutia wananchi kudai risiti pale wanapokuwa wamenunua bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/2024, mapato yaliyokusanywa katika vyanzo vyote ni shilingi bilioni 9,163.5. Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 6,878.9, sawa na asilimia 95.2 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 7,224.0. Ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi bilioni 10,437.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023 yanapatikana katika Kiambatisho Namba 1 cha Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025, misingi iliyotumika katika kuandaa shabaha za uchumi jumla ni pamoja na kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara, kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili; yaani kama ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko. Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha, kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula hapa nchini, uwepo wa amani, usalama, utawala bora, umoja, utulivu ndani ya nchi pamoja na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi wa maoteo yalifanyika, shabaha na malengo ya uchumi, jumla yatazingatiwa. Haya yatakayozingatiwa ni pamoja na haya yafuatayo;

(i) Pato halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.2 Mwaka 2023 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 Mwaka 2024.

(ii) Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia tatu hadi saba katika kipindi cha muda wa kati.

(iii) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.4 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2024/2025 kutoka uwiano halisi wa asilimia 11.9 uliofikiwa Mwaka 2022/2023

(iv) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 2.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2024/2025 kutoka matarajio ya asilimia 2.7 ya mwaka 2023/2024

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka

nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na la mwisho,

(vi) Kuimarika kwa viashiria vya ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2024. Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 47,424.9. Mapato ya ndani yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 34,436.2, sawa na asilimia 72.6 ya bajeti yote. Aidha, washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia shilingi bilioni 4,291.9, sawa na asilimia 9 ya bajeti. Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 6,141.9 kutoka soko la ndani na shilingi bilioni 2,555 kutoka soko la nje. Maoteo ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2024/2025 yamezingatia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato, matarajio ya ukuaji wa uchumi, hali ya uchumi wa dunia pamoja na mikakati ambayo Serikali inaendelea kuchukua katika kuongeza mapato ya ndani kama ilivyoainishwa kwenye sehemu ya pili ya mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 47,424.9 kwa mwaka 2024/2025. Kati ya kiasi hicho, Deni la Serikali ni shilingi bilioni 12,101.2, mishahara ni shilingi bilioni 11,774.8 na uendeshaji wa shughuli za Serikali shilingi bilioni 8,223.8. Aidha, matumizi kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 15,325.1 ikijumuisha ruzuku ya maendeleo (elimumsingi na sekondari bila ada na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu). Makadirio haya yamezingatia mahitaji ya kugharamia deni la Serikali, mishahara ya watumishi wa umma, uendeshaji wa miradi iliyokamilika ikiwemo miundombinu ya elimu, afya, umeme na maji, ugharamiaji wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mikakati itakayotumika katika kufikia lengo la makusanyo ya mapato ya ndani ni pamoja na kuendelea kutanua wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuhakikisha vyanzo hivyo vinaakisi misingi ya ukusanyaji mapato na kuhakikisha taasisi zenye sura za utoaji wa huduma kwa pamoja vilivyoboresha mifumo ya ukusanyaji vinaendelea na kuwezesha kutoa namba ya malipo

jumuishi ikijumuisha ulipaji wa kodi, ada na tozo mbalimbali kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 yameainishwa katika sehemu ya pili ya mwongozo. Namba ile ya mapato na ile ya matumizi ni namba moja, niliona kuna sehemu watu wanajumlisha na kupata trilioni 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maelekezo mahususi, Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/2025 umeainisha maelekezo mbalimbali kwa Maafisa Masuuli: -

(i) Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa, wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2024/2025 hakutakuwa na bajeti ya nyongeza ambayo itatengwa nje ya bajeti iliyotengwa katika utekelezaji wa mafungu husika.

(ii) Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutoa kipaumbele katika kutenga bajeti za kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuibua miradi mipya kama ambavyo Bunge limeelekeza.

(iii) Maafisa Masuuli waratibu na kushiriki vikao vya kamati za bajeti za mafungu husika.

(iv) Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa na mikakati ya kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika mafungu wanayosimamia

(v) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia majukumu ya msingi ya mafungu ili kuepuka uhamisho wa fedha usio wa lazima na uzalishaji wa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo mangine ya kuzingatia ni kutenga bajeti kwa ajili ya miradi inayoendelea, mchango wa Serikali *(counterpart fund)* katika miradi yenye masharti hayo inayotekelezwa kwa ushirikiano na washirika wa maendeleo, kugharamia

shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kugharamia shughuli za ushirikiano, kuimarisha Muungano na kulipa fidia katika maeneo ya utekelezaji wa miradi ikiwepo na miradi inayojengwa kwa nguvu za wananchi.

(vi) Wizara za Kisekta kutojumuisha bajeti za shughuli za mafungu ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye mafungu yao kwa kazi zinazoelekezwa na mafungu hayo. Aidha, kwa shughuli zinazotegemeana, Mafungu yapange kwa pamoja.

(vii) Kuzingatia Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 kinachoelekeza kutoingia mikataba ya washirika wa maendeleo ya kupokea misaada na mikopo pasipo idhini ya Waziri mwenye dhamana.

(viii) Kuainisha vihatarishi kwenye utekelezaji wa mpango na bajeti na mikakati ya kukabiliana navyo.

(ix) Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa kuweka ukomo wa zabuni zinazoweza kutekelezwa na wakandarasi wazabuni wasio wakazi hapa nchini ili kuwawezesha wale ambao ni wakazi yaani *(local content)* kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi wetu. Aidha, kuhakikisha makubaliano yote na washirika wa maendeleo katika miradi mikubwa yanazingatia ushirikishaji wa wazawa usiopungua asilimia 30 ya gharama ya mradi, asilimia 30 ya gharama ya mradi wapate wazawa.

(x) Kutekeleza miradi yenye mvuto wa kibiashara kwa utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi *(PPP)* ili kupunguza gharama zinazoweza kuepukika kwenye Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kwa kina tumeelezea utekelezaji pamoja na ufuatiliaji na tathimini. Kwa upande wa ufuatiliaji na tathmini baadhi ya vipaumbele ambavyo vimeelekezwa katika taarifa hii ni kuhakikisha kunakuwa na

mpango shirikishi wa ufuatiliaji na tathmini, kuandaa viashiria vya kupima utekelezaji wa malengo ili viwe vipimo vya mafanikio ya taasisi na mradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuweka mifumo thabiti ya ufuatiliaji na tathmini kuhakikisha kuwa mpango na bajeti unaakisi malengo na shabaha na viashiria vya utekelezaji wa mpango wa tatu wa maendeleo wa Taifa kwa Miaka 2021/2022 – 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni kuhakikisha kitengo cha ukaguzi wa ndani kinafuatilia uzingatiwaji wa sheria ya bajeti kuhusu utendaji wa kamati ya bajeti kwa lengo la kupitia na kujadili taarifa na ufuatiliaji wa tathmini na utekelezaji wa kila robo kwa mwaka ili kuweza kuleta uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu maelekezo mahususi ya mwongozo yanapatikana sehemu ya nne ya mwongozo huu. Katika

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha, mapendekezo ya mwongozo yatawezesha kukamilika kwa maandalizi ya bajeti za mafungu kwa wakati, kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani, kuimarika kwa utawala bora na utawala wa sheria na kuongezeka kwa uwajibikaji na ushiriki wa wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi katika uandaaji, utekelezaji wa pamoja na ufuatiliaji wa tathmini ya mpango na bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Maafisa Masuuli wa Wizara, idara zinazojitegemea, wakala za Serikali, ofisi za wakuu wa mikoa, mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi na mashirika ya umma wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu mapendekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango pamoja na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 sambamba na Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango pamoja na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niamba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi; kwa mujibu wa kifungu cha 9(1)(a) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 pamoja na Kanuni ya 113(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 ni mpango wa nne katika mfululizo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 uliobeba dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 kama ilivyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake. Uchambuzi wa Kamati ulifanyika kwa kurejea Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu

wa mwaka 2020, Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Dunia ya mwezi Februari, 2022 inayotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* pamoja na Nyaraka na miongozo mbalimbali ya Serikali inayohusu uandaaji wa Mipango na Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kumi na moja ambazo ni mapitio ya hali ya uchumi, mapitio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya mpango kwa mwaka 2022/2023 na robo ya kwanza 2023/2024, maeneo ya kipaumbele ya mpango kwa mwaka 2024/2025, ugharamiaji wa mpango wa maendeleo wa Taifa 2024/2025, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa, vihatarishi na mikakati ya kukabiliana navyo, mapungufu ya ujumla yaliyobainika kwenye mapendekezo ya mpango wa mwaka 2024/2025, mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka Taifa 2024/2025, maoni ya jumla, na sehemu ya mwisho ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ina lengo la kubainisha maeneo mbalimbali katika mpango na mwongozo yanayohitaji kufanyiwa maboresho kwenye mpango utakaowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo 2050; Dira ya Taifa ya Maendeleo iliyopo hivi sasa inategemewa kufika ukomo mwaka 2025. Hivyo, ni lazima tathmini ya utekelezaji wa dira hiyo ifanyike ikiwa ni maandalizi ya kutunga Dira Mpya ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba Serikali ipo katika mchakato wa kukamilisha tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ili kujenga msingi wa uandaaji wa dira inayofuata. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha tathmini hiyo mwaka huu wa fedha ili itumike kuandaa dira mpya ya 2050. Aidha, Kamati inaitaka Serikali katika mchakato huo kuzingatia maoni ya sekta binafsi, taasisi za elimu, asasi za kiraia na makundi au mtu mmoja mmoja ili dira itakayotungwa iwe na sura ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya hali ya uchumi; Kamati imefanya uchambuzi katika viashiria mbalimbali vya uchumi ambavyo vina athari ya moja kwa moja katika utekelezaji wa mpango na vinahatarisha uwezekano wa kutofikia malengo yaliyowekwa na Serikali. Uchambuzi wa viashiria hivyo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi wa Taifa; uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba uchumi wa Taifa kwa mwaka 2023 unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.2. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia, nchi zilizoendelea, nchi zinazoendelea na zinazoibuka, na nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kushuka hadi kufikia asilimia 3.0, 1.5, 4.0, na 3.3 mtawalia, kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 1. Sababu za kushuka kwa uchumi hizo ni pamoja na kudororo kwa uchumi wa Taifa la China unaotokana na kushuka kwa uwekezaji katika sekta ya mali zisizohamishika *(real estate)*, kupanda kwa bei ya mafuta, athari za UVIKO-19, vita ya Urusi na Ukraine pamoja kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi nyingi duniani unaonesha mwenendo wa kushuka katika mwaka 2023, wakati matarajio ya ukuaji wa uchumi wa Taifa yanaonesha kupanda, Kamati inaishauri Serikali kuweka makisio ya ukuaji wa uchumi yanayoakisi uhalisia wa hali ya mwenendo wa ukuaji wa uchumi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei; Kamati imebaini kwamba bidhaa za chakula na vinywaji baridi zinachangia kwa asilimia 28.2 ya mfumuko wa bei nchini. Kwa kuwa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* imetabiri uwepo wa mvua za El Nino kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba, 2023; na kwa kuwa kipindi hicho ndicho kipindi cha msimu wa kilimo ni wazi kwamba mvua hizo zinaweza kuathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Kamati inashauri Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 kutoa fedha za kutosha kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* kununua chakula cha kutosha ili kukabiliana upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza. Hatua hii iende

sambamba na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa maghala na vihenge ili kuongeza uwezo wa *NFRA* kuweza kuhifadhi chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yanatokana na ukweli kwamba uwezo wa nchi wa kuhifadhi chakula ni tani milioni tatu ambapo Serikali ina uwezo wa tani 500,000 na tani 2,500,000 ni za watu binafsi na Vyama vya Ushirika. Uwezo huu ni mdogo ukilinganisha na mahitaji, hivyo, Serikali ione umuhimu wa kuongeza miundombinu ya kuhifadhi chakula ili kile kitakachonunuliwa kiwe na sehemu ya kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urari wa malipo, biashara na huduma; urari wa jumla wa malipo, biashara na huduma za ziada ya dola za Marekani shilingi milioni 273.5. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ziada hiyo imechangiwa na mikopo kutoka nje. Ziada hii haimaanishi kuwa Serikali ina uwezo endelevu wa kukuza akiba yake ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na ukweli kwamba nakisi katika urari wa biashara ya bidhaa iliongezeka kwa asilimia 54.8 kutoka dola za Marekani shilingi milioni 4,616 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Marekani shilingi milioni 7,100.3 mwaka 2022 kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 2. Ongezeko hili lilitokana zaidi na uagizaji wa bidhaa na malighafi kutoka nje kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine zilizosababisha kuongezeka kwa nakisi ya urari wa biashara, ni mvurugiko wa mnyororo wa ugavi duniani na vita vya Urusi na Ukraine, kupanda kwa bei za bidhaa za mafuta ya kula, petroli na mbolea pamoja na kuongezeka kwa riba katika Soko la Fedha la Taifa la Marekani. Sababu hizi zilisababisha kuongezeka kwa gharama za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje na wakati huo huo bei za bidhaa zinazouzwa nje zikiwemo bei za mazao ya biashara kama vile kahawa na korosho yalishuka bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina ushauri ufuatao ili kupunguza nakisi ya urari wa biashara na kuongeza fedha za kigeni: -

(i) Kwa kuwa Serikali bado inaendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambayo inatumia bidhaa nyingi zinazoingizwa kutoka nje ikiwemo chuma, kuna haja ya Serikali kuweka mkakati mahususi wa kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje hususani utalii na usafirishaji ili kukabiliana na nakisi ya urari wa malipo ya kawaida. Hatua hizo zote kwa pamoja zitachangia kuimarika kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine za kigeni;

(ii) Serikali iboreshe mazingira yatakayowezesha uzalishaji wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa ndani kama vile mafuta ya kula, nyuzi za pamba, sukari ya viwandani, chuma na ngano. Hatua hii itapunguza uagizaji wa bidhaa hizi kutoka nje na kulinda akiba ya fedha za kigeni;

(iii) Kuendelea kufanya mapitio ya Sera za Kodi ambazo zitachochea matumizi ya bidhaa zinazozalishwa ndani kuliko zile zinazoagizwa kutoka nje ambazo zinaweza kuzalishwa nchini; na

(iv) Serikali iongeze uwekezaji pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara katika sekta za utalii na madini kwa kuwa zina muitikio wa haraka katika viashiria vya kiuchumi na zinaongoza kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa sekta binafsi imekua kutoka asilimia 9.9 mwaka 2021/2022 hadi kufika asilimia 22.2. Ukuaji huu umevuka lengo la Tamko la Sera ya Fedha la mwaka 2022/2023 la asilimia 10.3. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli za kilimo iliongezeka kwa asilimia 44.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji huu ulichangiwa uwepo wa dirisha la shilingi trilioni moja lililofunguliwa na Benki Kuu ambapo hadi kufikia mwezi Septemba, 2023 kiasi kilichokuwa kimetolewa ni shilingi bilioni 194.87 ili kuhamasisha benki za biashara kukopesha sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni dhahiri kwamba bila uwepo wa dirisha hili, kungekuwa na mikopo michache kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kilimo ukizingatia vihatarishi vilivyopo katika sekta hii. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhamasisha Benki Kuu kuendeleza uwepo wa dirisha hili muhimu ili kuchochea mikopo kwa sekta ya kilimo na kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa pamoja na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya riba; kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya riba ya mikopo na mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei nchini ulifika asilimia 4.6 katika mwaka ulioishia Juni, 2023. Wakati riba za mikopo zilikuwa ni asilimia 16.04 ikiwa ni mara 3.5 ya mfumuko wa bei na tofauti ya takribani asilimia 8.4 ikilinganishwa na riba za amana ambazo kwa kipindi hicho ilikuwa asilimia 7.64. Kamati inaamini kwamba viwango hivi vya riba pamoja na ada na tozo kubwa kwenye miamala ndio chanzo cha faida kubwa kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya gharama za uendeshaji wa mabenki nchini na kubaini chanzo cha riba kubwa ili kusaidia kupunguza riba za mikopo na tozo za miamala na hivyo kuhamasisha wananchi wengi zaidi kutumia huduma za kibenki. Vilevile Kamati inashauri riba za mikopo kwa watumishi wa umma na waliopo kwenye ajira rasmi na za kimkataba zipunguzwe kutokana na ukweli kwamba mikopo kwa watumishi wa umma inalipwa na waajiri moja kwa moja kutoka kwenye mishahara, na hivyo uwezekano wa kutolipika ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Deni la Serikali; uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba uwiano wa ulipaji wa deni kwa mauzo ya nchi unakaribia ukomo wa asilimia 15 ambapo hadi Juni, 2023 uwiano huu ulikuwa asilimia 14.1. Mwenendo huu una athari kwenye akiba ya fedha za kigeni ukizingatia kwamba takribani asilimia 58.7 ya Deni la Serikali ni deni la nje ambalo hulipwa kwa fedha za kigeni. Hivyo, endapo mauzo ya nchi hayawezi kukidhi malipo ya deni basi italazimika kutumia akiba ya fedha za kigeni kulipa deni na hivyo kupunguza uwezo wa nchi kuagiza bidhaa na huduma nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi za kuchochea mauzo ya nje kwa kuongeza mauzo ya mazao ya kibiashara yalioongezewa thamani, kuchochea uzalishaji wa bidhaa za viwandani, kukuza sekta ya utalii pamoja na huduma ili kuimarisha akiba ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Mpango kwa mwaka 2022/2023 na robo ya kwanza 2023/2024; Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2022/2023 ulitengewa jumla ya shilingi trilioni 15.0 sawa na asilimia 36.1 ya Bajeti ya Serikali. Hadi mwezi Juni, 2023 jumla ya shilingi trilioni 13.9 zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia 93.1 ya lengo. Uchambuzi wa utekelezji wa miradi mbalimbali ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 4281, Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa *(SGR);* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ukiwemo mradi huu wa reli ya kisasa *(SGR)*. Hata hivyo, ili reli hiyo iendeshwe kwa ufanisi na kuleta manufaa ni lazima urefu usipungue kilometa 400. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kukamilisha haraka kipande cha reli kinachounganisha Bandari ya Dar es Salaam na kipande cha Morogoro hadi Makutupora kilometa 722, ili reli hiyo ianze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii itaisaidia Serikali kuanza kukusanya mapato kutoka kwenye mradi huu, hasa ukizingatia kwamba mikopo iliyotumika kujenga reli hii inakaribia kuiva. Vilevile Kamati inashauri masuala yafuatayo: -

(i) Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ihakikishe inatafuta fedha za kutosha ili kuziba pengo la ufadhili wa mradi kwa ajili ya uendelezaji wa mradi. Kutokufanya hivyo kutasababisha ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi ambao wameshakabidhiwa loti mbalimbali;

(ii) Serikali ijielekeze kutumia mikopo yenye masharti nafuu na masharti ya kati katika ujenzi wa reli hiyo ili kuepuka

matumizi ya mikopo ya kibiashara ambayo ina riba za juu na inaiva katika kipindi cha muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya barabara; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu wa ulipaji wa madai ya wakandarasi wa barabara nchini. Kuanzia mwezi Agosti, 2023 Serikali imekuwa ikitoa shilingi bilioni 70 kwa ajili ya kulipa wakandarasi. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 50 ni kwa ajili ya wakandarasi wa ndani na shilingi bilioni 20 wakandarasi wa nje. Hatua hii inaenda kupunguza hati za madai na riba zinazotokana na ucheleweshaji wa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa miradi yote ya barabara iliyotolewa Taarifa ya utekelezaji katika Mapendekezo ya Mpango na kulinganisha na utekelezaji wa miradi hiyo katika Mipango ya mwaka mmoja mmoja iliyopita dhidi Mpango wa Miaka Mitano na kubaini masuala yafuatayo: - *(Makofi)*

(i) Miradi mingi ya barabara imekuwa haikamiliki kwa wakati;

(ii) Baadhi ya barabara zimekuwa zikitolewa taarifa miaka ya nyuma na hazijakamilika ila taarifa zake hazionekani katika taarifa ya utekelezaji wake katika Mapendekezo ya Mpango;

(iii) Serikali imeingia mikataba mingi ya vipande vya barabara wakati vipande vilivyopo katika barabara hiyo hiyo utekelezaji haujafikia hata asilimia 50;

(iv) Serikali kufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya barabara ambayo utekelezaji wake hautarajiwi kuanza ndani ya muda mfupi na hivyo kulazimika kurudia kufanya tena upembuzi pindi mradi unapotaka kuanza kutekelezwa ikiwa muda mrefu umepita tangu upembuzi wa awali ulipofanyika;

(v) Serikali kutozwa riba kutokana na kuchelewa kwa kulipa hati za madai ya wakandarasi;

(vi) Barabara kujengwa chini ya kiwango na hivyo kulazimu matengenezo ya mara kwa mara muda mfupi baada ya barabara kukamilika;

(vii) Usimamizi usioridhisha wa magari yanayozidisha uzito na hivyo kusababisha uharibifu wa barabara na madaraja;

(viii) Baadhi ya wakandarasi kushindwa kutekeleza miradi kutokana na kutolipwa kwa wakati na kupewa miradi mingi bila kupima uwezo;

(ix) Urefu wa barabara kubadilika katika taarifa mbalimbali za Serikali; na

(x) Uwepo wa wakandarasi wasiokuwa na uwezo .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uchambuzi huo, Kamati ina ushauri ufuatao: -

(i) Ujenzi wa miradi ya barabara kupimwa kwa ufanisi wa kila barabara kwa kulinganisha urefu uliokuwa umepangwa kujengwa katika mwaka husika. Hali ilivyo hivi sasa taarifa inayotolewa hujumuisha maeneo yaliyokamilika katika mwaka wa fedha uliotangulia na hivyo ni vigumu kupima ufanisi;

(ii) Upembuzi yakinifu wa barabara ufanyike pale tu ambapo Serikali ina nia ya kuanza ujenzi wa barabara husika;

(iii) Barabara zenye manufaa ya kiuchumi na za kimkakati zipewe kipaumbele;

(iv) Kupima uwezo wa wakandarasi kabla ya kuwapa zabuni za ujenzi wa barabara; na

(v) Kulipa kwa wakati madeni ya wakandarasi, ili kuepusha ongezeko la riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 3172, Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere MW 2,115; Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia katika kutekeleza mradi huu ambapo hadi kufika mwezi Julai, 2023, Serikali ilikuwa imeshamlipa mkandarasi asilimia 84.23 ya gharama zote za mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwake kutaletea Taifa manufaa makubwa ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa umeme wa uhakika. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza mradi huu wa kimkakati wenye manufaa mapana kwa taifa. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba mradi huo unakamilika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 3171, Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga; Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 15.0 kati ya shilingi bilioni 15.4 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi 1,048 kati ya wananchi 1,144, sawa na asilimia 97.3. Duniani kote ni nadra sana kukuta makaa ya mawe na chuma kuwa kwenye maeneo yanayokaribiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali miradi hii ilipangwa kutekelezwa kwa pamoja ili Makaa ya Mawe ya Mchuchuma yatumike kuyeyushia Chuma cha Liganga. Hata hivyo, Kamati imebaini Serikali ina nia ya kutenganisha miradi hii kwa kuanza kuchimba makaa ya mawe kwa sababu yamepanda bei katika Soko la Dunia. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi hii kwa pamoja kama ilivyokuwa imepangwa awali ili kuleta manufaa yaliyokusudiwa pamoja na kupunguza gharama za miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usambazaji wa Nishati ya Umeme Vijijini; Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya kupeleka umeme vijijini ambapo vijiji 10,987 kati ya vijiji 12,318 vimeunganishwa na umeme sawa na asilimia 89.19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa

kuendelea kuwahakikisha wananchi waishio vijijini wanatumia nishati ya umeme kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inaona ni vyema kukamilisha vijiji vilivyosalia 1,331 kabla ya kuelekeza kiasi kikubwa cha fedha kwenye vitongoji vilivyopo kwenye vijiji ambavyo vina umeme. Mfumo huo wa utekelezaji wa mradi unaathiri fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha vijiji vilivyosalia. Kamati inaishauri Serikali kutokuanza miradi mipya mpaka pale itakapohakikisha kuwa mradi wa awali umekamilika kwa asilimia 100. Hatua hii itasaidia sio tu kupima ufanisi, lakini vilevile kukamilika kwa maeneo yote ya mradi na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi Na. 6360, Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge. Kati ya miradi iliyopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Bunge ni pamoja na utwaaji wa maeneo yanayozunguka Bunge. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa daftari la uthamini ambalo limeshawasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fidia inalipwa kwa maeneo yanayomilikiwa na watu binafsi mapema iwezekanavyo ndani ya muda wa miezi Sita uliowekwa kisheria kuisha. Hatua hii itasaidia kuepuka kurudiwa kwa zoezi la tathmini ambalo litasababisha kuongezeka kwa gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi Na. 6501, Vitambulisho vya Taifa. Kamati katika nyakati tofauti imekuwa ikifuatilia na kutanzua changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(National Identification Authority-NIDA)* kuhusu uchapishaji wa Vitambulisho vya Taifa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwezesha ulipaji wa deni la mzabuni la jumla ya dola za Marekani milioni 7.6 sawa na shilingi bilioni 17 na kusamehe kodi kwenye kadi zinazotumika katika uchapishaji wa vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizi zote, vitambulisho vilivyochapishwa katika muda wa mwaka mmoja ni 1,849,931 na hivyo kufikisha jumla ya vitambulisho vilivyochapishwa kuwa 12,863,269 kati ya idadi ya watu 24,083,933 waliosajiliwa na kupewa namba ya utambuzi ikiwa ni sawa na asilimia 50 ya waliotakiwa kupewa vitambulisho tangu

kuanzishwa kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Gazeti la Serikali, Namba.122 la Tarehe 01/08/2008).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba mtambo uliosimikwa katika kiwanda cha kuchapisha vitambulisho vya *NIDA* una uwezo wa kuchapisha vitambulisho 4,500 kwa saa. Kwa vile upatikanaji wa kisilikoni *(chip)* za vitambulisho Duniani si changamoto tena, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba watu wote waliosajiliwa na wanaostahili wanapewa vitambulisho vyao. Aidha, wananchi ambao vitambulisho vyao vimekwishatolewa na hawajavichukua wahamasishwe kwa kutangaza orodha ya majina yao na eneo ambapo vitambulisho vyao vipo ili waweze kuvichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye maeneo ya kipaumbele ya mpango kwa mwaka 2024/2025. Mapendekezo ya mpango wa mwaka 2024/2025 yanatoa kipaumbele katika kukamilisha miradi na programu za maendeleo ambazo hazikukamilika katika Mipango iliyopita. Hatua hii inamaanisha kwamba miradi mipya itakayotekelezwa ni ile yenye matokeo ya haraka ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi kulingana na rasilimali zilizopo na mazingira ya uchumi duniani. Kamati imefanya uchambuzi kwenye maeneo ya kipaumbele na kubaini masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kielelezo. Miradi ya kielelezo iliyoainishwa kwenye mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2024/2025 ni michache ikilinganishwa na miradi ya kielelezo iliyoainishwa kwenye mpango wa miaka Mitano, (2021/2022 – 2025/2026). Miradi ambayo hijaorodheshwa ama haijatekelezwa au inatekelezwa kwa kusuasua. Miradi hiyo ni:

i) Mradi wa kufua umeme wa maji wa Rumakali (*Megawatt* 222);

ii) Ununuzi wa meli kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu;

iii) Ujenzi wa reli ya Mtwara - Mbamba *Bay* na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa kiwango cha kimataifa *(SGR)*; na

iv) Mradi wa Magadi Soda Engaruka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba miradi hii inaendelea kuwa ya kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2024/2025. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 15.32 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 32.32 ya bajeti yote ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kutoka shilingi trilioni 14.077 mwaka 2023/2024 hadi shilingi trilioni 15.325 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 8.8 (Trilioni 1.248). Kamati inaipongeza Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuhakikisha kwamba inatenga kati ya asilimia 30 hadi 40 ya bajeti kwa ajili ya maendeleo kama inavyoonekana katika jedwali Namba Tano, Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye maoni ya jumla. Miradi ya kilelezo ya muda mrefu ambayo haijakamilika. Kamati imefanya uchambuzi wa miradi ya kielelezo ambayo imekuwa haitekelezwi kwa muda mrefu ili kubaini changamoto zinazoikabili. Miradi hiyo ni Mradi wa Magadi Soda Engaruka, Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga, Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo, Mradi wa kufua umeme wa maji wa Rumakali, Mradi wa kufua umeme wa maji wa Ruhuji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda siyo rafiki sana naomba niende kuhitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU),* hakika umethibitisha uwezo wako kwa Taifa na Kimataifa katika kusimamia shughuli za Kibunge. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge

na Naibu Spika kwa ushirikiano wake na Kamati katika kipindi chote cha utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko Naibu Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Rais Kushika wadhifa huo, Tunaamini chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mtakuwa nguzo imara katika kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru Mheshimiwa, Prof. Kitila Mkumbo, Mbunge Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Mbunge, Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao na Kamati. Aidha, Kamati inawashukuru Dkt. Natu Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na Ndugu Lawrence Mafuru Katibu Mtendaji Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2024/2025 pamoja na Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri na ushirikiano wao katika kuchambua Mpango na Mwongozo ili kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nimshukuru pia Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati Ndugu Lilian Masabala, Ndugu Wilfred Akasi, Ndugu Jenifer Maurice na Ndugu Trifina Karaguza,

kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante.*(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/25 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25 - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa Mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele (a) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 pamoja na Kanuni ya 113 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 ni Mpango wa nne katika mfululizo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) uliobeba Dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa 2024/25 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 kama ilivyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake. Uchambuzi wa Kamati ulifanyika kwa kurejea Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021/22-2025/26), Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/23, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Dunia ya mwezi

Februari, 2022 inayotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) pamoja na Nyaraka na miongozo mbalimbali ya Serikali inayohusu uandaaji wa Mipango na Bajeti.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kumi na moja ambazo ni Mapitio ya Hali ya Uchumi, Mapitio ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Mpango kwa Mwaka – 2022/23 na Robo ya Kwanza 2023/24, Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango kwa Mwaka 2024/25, Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2024/25, Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa, Vihatarishi na Mikakati ya Kukabiliana navyo, Mapungufu ya Ujumla yaliyobainika kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Mwaka 2024/25, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka Taifa 2024/25, Maoni ya Jumla, na sehemu ya mwisho ni Hitimisho.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Taarifa hii ina lengo la kubainisha maeneo mbalimbali katika mpango na mwongozo yanayohitaji kufanyiwa maboresho kwenye Mpango utakaowasilishwa.

### 1.1. Maandalizi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Dira ya Taifa ya Maendeleo iliyopo hivi sasa inategemewa kufika ukomo mwaka 2025. Hivyo ni lazima tathmini ya Utekelezaji wa Dira hiyo ifanyike ikiwa ni maandalizi ya kutunga Dira Mpya ya Taifa. Kamati imebaini kwamba Serikali ipo katika mchakato wa kukamilisha tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ili kujenga msingi wa uandaaji wa Dira inayofuata. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha tathmini hiyo mwaka huu wa fedha ili itumike kuandaa Dira mpya ya 2050. Aidha, Kamati inaitaka Serikali katika mchakato huo kuzingatia maoni ya sekta binafsi, taasisi za elimu, asasi za kiraia na mtu mmoja mmoja ili dira itakayotungwa iwe na sura ya Kitaifa.

## 2.0. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi katika viashiria mbalimbali vya uchumi ambavyo vina athari ya moja kwa moja katika utekelezaji wa Mpango na vinahatarisha

uwezekano wa kutofikia malengo yaliyowekwa na Serikali. Uchambuzi wa viashiria hivyo ni kama ifuatavyo: -

### 2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 yanaonesha kuwa ukuaji wa uchumi wa dunia umepungua kutoka **asilimia 6.3** mwaka 2021 hadi **asilimia 3.5** mwaka 2022. Kushuka kwa ukuaji wa chumi za nchi zilizoendelea ambazo tunafanya nazo biashara pia ni wabia wetu wa maendeleo, kutaathiri ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kukabiliana na hali hiyo ili uchumi wa Tanzania usitetereke.

### 2.2. Ukuaji wa Uchumi wa Taifa

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba uchumi wa Taifa kwa mwaka 2023 unatarajiwa kukua kwa **asilimia 5.2.** Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa Dunia, nchi zilizoendelea, nchi zinazoendelea na zinazoibuka, na nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kushuka hadi kufikia **asilimia 3.0, 1.5, 4.0,** na **3.3** mtawalia, kama inavyoonekana kwenye **jedwali namba 1**. Sababu za kushuka kwa chumi hizo ni pamoja na kudororo kwa uchumi wa Taifa la China unaotokana na kushuka kwa uwekezaji katika sekta ya mali zisizohamishika *(Real Estate)*, kupanda kwa bei ya mafuta, athari za UVIKO-19, vita ya Urusi na Ukraine pamoja kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, uchumi wa nchi nyingi duniani unaonyesha mwenendo wa kushuka katika mwaka 2023, wakati matarajio ya ukuaji wa uchumi wa Taifa yanaonyesha kupanda. Kamati inaishauri Serikali kuweka makisio ya ukuaji wa uchumi yanayoakisi uhalisia wa hali ya mwenendo wa ukuaji wa uchumi duniani.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia (%)**

| KUNDI/MWAKA | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | MATARAJIO | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 023 | 2024 |
| Dunia | 3.6 | 2.8 | -2.8 | 6.3 | 3.5 | 3.0 | 2.9 |
| Nchi zilizoendelea | 2.3 | 1.7 | -4.2 | 5.6 | 2.6 | 1.5 | 1.4 |
| Nchi zinazoendelea na zinazoibukia | 4.7 | 3.6 | -1.8 | 6.8 | 4.1 | 4.0 | 4.0 |
| Nchi zinazoendelea na zinazoibukia Kiuchumi za Bara la Asia | 6.5 | 5.2 | -0.5 | 7.5 | 4.4 | 5.3 | 5.0 |
| Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara | 3.2 | 3.3 | -1.7 | 4.7 | 4.0 | 3.3 | 4.0 |

***Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25***

## 2.3. Ukuaji wa Uchumi wa Nchi za Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** pamoja na kwamba nchi ya Rwanda ni moja kati ya nchi 4 za Afrika ya Mashariki zenye mfumuko mkubwa wa bei, vilevile ni moja kati ya nchi zenye kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi kati ya nchi zote za Afrika Mashariki (rejea jedwali namba 2 na namba 3). Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ukuaji wa uchumi wa Rwanda umechangiwa zaidi na sekta binafsi, kwa mfano mwaka 2022 sekta ya huduma ukiondoa huduma zinazotolewa na Serikali imechangia **asilimia 30.8**, kilimo kimechangia **asilimia 25** na uzalishaji viwandani **asilimia 10.4**. Ukuaji wa sekta hizi unadhihirisha kwamba sekta binafsi ndio inayochangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa Rwanda na kusaidia utengenezaji wa ajira na kupunguza umaskini kwa wengi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati pia umebaini kuwa sekta zinazokua kwa kasi nchini ni Madini (**asilimia 10.9**), Fedha na Huduma (**asilimia 9.2**), Malazi na Huduma ya Chakula (**asilimia 9.0**) na Umeme (**asilimia 7.6**). Ukuaji wa sekta hizi umechangiwa kwa kiasi kikubwa na uwekezaji wa Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na

uwekezaji ili kuchochea ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Taifa.

### 2.4. Mfumuko wa Bei

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imebaini kwamba bidhaa za chakula na vinywaji baridi zinachangia kwa **asilimia 28.2** ya mfumuko wa bei nchini. Kwa kuwa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetabiri uwepo wa mvua za El nino kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba, 2023, na kwa kuwa kipindi hicho ndicho kipindi cha msimu wa kilimo ni wazi kwamba mvua hizo zinaweza kuathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo. Kamati inashauri Serikali katika mwaka wa fedha 2023/24 kutoa fedha za kutosha kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua chakula cha kutosha ili kukabiliana upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza. Hatua hii iende sambamba na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa maghala na vihenge ili kuongeza uwezo wa NFRA kuweza kuhifadhi chakula.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mapendekezo haya yanatokana na ukweli kwamba uwezo wa nchi wa kuhifadhi chakula ni **tani milioni 3** ambapo Serikali ina uwezo wa **tani 500,000** na tani **2,500,000** ni za watu binafsi na vyama vya ushirika. Uwezo huu ni mdogo ukilinganisha na mahitaji. Hivyo, Serikali ione umuhimu wa kuongeza miundombinu ya kuhifadhi chakula ili kile kitakachonunuliwa kiwe na sehemu ya kuhifadhiwa.

### 2.5. Urari wa Malipo, Biashara na Huduma

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** urari wa jumla wa malipo, biashara na huduma una ziada ya **dola za Marekani milioni 273.50.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ziada hiyo imechangiwa na mikopo kutoka nje. Ziada hii haimaanishi kuwa Serikali ina uwezo endelevu wa kukuza akiba yake ya fedha za kigeni. Hii inatokana na ukweli kwamba nakisi katika urari wa biashara ya bidhaa iliongezeka kwa **asilimia 54.8** kutoka **dola za marekani milioni 4,616** mwaka 2021 hadi kufikia **dola za marekani milioni 7,100.3** mwaka 2022 kama inavyoonekana kwenye jedwali na. 2**.** Ongezeko hili lilitokana zaidi na uagizaji wa bidhaa na malighafi

kutoka nje kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, sababu nyingine zilizosababisha kuongezeka kwa nakisi ya urari wa biashara ni mvurugiko wa mnyororo wa ugavi duniani na vita vya Urusi na Ukraine, kupanda kwa bei za bidhaa za mafuta ya kula, petroli na mbolea pamoja na kuongezeka kwa riba katika soko la fedha la Taifa la Marekani. Sababu hizi zilisababisha kuongezeka kwa gharama za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje na wakati huo huo bei za bidhaa zinazouzwa nje zikiwemo bei za mazao ya biashara kama vile Kahawa na Korosho yalishuka bei.

**Jedwali Na. 2: Mizania ya Urari wa Malipo, Biashara na Huduma**

| | **2021/22** | **2022/23** |
|---|---|---|
| Current account | -3,414.30 | -4,860.10 |
| Capital Account | 440 | 284.5 |
| Financial Account, excl. reserves and related items | 3,640.70 | 4,587.30 |
| **Total** | **666.40** | **11.70** |
| Net Errors and Omissions | -667.50 | 261.80 |
| **Overall Balance** | **-1.10** | **273.50** |

***Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2023***

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina ushauri ufuatao ili kupunguza nakisi ya urari wa biashara na kuongeza fedha za kigeni:

i. Kwa kuwa Serikali bado inaendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambayo inatumia bidhaa nyingi zinazoingizwa kutoka nje ikiwemo chuma, kuna haja ya Serikali kuweka mkakati mahususi wa kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje hususani utalii na usafirishaji ili kukabiliana na nakisi ya urari wa malipo ya kawaida. Hatua hizo zote kwa pamoja zitachangia kuimarika kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine za kigeni;

ii. Serikali iboreshe mazingira yatakayowezesha uzalishaji wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa ndani kama vile mafuta ya kula, nyuzi za pamba, sukari ya viwandani, chuma na ngano. Hatua hii itapunguza uagizaji wa bidhaa hizi kutoka nje na kulinda akiba ya fedha za kigeni;

iii. Kuandaa Sera za Kodi ambazo zitachochea matumizi ya bidhaa zinazozalishwa ndani kuliko zile zinazoagizwa kutoka nje ambazo zinaweza kuzalishwa nchini; na

iv. Serikali iongeze uwekezaji pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara katika sekta za utalii na madini kwa kuwa zina muitikio wa haraka katika viashiria vya kiuchumi na zinaongoza kwa kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

**2.6. Ujazi wa Fedha na Karadha.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) umeongezeka kwa **asilimia 13.7** kutoka **shilingi trilioni 35.5** hadi kufikia **shilingi trilioni 42.2** ikiwa imevuka lengo lililowekwa kwenye tamko la Sera ya fedha ya mwaka 2022/23 la **asilimia 10.** Aidha, kwa mujibu wa Taarifa ya Benki Kuu, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kufikia Agosti, 2023 ulikua kwa **asilimia 17.4** ukilinganisha na lengo la mwaka 2023/24 la **asilmia 10.3.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa kuwa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) imevuka lengo la **asilimia 10,** na kwa kuwa ongezeko hili linaweza kuchangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika uchumi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Benki Kuu kutumia nyenzo za sera ya fedha ili kudhibiti ujazi wa fedha kwenye uchumi uendane na malengo yaliyowekwa. Vilevile, Serikali ihamasishe matumizi ya mfumo rasmi ya kifedha ili kupunguza kiwango cha fedha taslimu ambacho kiko katika mfumo usio rasmi. Hatua hii itaiongezea Serikali mapato na kuimarisha udhibiti wa sera za fedha, pamoja na kuyawezesha mabenki kuongeza amana na uwezo wa kukopesha.

## 2.7. Mikopo kwa Sekta Binafsi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mikopo ya sekta binafsi imekua kutoka **asilimia 9.9** mwaka 2021/22 hadi kufika **asilimia 22.2**. Ukuaji huu umevuka lengo la Tamko la Sera ya Fedha la mwaka 2022/23 la **asilimia 10.3**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli za kilimo iliongezeka kwa **asilimia 44.5**. Ukuaji huu ulichangiwa uwepo wa dirisha la **shilingi trilioni moja** lililofunguliwa na Benki Kuu ili kuhamasisha benki za biashara kukopesha sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi **asilimia 10**. Aidha, ni dhahiri kwamba bila uwepo wa dirisha hili, kungekuwa na mikopo michache kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kilimo ukizingatia vihatarishi vilivyopo katika sekta hii. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhamasisha Benki Kuu kuendeleza uwepo wa dirisha hili muhimu ili kuchochea mikopo kwa sekta ya kilimo na kuongeza mchango wake katika pato la taifa pamoja na kupunguza umaskini.

## 2.8. Viwango vya Riba

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya riba ya mikopo na mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei nchini ulifika **asilimia 4.6** katika mwaka ulioishia Juni, 2023 wakati riba za mikopo zilikuwa **asilimia 16.04** ikiwa ni mara **3.5** ya mfumuko wa bei na tofauti ya takribani **asilimia 8.4** ikilinganishwa na riba za amana ambazo kwa kipindi hicho ilikuwa **asilimia 7.64**. Kamati inaamini kwamba viwango hivi vya riba pamoja na ada na tozo kubwa kwenye miamala ndio chanzo cha faida kubwa kupita kiasi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya gharama za uendeshaji wa mabenki nchini na kubaini chanzo cha riba kubwa ili kusaidia kupunguza riba za mikopo na tozo za miamala na hivyo kuhamasisha wananchi wengi zaidi kutumia huduma za kibenki. Vilevile, Kamati inashauri riba za mikopo kwa watumishi wa umma na waliopo kwenye ajira rasmi na za kimkataba zipunguzwe kutokana na ukweli kwamba mikopo kwa watumishi wa umma inalipwa na waajiri moja kwa moja kutoka kwenye mishahara, na hivyo uwezekano wa kutolipika ni mdogo.

## 2.9. Sekta Ndogo ya Fedha (Micro-Finance)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** hadi kufikia mwezi Juni 2023, Benki Kuu ya Tanzania imetoa leseni **1,307** na kusajili vikundi vya akiba na mikopo **42,257.** Aidha, pamoja na uwepo na Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha Na. 10 ya mwaka 2018, sekta hii haisimamiwi kikamilifu na hivyo kusababisha kuongezeka kwa mikopo isiyo rafiki na inayoleta madhara, na madhila kwa wananchi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa sekta hii inasimamiwa kwa karibu kwa kuhakikisha kanuni za sheria hiyo zinafuatwa ikiwa ni pamoja na masharti ya kumlinda mkopaji dhidi ya mikopo isiyo rafiki yaliyoko kwenye sheria hiyo.

## 2.10. Deni la Serikali

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba uwiano wa ulipaji wa deni kwa mauzo ya nchi unakaribia ukomo wa **asilimia 15** ambapo hadi Juni, 2023 uwiano huu ulikuwa **asilimia 14.1**. Mwenendo huu una athari kwenye akiba ya fedha za kigeni ukizingatia kwamba takribani **asilimia 58.71** ya deni la Serikali ni deni la nje ambalo hulipwa kwa fedha za kigeni. Hivyo, endapo mauzo ya nchi hayawezi kukidhi malipo ya deni basi italazimika kutumia akiba ya fedha za kigeni kulipa deni na hivyo kupunguza uwezo wa nchi kuagiza bidhaa na huduma nje. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi za kuchochea mauzo ya nje kwa kuongeza mauzo ya mazao ya kibiashara yalioongezewa thamani, kuchochea uzalishaji wa bidhaa za viwandani, kukuza sekta ya utalii pamoja na huduma ili kuimarisha akiba ya fedha za kigeni**.**

## 2.11. Maendeleo ya Watu

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Tanzania ina jumla ya idadi ya watu **61,741,120**. Kati ya watu hao idadi ya nguvu kazi yenye umri kati ya miaka 15 hadi 64 imeongezeka kwa **asilimia 20.6** kutoka watu **25,750,116** hadi kufikia watu **31,047,894** ambayo ni sawa na **asilimia 54.8** ya idadi ya watu wote kwa mwaka 2022. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba idadi ya kundi tegemezi ni **asilimia 87** ya watu wote waliopo nchini.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa maana nyingine watu wanaofanya kazi Tanzania ni **8,026,346** kati ya watu **61,741,120** sawa na **asilimia 13** ya idadi ya watu wote. Takwimu hizi zinaashiria kwamba kuna idadi kubwa ya nguvu kazi ambayo haitumiki kikamilifu. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuweka mikakati itakayochochea uwekezaji zaidi kuwekeza zaidi kwenye sekta zinazoweza kuzalisha ajira kwa wingi kama vile kilimo, mifugo, uvuvi, utalii, viwanda, usafiri na usafirishaji ili kupunguza utegemezi huo. Aidha, ni wakati muafaka kwa Serikali kuangalia upya Sera zake kuhusu idadi ya watu ili ongezeko la watu liende sambamba na kasi ya ukuaji wa uchumi.

### 2.12. Pato la Kila Mtu

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Taarifa inaonesha kuwa pato la mtu mmoja nchini limekua kutoka **dola za Marekani 1,080** mwaka 2020 hadi kufikia **dola za Marekani 1,200** mwaka 2023. Pato hilo hukokotolewa kwa njia ya wastani wa Pato la Taifa kwa kila mwananchi ambapo Pato la Taifa kwa bei za miaka husika hugawanywa kwa idadi ya watu. Hivyo, kipimo hiki si kipimo kizuri cha kutathmini mgawanyo wa Pato la Taifa kwa kila mtu. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia vipimo vingine vinavyozingatia vielelezo vingine vya hali ya umaskini nchini.

## 3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA MPANGO KWA MWAKA – 2022/23 NA ROBO YA KWANZA 2023/24

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ulitengewa jumla ya shilingi **trilioni 15.006** sawa na **asilimia 36.18** ya Bajeti ya Serikali. Hadi mwezi Juni 2023 jumla ya **shilingi trilioni 13.971** zilikuwa zimetolewa sawa na **asilimia 93.1** ya lengo. Uchambuzi wa utekelezji wa miradi mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

### 3.1. Mradi Na. 4281: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR).

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ukiwemo mradi huu wa reli ya kisasa (SGR). Hata hivyo, ili reli hiyo

iendeshwe kwa ufanisi na kuleta manufaa ni lazima urefu usipungue **kilomita 400**. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kukamilisha haraka kipande cha reli kinachounganisha bandari ya DSM na kipande cha Morogoro hadi Makutupora (**kilomita 722**) ili reli hiyo ianze kutumika. Hatua hii itaisaidia Serikali kuanza kukusanya mapato kutoka kwenye mradi huu hasa ukizingatia kwamba mikopo iliyotumika kujenga reli hii inakaribia kuiva. Vilevile, Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

i. Katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali ihakikishe inatafuta fedha za kutosha ili kuziba pengo la ufadhili wa mradi kwa ajili ya uendelezaji wa mradi. Kutokufanya hivyo kutasabaisha ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi ambao wameshakabidhiwa loti mbalimbali; na

ii. Serikali ijielekeze kutumia mikopo yenye masharti nafuu na masharti ya kati katika ujenzi wa reli hiyo ili kuepuka matumizi ya mikopo ya kibiashara ambayo ina riba za juu na inaiva katika kipindi cha muda mfupi.

### 3.2. Utekelezaji wa Miradi ya Barabara.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu wa ulipaji wa madai ya wakandarasi wa barabara nchini. Kuanzia Mwezi Agosti, 2023 Serikali imekuwa ikitoa **shilingi bilioni 70** kwa ajili ya kulipa wakandarasi, kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 50 ni** kwa ajili ya wakandarasi wa ndani na **shilingi bilioni 20** wakandarasi wa nje. Hatua hii inaenda kupunguza hati za madai na riba zinazotokana na ucheleweshaji wa malipo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa miradi yote ya barabara iliyotolewa Taarifa ya utekelezaji katika Mapendekezo ya Mpango na kulinganisha na utekelezaji wa miradi hiyo katika Mipango ya Mwaka mmoja mmoja iliyopita dhidi Mpango wa Miaka mitano na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Miradi mingi ya barabara imekuwa haikamiliki kwa wakati;

ii. Baadhi ya barabara zimekuwa zikitolewa Taarifa miaka ya nyuma na hazijakamilika ila Taarifa zake hazionekani katika Taarifa ya Utekelezaji wake katika Mapendekezo ya Mpango;

iii. Serikali kuingia mikataba mingine ya vipande vya barabara wakati vipande vilivyopo katika barabara hiyo hiyo utekelezaji haujafikia hata asilimia 50;

iv. Serikali kufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya barabara ambayo utekelezaji wake hautarajiwi kuanza ndani ya muda mfupi, na hivyo kulazimika kurudia kufanya tena upembuzi pindi mradi unapotaka kuanza kutekelezwa ikiwa muda mrefu umepita tangu upembuzi wa awali ulipofanyika;

v. Serikali kutozwa riba kutokana na kuchelewa wa kulipa hati za madai ya wakandarasi;

vi. Barabara kujengwa chini ya kiwango na hivyo kulazimu matengenezo ya mara kwa mara muda mfupi baada ya barabara kukamilika;

vii. Usimamizi usioridhisha wa magari yanayozidisha uzito na hivyo kusababisha uharibifu wa barabara na madaraja;

viii. Baadhi ya wakandarasi kushindwa kutekeleza miradi kutokana na kutolipwa kwa wakati na kupewa miradi mingi bila kupima uwezo;

ix. Urefu wa barabara kubadilika katika taarifa mbalimbali za Serikali; na

x. Uwepo wa wakandarasi wasio na uwezo .

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kufuatia uchambuzi huo, Kamati ina ushauri ufuatao:-

i. Ujenzi wa miradi ya barabara kupimwa kwa ufanisi wa kila barabara kwa kulinganisha urefu uliokuwa umepangwa kujengwa katika mwaka husika. Hali ilivyo hivi sasa taarifa

inayotolewa hujumuisha maeneo yaliyokamilika katika mwaka wa fedha uliotangulia na hivyo ni vigumu kupima ufanisi;

ii. Upembuzi yakinifu wa barabara ufanyike pale tu ambapo Serikali ina nia ya kuanza ujenzi wa barabara husika;

iii. Barabara zenye manufaa ya kiuchumi na za kimkakati zipewe kipaumbele;

iv. Kupima uwezo wa wakandarasi kabla ya kuwapa zabuni za ujenzi wa barabara; na

v. Kulipa kwa wakati madeni ya wakandarasi, ili kuepusha ongezeko la riba.

**3.3. Mradi Na. 3172: Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115).**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia katika kutekeleza mradi huu ambapo hadi kufika mwezi Julai, 2023, Serikali ilikuwa imeshamlipa mkandarasi **asilimia 84.35** ya gharama zote za mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2024. Kukamilika kwake kutaletea Taifa manufaa makubwa ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa umeme wa uhakika. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba mradi huo unakamilika kama ilivyopangwa.

**3.4. Mradi Na 4294: Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** pamoja na uwekezaji mkubwa ambao umefanywa na unaendelea kufanywa na Serikali kwa Shirika la ndege, bado viwanja vingi nchini vinakabiliwa na ukosefu wa miundombinu wezeshi. Miundombinu hiyo ni taa kwenye viwanja vya ndege vya kimkakati vya Arusha, Bukoba na Mtwara. Vilevile, miradi mingi ya ujenzi wa viwanja imekuwa inachukua muda mrefu kukamilika kama vile ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha ndege cha Mwanza. Ili kuongeza idadi ya miruko, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba uboreshaji wa Shirika unaenda sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege.

## 3.5. Mradi Na 3155: Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mradi huu ukikamilika utakuwa na manufaa yafuatayo: kuchochea uzalishaji wa nishati ya umeme, kuongeza matumizi ya gesi kama nishati ya kuendeshea magari na mitambo, kuongeza mauzo ya bidhaa hiyo nje ya nchi, kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kutumia nishati hiyo majumbani pamoja na uzalishaji wa mbolea. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha majadiliano mapema iwezekanavyo ili mradi uanze kutekelezwa na Taifa kunufaika.

## 3.6. Mradi Na 3176: Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) lenye urefu wa km 1,443.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kulipa jumla ya **dola za Marekani milioni 193.03** kama sehemu ya mtaji wa **dola za Marekani milioni 308**. Aidha, ulipaji wa fidia umekamilika kwa **asilimia 99** ambapo wananchi **387** kati ya **388** wanaopisha ujenzi wa kambi zitakazotumika wakati wa ujenzi wameshalipwa, na wananchi **9,416** kati ya watu **9,510** wanaopisha eneo la mkuza wamelipwa. Aidha, kukamilika kwa mradi huu kutaletea Taifa manufaa makubwa ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya bandari ya Tanga. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaendelea kununua sehemu yake ya hisa ili mradi utakapokamilika Taifa linufaike na gawio.

## 3.7. Mradi Na. 3171: Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia jumla ya **shilingi bilioni 15.02** kati ya **shilingi bilioni 15.43** kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi **1,048** kati ya wananchi **1,144**, sawa na **asilimia 97.3**. Duniani kote ni nadra sana kukuta makaa ya mawe na chuma kuwa kwenye maeneo yanayokaribiana. Awali miradi hii ilipangwa kutekelezwa kwa pamoja ili makaa ya mawe ya mchuchuma yatumike kuyeyushia chuma cha Liganga. Hata hivyo, Kamati imebaini Serikali ina nia ya kutenganisha Miradi hii kwa kuanza kuchimba makaa ya mawe kwa sababu

yamepanda bei katika soko la Dunia. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi hii kwa pamoja kama ilivyokuwa imepangwa awali ili kuleta manufaa yaliyokusudiwa pamoja na kupunguza gharama za miradi.

### 3.8. Usambazaji wa Nishati ya Umeme Vijijini

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya kupeleka umeme vijijini ambapo vijiji **10,987** kati ya vijiji **12,318** vimeunganishwa na umeme sawa na **asilimia 89.19**. Hata hivyo, Kamati inaona ni vyema kukamilisha vijiji vilivyosalia **1,331** kabla ya kuelekeza kiasi kikubwa cha fedha kwenye vitongoji vilivyopo kwenye vijiji ambavyo vina umeme. Mfumo huo wa utekelezaji wa mradi unaathiri fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha vijiji vilivyosalia. Kamati inashauri Serikali kutokuanza miradi mipya mpaka pale itakapo hakikisha kuwa mradi wa awali umekamilika kwa **asilimia 100.** Hatua hii itasaidia sio tu kupima ufanisi lakini vilevile kukamilika kwa maeneo yote ya mradi na kwa wakati.

### 3.9. Mradi Na. 6360: Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kati ya miradi iliyopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Bunge ni pamoja na utwaaji wa maeneo yanayozunguka Bunge. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa daftari la uthamini ambalo limeshawasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fidia inalipwa kwa maeneo yanayomilikiwa na watu binafsi mapema iwezekanavyo ndani ya muda wa miezi 6 uliowekwa kisheria kuisha. Hatua hii itasaidia kuepuka kurudiwa kwa zoezi la tathmini ambalo litasabisha kuongezeka kwa gharama.

### 3.10. Mradi Na. 6284: Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, pamoja na Serikali kuendelea kuunganisha na kuhuisha mifumo yake bado kuna uwepo wa mifumo mingi ambayo haisomani, haijaunganishwa na haibadilishani Taarifa na mifumo mingine ya Serikali. Kwa mfano, Mfumo wa Utendaji Kazi kwa mtumishi (PEPMIS) na kwa taasisi

(PIPMIS), Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS), Mfumo wa Tathmini ya Mahitaji ya Watumishi wa Umma (e-HRP); Mifumo ya e-Mrejesho, e-Mikutano, e-Rufaa, e-Dodoso pamoja na Shared Helpdesk Mifumo hii yote inasimamiwa na Ofisi ya Rais Utumishi. Kamati inaishauri Serikali badala ya kuanzisha mifumo mipya ni vyema kuwe na mfumo mmoja *(core system)* wa watumishi wenye moduli mbalimbali ili kupunguza wingi wa mifumo na changamoto za kusomana na kubadilishana taarifa.

### 3.11. Mradi Na. 6501: Vitambulisho vya Taifa

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati katika nyakati tofauti imekuwa ikifuatilia na kutanzua changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(National Identification Authority-NIDA)* kuhusu uchapishaji wa Vitambulisho vya Taifa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwezesha ulipaji wa deni la mzabuni la jumla ya **dola za Marekani milioni 7.6** sawa na **shilingi bilioni 17** na kusamehe kodi kwenye kadi zinazotumika katika uchapishaji wa vitambulisho. Pamoja na hatua hizi zote, vitambulisho vilivyochapishwa katika muda wa mwaka mmoja ni **1,849,931** na hivyo kufikisha jumla ya vitambulisho vilivyochapishwa kuwa **12,863,269** kati ya idadi ya Watu **24,083,933** waliosajiliwa na kupewa namba ya utambuzi ikiwa ni sawa na **asilimia 50** ya waliotakiwa kupewa vitambulisho tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Gazeti la Serikali, **namba.122 la tarehe 01/08/2008).**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba Mtambo uliosimikwa katika kiwanda cha kuchapisha vitambulisho vya NIDA una uwezo wa kuchapisha vitambulisho **4,500** kwa saa. Kwa vile upatikanaji wa kisilikoni (chip) za vitambulisho Duniani si changamoto tena, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba watu wote waliosajiliwa na wanaostahili wanapewa vitambulisho vyao. Aidha, wananchi ambao vitambulisho vyao vimekwisha tolewa na hawajavichukua wahamasishwe kwa kutangaza orodha ya majina yao na eneo ambapo vitambulisho vyao vipo ili waweze kuvichukua.

### 3.12. Huduma za Zimamoto na Ukoaji

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika siku za hivi karibuni yametokea matukio ya moto katika masoko makubwa nchini mfano soko la Kariakoo, Karume na Mbagala Rangi Tatu Dar es salaam. Matukio haya yamekuwa yakileta hasara kubwa kwa Wafanyabiashara na miundombinu ya biashara. Kamati inaishauri Serikali katika mwaka wa Fedha 2024/25 kuweka miundombinu ya maji na magari ya kuzimia moto kwenye maeneo ya masoko makubwa ili kuepusha hasara zinazojitokeza kutokana na matukio ya moto. Vilevile, ni lazima kuhakikisha viwanja vyote vya ndege nchini vinakuwa na magari ya zimamoto yanayoendana na hadhi ya viwanja hivyo.

### 3.13. Mradi Na. 4428: Uimarishaji wa Mashamba ya Magereza

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa mwaka mmoja gharama ya kuwalisha wafungwa nchini ni **Shilingi bilioni 10.42**. kamati inatambua kuwa, Jeshi la Magereza ni moja kati ya vyombo vya Serikali vyenye mashamba makubwa ambayo yangeweza kutumika kuzalisha chakula cha kutosha kuwalisha wafungwa na kuuza. Mashamba haya yamekuwa hayatumiki kikamilifu kutokana na kukosekana kwa mtaji wa kuyaendeleza ili magereza yaweze kuyasimamia na kuzalisha.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25 Kamati inaishauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa Jeshi la Magereza ili liendeleze mashamba yake. Aidha, kwa magereza ambayo hayana mashamba uwekezaji ufanyike kwenye miradi mingine kama vile ufyatuaji wa matofali na utengenezaji wa samani.

### 3.14. Mradi Na. 4283: Ujenzi wa Mkongo wa Taifa

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Tanzania iliunganishwa rasmi kwenye Mkongo wa Mawasiliano (Seacom International undersea fiber optic network) tarehe 23 Julai, 2009. Tangu Tanzania kuunganishwa na Mkongo huo kukabidhiwa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), umeweza kusambazwa nchini kwa jumla ya **kilomita 8,319 kati ya lengo la kilomita 15,000** kwa miaka 14 sawa na wastani wa **kilomita 594.2** kwa mwaka. Kasi hii ya

usambazaji ni ndogo ukilinganisha na mahitaji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza gharama za kutandaza njia ya mkongo kutoka **dola za marekani 100 kwa kilomita** hadi **dola za marekani 200.** Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia mfumo wa ubia na makampuni ya mawasiliano yaliyopo nchini ili mkongo huo usambazwe kwa kasi kuliko kutegemea Bajeti ya Serikali pekee.

**3.15. Mradi Na.4234: Mfumo wa Anuani za Makazi na Ukusanyaji wa Kodi za Majengo**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, lengo la mradi huu ni kutambua anuani sahihi za makazi ya watu, biashara na ofisi. Kamati imebaini mradi huu unaweza kusaidia Serikali katika ukusanyaji wa Kodi ya Majengo. Kupitia mradi huu idadi ya nyumba zilizosajiliwa ni **12,768,909** kati ya nyumba **14,348,372** zilizopo kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Kwa kutumia takwimu hizi, Kamati inaishauri Serikali katika mwaka wa fedha 2024/25 kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato kutoka chanzo hiki kwa walau kufikia ukuaji wa **asilimia 15** kutoka **asilimia 3** ya mwaka 2022/23.

**3.16. Kiwanda cha Viuwadudu Kibaha**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza uzalishaji wa dawa za viuwadudu *(pesticides)* ambazo zinatengenezwa na kiwanda hicho. Hadi sasa dawa za viuwadudu aina 2 zinatengenezwa na kutumiwa katika mazao ya pamba pamoja na taasisi za utafiti kama vile TARI. Hatua hii ni njema kwa kuwa sasa wakulima wataachana na kutumia viuwadudu ambavyo si vya asili na vinamadhara kwa afya za bidanamu. Vilevile, itaipunguzia Serikali gharama za kuagiza viuwadudu kutoka nje. Hivyo, Serikali ihamasishe matumizi ya viuwadudu vya asili na suala hili lipewe kipaumbele ni hatua madhubuti ya kuondokana na viuadudu ambavyo si vya asili.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** aidha, Kiwanda cha Viuwadudu cha Kibaha kinakabiliwa na changamoto za kukosekana kwa ithibati pamoja na mtaji wa uendeshaji. Katika mwaka wa Fedha 2023/24, Kamati iliagiza Serikali kutenga kiasi cha **shilingi bilioni 2.3**

ili zitumike kupata ithibati pamoja na kufanya uchambuzi wa soko la mbolea nchini. Ithibati hiyo itasaidia kiwanda hicho kuuza bidhaa zake kwenye masoko ya kikanda na kimataifa. Aidha, tafiti na tathmini inafanyika ili kuona uwezekano wa uzalishaji wa mbolea kwa sababu kiwanda hiki kina uwezo wa kuzalisha bidhaa hiyo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali katika mwaka wa fedha 2024/25 kutenga na kutoa kiasi cha **shilingi bilioni 2.3** ili kiwanda hicho kiweze kupata ithibati na kukamilisha utafiti.

### 3.17. Mchango wa Mifuko ya Jamii katika Uchumi wa Viwanda

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba Mifuko ya Hifadhi ya jamii Duniani huwekeza kwenye Hatifungani, Masoko ya Hisa, Majengo *(Real Estate)* pamoja na uwekezaji uliolindwa na mali *(Asset Backed Investment)*. Uamuzi wa Serikali wa kuelekeza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza moja kwa moja kwenye uchumi wa viwanda ulikuwa mzuri lakini njia iliyotumika haikuwa sahihi. Uwekezaji wa moja kwa moja kwenye ujenzi wa viwanda na uzalishaji mashambani sio mzuri sana kwa sababu mifuko hii haina uzoefu wa kuendesha na kusimamia miradi iliyoko kwenye sekta hizo na hivyo, kuhatarisha michango ya wanachama. Hivyo, Kamati inaishauri Mifuko ya Hifadhi ya jamii kuliko kujiingiza moja kwa moja kwenye biashara ambazo haina uzoefu nazo ijielekeze katika masoko ya mitaji ili sekta binafsi ipate mitaji na kuwekeza kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji kama vile Kilimo, ujenzi na viwanda.

### 3.18. Kilimo cha Umwagiliaji

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Tanzania ina jumla ya hekta **milioni 29.4** zinazofaa kwa ajili ya Kilimo cha umwagiliaji. Hadi kufikia mwezi Juni, 2023 jumla ya hekta zilizokuwa chini ya Kilimo cha umwagiliaji zilikuwa hekta **822,285.6** sawa na **asilimia 2.8** ya eneo lote linalofaa kwa umwagiliaji. Aidha, lengo lililokuwa limewekwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano lilikuwa ni kufikia hekta **milioni 1.2** ifikapo mwaka 2025/26 ambapo hadi kufika Juni, 2023 limetekelezwa kwa **asilimia 68.5**. Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji ambapo katika miaka 2 (2022/23 na 2023/24)

imeongeza hecta **190,000**. Hata hivyo, kasi hii ni ndogo ukilinganisha na mahitaji ya kupanua eneo la umwagiliaji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini ili kufikia lengo lililowekwa ni lazima katika kipindi kilichobaki kuongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta **188,857.5** kila mwaka. Vilevile, Kamati imebaini kuna muingiliano wa Kitaasisi kati ya Bodi za Mabonde ya maji yaliyoko chini ya Wizara ya Maji na Tume ya Umwagiliaji iliyo chini ya Wizara ya Kilimo. Pamoja na kwamba Tume inajenga miundombinu ya umwagiliaji, mmiliki wa maji na anaeamua yatozwe kiasi gani ni Bodi za Mabonde ya Maji zilizo chini ya Wizara ya Maji. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuondoa mkanganyiko huu wa kitaasisi ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

### 3.19. Mradi Na. 4486: Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Programu hii ilipangwa kutekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilianza mwaka 2017/18 – 2022/23 na awamu ya pili ilitarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka 2023/24 – 2028/29. Aidha, Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango haijaainisha juu ya utekelezaji wa awamu ya pili baada ya awamu ya kwanza kukamilika Juni, 2023. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa utekelezaji wa awamu ya kwanza umefanyiwa tathmini na Wizara inakamilisha Mpango Mkakati wa Kilimo Tanzania 2050 *(Tanzania Agriculture Master Plan 2050)* ambapo awamu ya pili ya utekelezaji wa programu ya ASDP II itakuwa ni sehemu ya mpango huu. Lengo la Serikali kuja na Mpango huu ni ili kuhuisha Mipango ya kilimo na Dira ya Taifa ya Maendeleo inayotarajiwa ili kuleta tija na hivyo kuleta manufaa yanayotarajiwa. Kamati inashauri Serikali kukamilisha Mpango huo mapema kabla ya kuanza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

### 3.20. Upatikanaji wa Mbolea ya Ruzuku

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** hadi kufikia Juni, 2023 jumla ya **shilingi bilioni 214.8** zilitumika kwenye ruzuku ya mbolea na hivyo kusaidia mbolea kupatikana kwa bei nafuu. Kutokana na ruzuku hiyo mbolea zilizosambazwa ziliongezeka kutoka **tani 363,599** mwaka

2021/22 hadi kufika **tani 531,091** mwaka 2022/23. Ongezeko hili limewezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka **tani 17,148,290** mwaka 2021/22 hadi **tani 20,402,014** mwaka 2022/23. Ili ruzuku hii iwe endelevu Kamati inaishauri Serikali kuchukua tahadhari katika utaratibu wa utolewaji wa ruzuku wa hivi sasa ili usije kusababisha hasara kama ilivyokuwa ruzuku ya mfumo wa vocha. Vilevile, Serikali ipitie upya viwango vya kodi, ada na tozo kwenye bidhaa ya mbolea ili ipatikane kwa bei nafuu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiwezesha Kampuni ya Taifa ya Mbolea (TFC) mtaji wa **shilingi bilioni 114 zilizotokana na mtaji kutoka Serikalini, mkopo wa JICA na ruzuku kutoka Serikalini** ili iweze kuagiza mbolea moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji. Kamati inaishauri Serikali kuendelee kuwekeza katika Kampuni yake ya TFC ili iweze kuagiza mbolea kwa bei nafuu. Hatua hii itaenda kupunguza bei ya mbolea nchini.

### 3.21. Upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mradi huu ulikuwa una lengo la kutafuta masoko ya mazao ya kilimo ya wakulima ndani na nje ya nchi. Aidha, Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango inaonyesha kuwa wanunuzi wakubwa wa soko la mazao ya nafaka nchini ni Taasisi za Serikali. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba hakuna taarifa iliyotolewa kuhusu utafutaji na upatikanaji wa masoko nje ya nchi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inashauri Serikali kuendelea na mikakati ya kutafuta masoko ya mazao ya kimkakati nje ya nchi ili kuongeza fedha za kigeni kwa kushirikiana na sekta binafsi. Vilevile, Kamati inai shauri Serikali kuongeza uwekezaji kwenye miundombinu na mifumo ya ithibati (*Certification)* ya bidhaa zetu ili ziweze zikidhi viwango vinavyotakiwa kwenye masoko ya Kimataifa.

### 3.22. Kuimarisha Mifumo ya Upatikanaji wa Mitaji katika Sekta ya Kilimo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa upatikanaji wa mikopo katika sekta mbalimbali na kubaini kwamba katika mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya **shilingi trilioni 2.622** zilitengwa na mabenki kwa ajili ya shughuli za kilimo kwa riba isiyozidi **asilimia 10** kwa mchanganuo ufuatao **NMB-trilioni 1.62, TADB- bilioni 151.7, CRDB-bilioni 801, Mfuko wa Pembejeo-milioni 70.** Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa kati ya kiasi hicho ni **asilimia 7 tu** kilitumika katika shughuli za uzalishaji na **asilimia 93** zilitumika kwenye biashara ya mazao. Kiwango hiki ni kidogo na hivyo ni wazi kwamba uzalishaji katika sekta hii itabaki kuwa chini. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Benki Kuu kutumia nyenzo za sera za fedha na kibajeti ili kuhakikisha mikopo mingi inaekelezwa katika shughuli za uzalishaji wa kilimo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga **shilingi trilioni moja** kwa ajili ya kukopesha mabenki yatakayotoa mikopo kwa sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi **asilimia 10** na hivyo kutoa hamasa kwa mabenki ya biashara kutenga fedha nyingi.

### 3.23. Maliasili na Utalii

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** idadi ya watalii imeongezeka kutoka watalii **922,692** mwaka 2021 hadi kufikia watalii **1,454,920** mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 57.7**. Ongezeko hilo limeongeza fedha za kigeni nchini kutoka **dola za marekani bilioni 1.31** mwaka 2021 hadi kufikia **dola za marekani bilioni 2.53** mwaka 2022. Pamoja na ongezeko hili, sekta ya Utalii bado haijaweza kulinufaisha Taifa kama inavyotarajiwa ukilinganisha na idadi ya vivutio vilivyopo nchini. Taarifa ya Shirika la World Economic Forum (WEF) inaonyesha kwamba Tanzania ni kwanza katika Bara la Afrika na ya 12 duniani kwa kuwa na vivutio bora vya asili vya utalii na ya 32 kwa Bara la Afrika kwa kuwa na rasilimali bora za mali kale.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba sekta ya utalii inanufaika na mkopo wa *Extended Credit*

*Facility* kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa awamu ya 4 unaotarajiwa kutolewa mwezi Machi, 2024 wa **shilingi bilioni 349.8**. Fedha hizo zitumike katika kuboresha miundombinu ya utalii. Hatua hii itasaidia kuchochea ukuaji wa sekta hii na hivyo kuongeza ziada kwenye urari wa malipo ya huduma. Aidha, Serikali imepata mafanikio makubwa katika kudhibiti ujangili kupitia Jeshi Usu ambapo jumla ya **shilingi bilioni 2.7** zilitumika katika mwaka wa fedha 2022/23. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuboresha Jeshi Usu ili kuondoa changamoto zilizopo kwa kuwa bado Jeshi hilo ni muhimu katika Sekta hii.

**3.24. Mradi Na. 4647: Kupanda Miti Kibiashara**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, sekta ya misitu inaweza kuongeza fedha za kigeni kupitia biashara ya hewa ukaa (Carbon Trading). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia wakala wa misitu (TFS) kufanya tathmini ya misitu iliyopo nchini kwa lengo la kupata takwimu sahihi ili kunufaika na fursa ya biashara ya hewa ukaa. Aidha, Serikali ihamasishe wananchi kupanda misitu ya kibiashara na kutunza misitu ya asili iliyopo ili kulinda mazingira na kujipatia kipato.

**3.25. Soko la Bidhaa Tanzania- *(Tanzania Merchantile Exchange-TMX)***

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** changamoto inayolikabili Soko la Bidhaa Tanzania ni uwepo wa mazao yaliyoimarika katika mfumo wa stakabadhi za ghala kuendelea kuuzwa kwa mfumo wa minada na hivyo wakulima kutopata kipato stahiki. Hivyo, inapendekezwa kutolewa kwa Tamko la Kisera litakaloruhusu mazao yaliyo katika Mfumo wa stakabadhi za ghala kuuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). Vilevile, bidhaa zingine zinazoweza kuuzwa kwenye soko hilo ni mifugo, mazao ya misitu na madini.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Tamko hili liende sanjari na kuunganisha Sheria inayosimamia Stakabadhi za ghala na Sheria ya Masoko ya Bidhaa. Hivyo, Kamati inashauri Tamko hilo la kisera pamoja na kuunganisha Sheria vifanyike kabla ya msimu wa mavuno wa mwaka 2023/24 pamoja na kuondoa mkanganyiko uliopo baina ya soko la TMX na Bodi za mazao.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** vilevile, ili soko la TMX lifanye kazi vizuri ni lazima kuboresha kujenga miundombinu kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya mbogamboga na matunda *(perishables)*. Changamoto hii imesababisha mazao yaliyopo katika kundi hilo kushindwa kuuzwa kwenye la TMX. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa katika mwaka wa fedha 2024/25 inatenga fedha kwa ajili wa ujenzi wa miundombinu hiyo ili kuongeza mazao katika mfumo wa stakabadhi na kuwasaidia wakulima wa mazao haya na hivyo kuongeza kipato.

**3.26. Mradi Na. 6260: Mradi wa Kuwezesha Taasisi: Kuimarisha Maendeleo ya Soko la Ndani na Nje – TANTRADE**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kupitia azimio la Septemba 9, 2021 Bunge liliridhia mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo huru la Biashara la Afrika (*Agreement Establishing African Continental Free Trade Area – AfCFTA*). Lengo la eneo hilo ni kukuza biashara, uchumi, uwekezaji pamoja na kuhamasisha umoja wa forodha Afrika. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina ya fursa zilizopo katika Eneo huru la Biashara la Afrika ili elimu itakayotolewa kwa wafanyabiashara iwe na lengo la kulinufaisha Taifa na fursa zinazotokana na soko hilo. Aidha, Serikali iendelee kuhuisha taratibu za biashara na uwekezaji za ndani ya nchi ili kuvutia uwekezaji zaidi na kurahisisha ufanyaji biashara.

**3.27. Sekta ya Afya**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imechambua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Sekta ya Afya na imebaini masuala yafuatayo;

**a) Mradi Na. 5429: Huduma ya Afya ya Msingi**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo iliyowasilishwa na Serikali mwaka 2022/23 ilionyesha kuendelea na ujenzi wa **zahanati 495**. Aidha, Taarifa iliyowasilishwa na Serikali inaonyesha kukamilika kwa ujenzi wa **zahanati 228** na kuendelea na ujenzi wa **zahanati 72,** hivyo kufanya jumla ya Zahanati zinazoendelea kujengwa na zilizo kamilika kuwa 300 takwimu hizi

zinaonyesha kwamba zahanati 195 hazikutolewa Taarifa kuhusu utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali kukamilisha zahanati 195 zilizokuwa kwenye mpango wa 2022/23.

### b) Changamoto ya watumishi kwenye sekta ya Afya

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kamati imebaini kwamba hadi mwezi Machi, 2023 watumishi waliokuwa kwenye sekta ya Afya ni **106,616** sawa na **asilimia 48.7** sawa na mahitaji ya watumishi **219,061**. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaajiri watumishi wa kutosha katika sekta hii ili Sheria ya Bima ya afya kwa wote iliyopitishwa na Bunge isikwamishwe na kukosekana kwa watumishi kwenye vituo vya kutolea Huduma za Afya.

### c) Kuchochea Maendeleo ya Watu – Afya

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini bado kuna changamoto ya upatikanaji wa dawa kutokana na Bohari ya Dawa *(Medical Store Department-MSD)* kukosa mtaji wa kutosha. Changamoto hii imesababisha MSD kuwa duka la dawa badala ya kuwa bohari ya dawa. Jumla ya **shilingi bilioni 562** zinahitajika ili kuwezesha MSD kimtaji ili ijiendeshe kibiashara na kwa ufanisi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kutoa mtaji kwa Bohari ya Dawa (MSD) ili kuwezesha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa wakati. Hivi sasa MSD inategemea fedha za Taasisi husika ili iagize dawa na vifaa tiba jambo ambalo limekuwa linachelewesha upatikanaji wa dawa.

### 3.28. Miradi ya Elimu

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/23 katika sekta ya elimu na kubaini kwamba fedha nyingi katika sekta hii zimeelekezwa katika maeneo yafuatayo: -

i. Miundombinu ya kujifunzia na kujifunza;

ii. Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambapo zimetumika shilingi **bilioni 656.9**; na

iii. Elimu msingi na sekondari bila ada ambapo zimetumika **bilioni 454.96**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** maeneo ambayo yamepokea fedha kidogo ni kama yafuatayo:

i. Ununuzi wa vitabu vya kiada na ziada;

ii. Shughuli za utafiti ambapo zimetumika **shilingi bilioni 4.9** sawa na **asilimia 0.003 ya Pato la Taifa,** chini ya lengo la kutenga asilimia 1 ya pato la Taifa kwa ajili ya utafiti;

iii. Mafunzo kwa vitendo; na

iv. Mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya kati.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufuatia uchambuzi huo Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: -

i. Kutenga fedha za kutosha kwenye utafiti na ubunifu ili elimu inayotolewa iendane na wakati na mabadiliko ya sayansi na teknolojia;

ii. Kuhakikisha elimu inayotolewa inaendana na mazingira na inawaanda vijana kwenye stadi za kazi kwa kuongeza mafunzo kwa vitendo;

iii. Kufanya tathmini ya mahitaji ya rasilimali watu (human resource audit) ili kuangalia mahitaji ya wataalamu katika kada mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha elimu inayotolewa inaenda kukidhi mahitaji; na

iv. Mitaala ya elimu inayoandaliwa na Serikali iangalie mahitaji na hali ya uchumi ya eneo husika, pamoja na shughuli za kiuchumi za eneo husika ili kuleta tija.

### 3.29. Ardhi, Mipango miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Sekta ya Ardhi nchini inakumbwa na changamoto zifuatazo: -

i. Kodi ya pango la ardhi kutokukusanywa kikamilifu, ambapo katika kipindi cha Julai 2022 - Mei, 2023 Serikali iliweza kukusanya **shilingi bilioni 132.97** sawa na **asilimia 53.2** ya lengo la kukusanya **shilingi bilioni 250.1** kutoka kwenye chanzo hiki.

ii. Migogoro ya ardhi mijini na vijijini;

iii. Kipande kimoja cha ardhi kugawiwa kwa mtu zaidi ya mmoja;

iv. Kutokuwepo kwa mipango miji na hivyo kuchochea makazi holela; na

v. Ucheleweshaji wa utoaji wa hati miliki za ardhi na urasimu katika ofisi za masijala za ardhi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza masuala yafuatayo katika mwaka wa fedha 2024/25;

i. Kufuatilia madeni ya pango la Ardhi kwa kuandaa na kutangaza orodha ya wadaiwa ambao hawajalipa kodi ya Ardhi na kuweka sharti la kisheria endapo Ardhi haijalipiwa pango kwa miaka mitatu mfululizo, Hati irejeshwe Serikalini;

ii. Kuharakisha na kuhamasisha upimaji wa ardhi mijini na vijijini ili kuondoa migogoro ya ardhi na makazi holela;

iii. Kutumia mifumo ya kidigitali katika kuhifadhi nyaraka ili kuondoa urasimu uliopo katika ofisi za masijala ya ardhi nchini;

iv. Kuharakisha mchakato wa utoaji hati miliki kwa wananchi waliokwisha lipia;

v. Miradi ya upimaji na uendelezaji wa miji izingatie maeneo ya kupitisha miundombinu ya maji safi na maji taka, barabara, mkongo wa mawasiliano, umeme na gesi;

vi. Kuangalia uwezekano wa kuanzisha kitengo cha kusimamia ukusanyaji wa kodi ya ardhi badala ya kutegemea maafisa ardhi; na

vii. Kuhakikisha kiasi kikubwa cha fedha za mradi wa Benki ya Dunia wenye thamani ya **dola za Marekani milioni 150** zitumike kwenye upimaji wa Ardhi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** hatua zilizopendekezwa na Kamati zitapunguza migogoro ya wakulima na wafugaji, kuimarisha matumizi bora ya ardhi, kulinda vyanzo vya maji, kulinda uharibifu wa mazingira pamoja na kuongeza mapato ya Serikali.

**3.30. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa miradi ya maji iliyotekelezwa na kubaini yafuatayo;

i. Jumla ya watu **milioni 12.6** hawapati huduma ya maji safi na salama na kati yao watu **milioni 9.4** wanaishi ni vijijini na **milioni 3.2** wanaishi mijini. Takwimu hizi zinaonyesha upatikanaji wa maji kwa wastani lakini haziakisi hali halisi ya upatikanaji wa maji mijini na vijijini. Jedwali namba 3 linaonesha hali ya upatikanaji wa maji vijijini na mijini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali katika mwaka wa fedha 2024/25 kufanya tathmini ya kina ya upatikanaji wa maji safi na salama nchini ili kuwa na takwimu zinazoakisi uhalisia.

ii. Kupitia fedha za mkopo wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO - 19 (TCRP), Serikali ilinunua seti 25 za mitambo kwa ajili ya kuchimba visima vya maji pamoja na mabwawa. Aidha, Kamati imebaini kwamba mitambo hii haitumiki kikamilifu kutokana na kuwa kuna Mamlaka

za Serikali za Mitaa hazina uwezo wa kifedha wa kukodi mitambo hiyo**.** Hivyo, Kamati inaishauri Serikali katika mwaka 2024/25 kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya kukodi mitambo hiyo ili itumike kikamilifu.

**Jedwali Na. 3. Hali ya Upatikanaji wa Maji Salama Vijijini na Mijini.**

| Kiashiria | Idadi ya Watu | Idadi ya watu wanaopata maji vijijini na Mijini | Wasiopata maji Salama |
|---|---|---|---|
| **Watu wanaokaa vijijini** | 40,501,519 (Asilimia 65.6) | 31,376,838 (Asilimia 77) | 9,372,302 (Asilimia 23) |
| **Watu wanaokaa mijini** | 21,238,6019 (Asilimia 34.4) | 18,052,810 (Asilimia 65) | 3,185,791 (Asilimia 35) |
| **Idadi ya Watu Wote** | 61,740,120 (Asilimia 100) | 49,429,648 (Asilimia 80.06) | 12,558,093 (Asilimia 19.94) |

***Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25***

### 3.31. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, pamoja na kwamba mabadiliko ya tabianchi ni moja ya sababu iliyoathiri utekelezaji wa bajeti na malengo ya Serikali, bado uwekezaji katika mazingira ni mdogo. Katika mwaka 2022/23 kiasi cha fedha kilichotumika kwa ajili ya shughuli za mazingira ni **shilingi bilioni 22.3**, kiasi hiki ni kidogo ukilinganisha na hali ya uharibifu wa mazingira. Kamati inaishauri Serikali kutafuta vyanzo vya uhakika vya mapato vya ndani na nje kwa ajili ya Mfuko wa Mazingira ili usaidie kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Mfano fedha za mfuko wa kufadhili miradi ya mabadiliko ya tabia nchi (climate change financing).

### 3.32. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali inatekeleza mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ikiwa ni moja ya njia za kutokomeza

umaskini. Mradi huu unatekelezwa kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mradi huu unakuwa endelevu pindi mkopo kutoka Benki ya Dunia utakapokoma.

## 4.0. MAENEO YA KIPAUMBELE YA MPANGO KWA MWAKA 2024/25

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2024/25 yanatoa kipaumbele katika kukamilisha miradi na programu za maendeleo ambazo hazikukamilika katika Mipango iliyopita. Hatua hii inamaanisha kwamba miradi mipya itakayotekelezwa ni ile yenye matokeo ya haraka ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi kulingana na rasilimali zilizopo na mazingira ya uchumi duniani.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi kwenye maeneo ya kipaumbele na kubaini masuala yafuatayo;

### 4.1. Miradi ya Kielelezo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** miradi ya kielelezo iliyoainishwa kwenye mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2024/25 ni michache ikilinganishwa na miradi ya kielelezo iliyoainishwa kwenye Mpango wa Miaka 5 (2021/22 – 2025/26). Miradi ambayo hijaorodheshwa ama haijatekelezwa au inatekelezwa kwa kususua. Miradi hiyo ni;

i. Mradi wa kufua umeme wa maji wa Rumakali (MW222);

ii. Ununuzi wa meli kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu;

iii. Ujenzi wa reli ya Mtwara - Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa kiwango cha kimataifa (SGR); na

iv. Mradi wa Magadi Soda Engaruka.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Hivyo, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba miradi hii inaendelea kuwa ya kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2024/25.

## 4.2. Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

### 4.2.1. Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa ukuaji wa uchumi wa Taifa na kubaini kwamba katika kipindi cha miaka 6 malengo ya makisio ya ukuaji wa uchumi yamekuwa hayafikiwi kwa wastani wa **asilimia 0.48** kutokana na sababu mbalimbali. Hata hivyo, Pato la Taifa kwa mwaka 2023 linakadiriwa kukua kwa **asilimia 5.2** kutoka **asilimia 4.7** ya mwaka 2022 sawa na ongezeko la ukuaji kwa **asilimia 0.5.** Vilevile uchumi huo unatarajiwa kuongezeka hadi **asilimia 5.8** mwaka 2024. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba makisio ya ukuaji wa uchumi iliyojiwekea yanakuwa halisi kwa sababu kutokufanya hivyo kutasababisha kutokufikia malengo na kuathiri utekelezaji wa mipango na bajeti. Jedwali namba 4 linaonyesha mwenendo wa maoteo na ukuaji halisi wa uchumi.

**Jedwali Na 4. Mwenendo wa Maoteo na Ukuaji halisi wa Uchumi (2017-2022)**

| Mwaka | Pato la Taifa | | |
|---|---|---|---|
| | Maoteo | Halisi | Tofauti |
| | A | B | (A-B) |
| 2017 | 7.1 | 6.8 | 0.3 |
| 2018 | 7.2 | 7.0 | 0.2 |
| 2019 | 7.3 | 7.0 | 0.3 |
| 2020 | 6.9 | 5.5 | 1.4 |
| 2021 | 5.6 | 4.9 | 0.7 |
| 2022 | 4.7 | 4.7 | 0 |

***Chanzo. Hotuba za Bajeti na Kitabu cha hali ya Uchumi***

### 4.2.2. Kupunguza nakisi kwenye urari wa biashara na huduma kwa kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa mikakati ya Serikali iliyobainishwa katika Mpango ili kupunguza nakisi kwenye urari wa biashara na huduma kwa kuongeza

mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Hata hivyo, mikakati iliyobainishwa katika Mpango kwenye sekta za uzalishaji hasusan kilimo, mifugo na uvuvi ni sawa na ya miaka iliyopita. Vilevile, Kamati imebaini kwamba mikakati mingine ambayo Serikali imejiwekea haijabainishwa katika Mpango. Kamati inaishauri Serikali ibainishe mikakati ya Kisekta ya kupunguza nakisi ya urari wa jumla katika Mpango na si kuachwa katika sekta husika.

## 5.0. UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2024/25

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali imepanga kutumia jumla ya **shilingi trilioni 15.32** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, sawa na **asilimia 32.32** ya bajeti yote ya mwaka 2024/25**.** Aidha, bajeti ya Maendeleo imeongezeka kutoka **shilingi trilioni 14.077** mwaka 2023/24 hadi **shilingi trilioni 15.325** smwaka 2024/25 sawa na ongezeko la **asilimia 8.8 (Trilioni 1.248)**. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuhakikisha kwamba inatenga kati ya **asilimia 30** hadi **40** ya Bajeti kwa ajili ya maendeleo kama inavyoonekana katika jedwali namba 5.

**Jedwali Na. 5. Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2022/23 – 2024/25 (Shilingi Trilioni)**

| **Mwaka** | **Bajeti ya Maendeleo** | **Jumla kuu ya Bajeti** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| 2022/23 | 15.006 | 41.48 | 36.18 |
| 2023/24 | 14.077 | 43.34 | 32.48 |
| 2024/25 | 15.325 | 47.42 | 32.32 |

***Chanzo. Hotuba za Bajeti na Kitabu cha hali ya Uchumi***

### 5.1. Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Kugharamia Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa vyanzo bunifu vya kugaharamia Mpango vilivyotajwa katika Mpango wa mwaka 2024/25 na kubaini kwamba vyanzo hivyo vimebainishwa pia katika Mpango wa tatu Maendeleo wa Miaka mitano na havijawahi tumika. Vyanzo hivyo ni :-

i. Hatifungani za Manispaa, Miundombinu, Buluu, Makampuni, Kiislamu pamona na Mazingira;

ii. Dhamana za Muda wa Kati;

iii. *Micro-Saving Bond na Lease Financing*; na

iv. Mitaji ya muda mrefu kupitia utaratibu wa *syndication* na bima na ugharamiaji hatarishi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali katika mwaka 2024/25 kuanza kutumia vyanzo hivyo katika ugharamiaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, ili Hatifungani za Halmashauri ziweze kutumika katika kugharamia miradi, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya utaratibu wa kuhamisha vyanzo vya Mapato ya Halmshauri kwenda Serikali kuu ili Halmashauri ziwe na uwezo wa kifedha kwa ajili ya kulipa riba na mtaji wa hatifungani zitakazotolewa.

### 5.2. Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Kutekeleza Mpango

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mpango wa Maendeleo wa Tatu wa Miaka Mitano umebainisha kwamba sekta binafsi katika mwaka wa fedha 2024/25 inatarajiwa kuchangia kiasi cha **shilingi trilioni 12.297** katika utekelezaji wa Mpango. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba hakuna mfumo uliowekwa na Serikali ili kubaini ni kiasi gani cha rasilimali fedha kimewekezwa na sekta binafsi katika utekelezaji wa mpango kwa miaka mitatu iliyopita. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali kama vile Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELLA) pamoja na Taasisi miamvuli za sekta binafsi kuweka mfumo utakaosaidia kupata takwimu hizo muhimu wakati wa upimaji wa utekelezaji wa Mpango.

## 6.0. UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa Utekelezaji Mpango wa mwaka 2022/23 na kubaini kwamba

katika mwaka wa fedha 2022/23 ni miradi **253** tu ndio iliyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini. Aidha, Kamati imepitia orodha ya miradi iliyokuwa imebainishwa katika kitabu cha nne cha bajeti (Volume IV) kinachohusu makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo (Public Expenditure Estimates Development Votes) na kubaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/23 Serikali ilikuwa na takribani miradi **2,572.** Hivyo, miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini ni **asilimia 9.84** ya miradi yote ya Serikali.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** vilevile, Kamati imefanya uchambuzi wa Mfumo wa Ufatiliaji na Tathmini uliopendekezwa katika Mpango na kubaini kwamba Mfumo huo unaongozwa na nyenzo zifuatazo: -

i. Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26;

ii. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25;

iii. Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma;

iv. Sheria ya Bajeti, Sura 439;

v. Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha;

vi. Waraka Na. 5 wa Hazina wa Mwaka 2020/21 Kuhusu Matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS); na

vii. Waraka Na. 1 wa Hazina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, ukiondoa Sheria ya Bajeti, Sura 439 ambayo katika sehemu ya 5 ya Sheria hiyo imeweka masharti kuhusu Utekelezaji, Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa wa Bajeti. nyenzo nyingine zimeshindwa kusimamia utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Serikali. Udhaifu katika Tathmini na Ufuatiliaji umekuwa ukionekana kwenye Taarifa ya Mbio za Mwenge na Ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wanapoibua ubadhilifu katika

miradi na mapungufu katika utekelezaji wa miradi. Madhara ya kutokuwa na Sera pamoja na Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji ni: -

i. Kuongezeka kwa gharama za miradi na miradi kutokukamilika kwa wakati;

ii. Miradi kutekelezwa kwa muda mrefu kuliko uliokusudiwa

iii. Miradi kutokufikia malengo yaliyokusudiwa; na

iv. Miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kutokana na sababu hizi Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kukamilisha utungaji wa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini na kisha kutunga Sheria ambayo itabainisha mgawanyo wa majukumu na adhabu katika kufanya Ufuatiliji na Tathmini. Aidha, pamoja na nia ya Serikali ya kuanzisha nafasi ya Naibu Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango atakayeshughulikia masuala ya ufuatiliaji na tathmini, nia hii haitoleta manufaa yanayotarajiwa kutokana na kukosekana kwa Sera na Sheria ambazo ndio msingi katika masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini.

## 7.0. VIHATARISHI NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa vihatarishi pamoja na mikakati ya kukabiliana navyo na kubaini kwamba, vihatarishi hivyo vimegawanyika katika makundi makuu matatu. Vihatarishi vya Kimkakati *(Strategic Risks),* vihatarishi vya Kifedha *(Financial Risks)* na vihatarishi vya utekelezaji *(Operation Risks)*. Kamati imebaini kwamba vihatarishi vya utekelezaji (Operation Risks) ni kati ya vihatarishi vinavyoweza kudhibitiwa kirahisi ukilinganisha na vihatarishi vingine. Kwa upande wa vihatarishi vya kimkakati na kifedha endapo vihatarishi vitajitokeza ni wazi kwamba vitaathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2024/25**.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba vihatarishi hivyo vinakuwa na Mpango wa Usimamizi wa vihatarishi kwa Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea ili kuhakikisha kwamba vinapojitokeza madhara yake hayawi

makubwa. Aidha, ni vyema Serikali ikapitia na kuongeza mikakati ya kudhibiti uharibifu wa mazingira kwa kutenga fedha za kutosha kwenye Mfuko wa Mazingira na Taasisi zinazosimamia mazingira ili kurejesha mazingira yaliyoharibika katika hali yake ya awali.

## 8.0. MAPUNGUFU YA UJUMLA YALIYOBAINIKA KWENYE MPANGO WA MWAKA 2024/25

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mapungufu mengine yaliyobainika katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/25 ni:-

i. Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango haijaweza kuainisha ajira zilizozalishwa kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya mwaka 2022/23;

ii. Miradi iliyokamilika katika mwaka wa fedha 2021/22 kuendelea kutolewa Taarifa kama vile imekamilika katika Mwaka 2022/23;

iii. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Utekelezaji wa Mpango haijabainisha manufaa yanayotarajiwa kupatikana mara baada ya miradi hiyo kukamilika;

iv. Baadhi ya miradi ya maendeleo kutobainishwa maeneo ambayo inatekelezwa;

## 9.0. MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA TAIFA 2024/25

### 9.1. Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa ukuaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani vya mapato kwa miaka mitano iliyopita 2017/18 - 2022/23. Takwimu zinaonyesha kwamba mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi na mapato ya Halmashauri yalikua kwa wastani wa **asilimia 10.5, 2.5 na 14.9** mtawalia. Hivyo, makisio ya ukuaji wa ukusanyaji wa mapato ndani kwa **asilimia 10.5** unaweza kufikiwa.

## 9.2. Vihatarishi vya Madeni Sanjari

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Sheria ya Mikopo na dhamana ya Serikali Sura ya 134 inatoa fursa kwa Serikali kutoa dhamana kwa mashirika ya umma ili yaweze kukopa katika mabenki na taasisi za kifedha kwa lengo la kupata mitaji. Hata hivyo, endapo shirika la umma lililopewa dhamana likishindwa kulipa mkopo Serikali inawajibika kurejesha mkopo kwa niaba ya shirika au kampuni husika iliyodhaminiwa. Endapo hali hii itajitokeza ni wazi kwamba itaongezea na itaathiri deni la Serikali na Bajeti ya Serikali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya uwezo wa kulipa deni la Serikali endapo madeni sanjari yatatakiwa kulipwa na Serikali. Vilevile, ni vyema makampuni ya Serikali yanayojiendesha kibiashara kutafuta mitaji katika masoko ya mitaji kama vile (*Dar es salaam Stock Exchange-DSE)* ili kupunguza mahitaji ya kudhaminiwa na Serikali**.**

## 9.3. Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa na Kusimamia Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi Katika Taasisi za Umma. Kamati imebaini kwamba, Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma unaotumika hivi sasa ni wa mwaka 2012. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia upya Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika sekta ya umma ili uendane na wakati.

## 9.4. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mwongozo unawaelekeza maafisa masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma kuanza maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Muda wa Kati *(Medium Term Expenditure Framework-MTEF)* mara baada ya Mwongozo kuidhinishwa. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba ukomo wa bajeti kwa mafungu mbalimbali unatolewa mwezi Machi, 2024 mara baada ya Mpango na Mwongozo kuwasilishwa Bungeni. Hatua hii hulazimu baadhi ya Maafisa Masuuli kubadili bajeti zao na kuandaa vitabu kwa ajili ya Kamati za Bunge, vinavyoendana na ukomo uliotolewa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, ratiba hii imekuwa na madhara kwa Serikali za Mitaa hasa pale ambapo bajeti inakuwa imekwisha pitishwa na vikao vyote vya Halmashauri na kikao cha Ushauri wa Mkoa (RCC). Hivyo mabadiliko hufanywa na Mkurugenzi bila kushirikisha vikao vya maamuzi. Kamati inaishauri Serikali kuwa ni vyema mwongozo wa uandaaji wa Bajeti utakapotolewa uende sanjari na ukomo wa kila fungu na endapo mabadiliko yanafanyika yawe ni ya kuongeza Bajeti na si kupunguza.

### 9.5. Uwasilishaji na Uchambuzi wa Mpango na Bajeti

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha nakala mango *(hard copy)* mbili (2) ya makadirio ya mapato na matumizi ya fungu husika, siku tano (5) kabla ya kuanza uchambuzi kwa kuzingatia ratiba ya uchambuzi. Kwa kuwa makadirio ya mapato na matumizi ya fungu husika hufanyika kwa kutumia mifumo ya CBMS na PlanRep, Kamati inaishauri Serikali kuboresha mifumo hii, ili Taarifa zinazowasilishwa kwa nakala mango zipatikane kupitia mifumo. Lengo ni kupunguza gharama za kusafiri kwa ajili ya kuwasilisha nakala mango.

### 9.6. Kiwango cha Ubadilishaji Fedha

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mwongozo unaonyesha kwamba katika maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia kiwango elekezi cha ubadilishaji wa fedha za kigeni ambacho ni **dola moja ya Marekani kwa shilingi za Tanzania 2,555**. Kamati imebaini kwamba viwango vya ubadilishaji fedha nchini kwenye mikataba hutumika kwa namna mbili. Moja ni kiwango kilichokubalika katika mkataba na pili ni kutokana na kiwango cha kubadilisha fedha cha siku husika kwa mujibu wa Taarifa za Benki Kuu. Hivyo Kamati inaishauri Serikali ni vyema Maafisa Masuuli watumie kiwango cha ubadilishaji fedha cha siku husika kwa mujibu wa Taarifa za Benki Kuu wakati wa kufanya malipo ya bidhaa na huduma au siku mkataba unapoingiwa ili kutopoteza fedha za Serikali endapo kiwango hiki kitakuwa kikubwa kuliko bei ya soko.

## 9.7. Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Bunge lilitunga Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma Sura 410. Kifungu cha 56(3) kinataka taasisi nunuzi kutoa upendeleo kwa zabuni za baadhi ya bidhaa zilizotengenezwa, zilizochimbwa au kuzalishwa nchini kwa kuzingatia masharti yatakayoainishwa katika kanuni. Kamati imebaini kwamba kanuni za Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma zinatarajiwa kuongeza kiwango cha upendeleo wa ndani kutoka **Shilingi bilioni 5** hadi **Bilioni 50** hazijatangazwa. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kukamilisha mapema iwezekanavyo Kanuni hizo na kuzitangaza kwenye gazeti la Serikali kabla ya mwaka wa fedha 2024/25 kuanza.

## 9.8. Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imebaini kwamba mikakati ya Serikali wa kuongeza fedha za kigeni nchini, hauendi sanjari na mkakati wa kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa Wizara, Idara, Wakala na Taasisi za Serikali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka sharti la lazima, kwa maafisa masuuli wote kuhakikisha kwamba ununuzi wa bidhaa na huduma kuanzia mwaka wa fedha 2024/25 kipaumbele kiwe kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa na kupatikana nchini kabla ya kuagiza au kununua bidhaa na huduma nje ya nchi.

## 9.9. Udhibiti wa Ununuzi kwa Kutumia Rasilimali za Ndani (Force Account)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imebaini kwamba katika kudhibiti matumizi ya fedha za umma, Maafisa Masuuli wameelekezwa kuzingatia Mwongozo wa utaratibu wa Matumizi ya rasilimali za ndani (*Force Account)* wa mwaka 2020 katika utekelezaji wa miradi ili kupunguza gharama. Kwa kuwa kifungu 75(2) cha Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023, Sura 410, kimefanya mabadiliko katika baadhi ya masharti yaliyokuwepo kwenye utaratibu wa Matumizi ya rasilimali za ndani (*Force Account)* wa awali, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mwongozo mpya wa mwaka 2023.

## 9.10. Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mwongozo haukutoa maelekezo kwa maafisa masuuli wa ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha kwa ajili ya kufanya Ufuatiliaji na Tathimini. Kamati inaitaka Serikali kuweka sharti la lazima kwa maafisa masuuli wote kutenga fedha kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini ya miradi ya maendeleo katika ofisi zote za umma zenye miradi.

## 10.0. MAONI YA JUMLA

## 10.1. Miradi ya Kilelezo ya Muda Mrefu Ambayo Haijakamilika

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa miradi ya kielelezo ambayo imekuwa haitekelezwi kwa muda mrefu ili kubaini changamoto zinazoikabili. Miradi hiyo ni Mradi wa Magadi Soda Engaruka, Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga, Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo, Mradi wa kufua umeme wa maji wa Rumakali **(MW 222)**, Mradi wa kufua umeme wa maji wa Ruhudji **(MW 358)** na Miradi ya kuendeleza maeneo huru ya kuongeza mauzo nje *(Special Economic Zone-SEZ)* na *(Export Processing Zone-EPZ)*. Masuala yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

i. kukosekana kwa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo;

ii. kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu na upembuzi wa kina kabla ya kuweka miradi ya kimkakati kwenye Mpango;

iii. kutolipa fidia kwa maeneo ambayo miradi inatarajiwa kutekelezwa;

iv. miradi ya kimkakati kuwa mingi ukilinganisha na uwezo wa Bajeti ya Serikali kila mwaka;

v. kukosekana kwa fedha kwa ajili ya kulipia leseni zinazotolewa na Wizara;

vi. ushirikishwaji duni wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi; na

vii. miradi kutekelezwa kwa kutegemea Bajeti ya Serikali pekee.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati ina ushauri ufuatao ili kutanzua vikwazo vya utekelezaji wa miradi hiyo:-

i. Kutekeleza miradi michache yenye manufaa itakayo kamilika kwa wakati kuliko kuwa na miradi mingi isiyokamilika kwa wakati;

ii. Miradi yenye sura ya kibiashara itekelezwe kwa ushirikiano na Sekta Binafsi kwa Mfumo wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP);

iii. Kuhakikisha kwamba miradi ya madini adimu inatekelezwa kwa wakati ili matumizi yake yasipitwe na wakati na hivyo kushindwa kuliletea Taifa manufaa;

iv. Kulipa fidia ya miradi kabla ya kuanza hatua za utekelezaji;

v. Kuanzisha utaratibu maalumu wa kusamehe ada za leseni kwa miradi ambayo inamilikiwa na Taasisi za Serikali na inatakiwa kulipa ada ya leseni kwa Taasisi nyingine ya Serikali;

vi. Kuandaa miundombinu ya msingi kabla ya kuanza kutekeleza mradi;

vii. Serikali kupitia Tume ya Mipango kuanzisha kitengo mahsusi cha kusanifu na kuhakiki ubora wa miradi iliyo sanifiwa ili kukabiliana na changamoto ya usanifu duni; na

viii. Kuhakikisha kwamba hatua zote za Mradi kama vile usanifu wa awali na usanifu wa kina zinakamilika kabla ya kuanza kutekeleza mradi.

### 10.2. Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi za Umma Kutoshirikiana wakati wa Kupanga na Kutekeleza Miradi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imebaini kwamba Wizara, Idara na Taasisi za Umma hazishirikiani katika kutekeleza miradi. Hali hii imesababisha baadhi ya Taasisi kutekeleza miradi katika ngazi ya Serikali za Mitaa lakini uratibu na usimamizi hufanyika Serikali Kuu na hivyo miradi kukosa uangalizi na kutekelezwa chini ya kiwango.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mfano mwingine ni Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira. Wizara zote hizi zinachimba mabwawa na visima kwa matumizi tofauti, mfano mabwawa ya kilimo, uvuvi na umwagiliaji. Miradi hii inaweza kutekelezwa na Wizara moja ya maji na bwawa hilo likatumika kwa shughuli za kilimo, uvuvi na umwagiliaji. Kukosekana kwa ushirikiano kunasababisha uwepo wa mabwawa madogo na visima vifupi visivyokuwa na tija. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba Wizara zinapotekeleza miradi ambayo ama inashabihiana au ni mtambuka wahusika wote washirikishwe na Fedha zitengwe kupitia Fungu moja kuliko kutawanya fedha kidogo kidogo katika mafungu mengi.

### 10.3. Ushirikiano wa Kimataifa na Uchumi wa Kidiplomasia

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kubaini kwamba imejikita katika kujenga vitega uchumi, ofisi na makazi ya Watumishi na Balozi nje ya nchi kwa lengo la kuboresha miundombinu na kuongeza mapato. Kamati inashauri Balozi zetu pia kujikita katika dhana ya Uchumi wa Kidiplomasia yenye lengo la kujenga ushirikiano wa Kimataifa, kuongeza uwekezaji wa kigeni, biashara ya bidhaa na huduma nje ya nchi, na kusaidia nchi kujinasua kwenye umaskini na mdororo wa uchumi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/25 Ofisi za Balozi zinatekeleza majukumu yanayoakisi dhana ya Uchumi wa Kidiplomasia pamoja na kuimarisha miundombinu yake.

### 10.4. Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma umeongezeka kutoka **shilingi trilioni 67.79** mwaka 2020/21 hadi **shilingi trilioni 70.67** mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la **asilimia 4.24**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina hayaakisi uwekezaji uliofanywa na Serikali. Ambapo, katika mwaka 2022/23 Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikusanya **shilingi trilioni 1.011** ukilinganisha na uwekezaji wa **shilingi trilioni 70.67.** Aidha, uwekezaji huu ni kwa mashirika yote, yanayojiendesha kibiashara na yanayotoa huduma. Kamati inashauri masuala yafuatayo kuhusiana na ofisi hii:-

i. Kutenganisha mitaji iliyotolewa na Serikali kwa Mashirika yanayotoa huduma na yanayojiendesha kibiashara ili kupima ufanisi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kukusanya mapato na kupima ufanisi wa utendaji kazi wa Mashirika;

ii. Kupitia upya Sheria ya Msajili wa Hazina ili kuondoa mapungufu yaliyopo na kuakisi muelekeo mpya na majukumu ya ofisi hiyo;

iii. Kuanzisha Mamlaka ya Uwekezaji wa Umma (Public Investment Authority);

iv. Kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ambao utatumika kuwezesha kimtaji Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara; na

v. Kuainisha vyanzo vya mapato kwa ajili ya Mfuko wa Uwekezaji.

### 10.5. Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura 103 imefanyiwa marekebisho makubwa mara mbili mwaka 2018 na 2023. Lengo la marekebisho ilikuwa ni kutatua changamoto zilizokuwa zinakwamisha utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia. Hata hivyo, utekelezaji wa miradi kwa njia

hii umekuwa si wa mafanikio na orodha ya miradi hiyo imekuwa ikijirudia kila mwaka. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba changamoto inayokabili utekelezaji wa miradi kwa njia ya PPP ni mtazamo hasi wa watumishi wa umma kutumia njia hii kutekeleza miradi na kukosekana kwa fedha kwa ajili ya kuandaa maandiko yanayokidhi vigezo vya miradi inayotekelezwa kwa njia hii.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali katika mwaka wa fedha 2024/25 kuwaelekeza Maafisa masuuli kubainisha miradi yote iliyopo katika maeneo yao inayoweza kutekelezwa kwa mfumo wa PPP. Aidha, Serikali itenge Bajeti ya kutosha katika Mfuko wa Uwezeshaji wa Miradi ya PPP (PPP Facilitation Fund) ili zitumike kuandaa maandiko yatakayowezesha miradi kutekelezwa kwa njia ya PPP.

### 10.6. Mwenendo wa Soko la Hisa

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Sheria ya Mawasiliano ya kieletroniki na Posta, Sura 306 kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016, inazitaka kampuni zote za mawasiliano kujiorodhesha kwenye Soko la Hisa la Dar-es-salaam. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kwa takribani miaka 7 ni kampuni moja tu ya mawasiliano ya Vodacom ambayo imejiorodhesha katika soko. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha makampuni yote ya mawasiliano yanatekeleza takwa hilo la kisheria ili watanzania wanufaike na mapato yanayotokana na sekta hiyo.

### 10.7. Kuanzishwa kwa Mabaraza ya Biashara Kwenye nchi ambazo ni wabia wakubwa wa Biashara *(Tanzania Business Council – TBC)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kati ya maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na kuimarisha utendaji wa mabaraza ya biashara katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Kamati inaishauri Serikali itekeleze kipaumbele hiki na Balozi zetu zilizopo kwenye nchi ambazo ni wabia wakubwa wa biashara na Tanzania, kama vile China, India Falme za Kiarabu, Afrika ya Kusini, Kongo DRC, Rwanda, Burundi, Kenya na Zambia. Mabaraza haya yatakuwa kama kitovu cha biashara kati ya wafanyabishara wa kitanzania

na nchi hizo. Pamoja na kuwa kitovu, mabaraza haya yatahusika na utoaji wa taarifa mbalimbali za mabadiliko ya kisheria katika nchi hizo.

**10.8. Uwezeshaji wananchi Kiuchumi *(Economic Empowernment)***

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa Mpango wa Mwaka mmoja na kubaini kwamba hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kuwezesha wananchi zimetawanyika katika sekta mbalimbali na hivyo ni vigumu kupima ufanisi wake. Hata hivyo, pamoja na uwepo wa Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004 *(The Economic Epowerment Act)* iliyoanzisha Baraza la Uratibu wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(National Economic Empowerment Council)*, Baraza hilo halijaweza kusimamia jitihada za uwezeshaji na badala yake limekuwa ni chombo cha uratibu wa shughuli za uwezeshaji. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuipitia upya Sera na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili Sheria hiyo ijumuishe hatua zote za uwezeshaji zilizotawanyika katika sekta na sheria mbalimbali ili zisimamiwe na Sheria moja.

**10.9. Tofauti ya Takwimu za Serikali**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** moja ya changamoto ambayo Kamati imekuwa ikikumbana nayo kwa kipindi kirefu ni utofauti wa Takwimu za Serikali. Utofauti huo unaonekana katika Taarifa mbalimbali za Serikali katika kipindi kimoja au Taasisi mbili za Serikali kutoa Takwimu zinazotofautiana juu ya suala moja. Utofauti huu umekuwa unaleta mkanganyiko katika uchambuzi hasa pale ambapo ushauri wa kamati unahitaji takwimu. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha katika mwaka wa fedha 2024/25 Takwimu zinazowasilishwa ziwe zimefanyiwa marejeo na kuhakikisha kuwa ni za uhakika ili Kamati iweze kushauri vyema.

**10.10. Ujenzi wa Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** moja ya changamoto ambayo inaikabili Serikali ni uvunjaji wa Mikataba bila kufuata Sheria au Mikataba kutofanyiwa upekuzi na upembuzi wa kutosha kabla ya kusainiwa. Hata hivyo, Ofisi inayotakiwa kusimamia na kutekeleza majukumu

hayo ipo katika Mikoa minne tu ya Tanzania. Hivyo, kuna ulazima wa Serikali kuongeza kasi ya  ya ujenzi wa Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali walau kwa kila kanda ili zitoe Huduma ya ushauri kwenye mikataba kwa ufanisi.

### 10.11. Reli ya TAZARA *(Cape Gauge Railway-CGR)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kutokana na uwekezaji unaofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam ili kuongeza ufanisi katika upokeaji wa meli na uondoshaji wa mizigo ni wazi kwamba Reli ya TAZARA itahitajika kwa kiasi kikubwa. Reli hii itasaidia kusafirisha mizigo inayoenda katika nchi za Zambia, Malawi na DRC Kongo. Hata hivyo, moja ya changamoto inayokwamisha uwekezaji katika Reli ya TAZARA kwa muda mrefu ni Sheria inayosimamia uendeshaji wa reli hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa mabadiliko ya Sheria hiyo ili uwekezaji ufanyike na Reli hii isaidie katika uondoshaji wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam.

### 10.12. Miradi ya Nishati

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Sekta ya Nishati katika siku za hivi karibuni imekumbwa na changamoto ya upatikanaji wa umeme wa uhakika. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Taifa limebarikiwa na vyanzo vingi vya kuzalisha umeme lakini havitumiki kikamilifu. Aidha, Kamati imefanya tathmini na kubaini kwamba changamoto kubwa iliyopo ni upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi katika sekta hiyo. Kamati, inaishauri Serikali kutumia njia ya ubia ili kupata fedha za kuwekeza katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia upepo, makaa ya mawe, jua na jotoardhi

### 10.13. Mradi wa BBT (Building Better Tomorrow)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mradi wa Building Better Tomorrow - BBT unatekelezwa kupitia fedha za mkopo wa ECF  kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Mradi huo unatekelezwa na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Lengo la mradi huu ni kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo kuhusu kilimo cha kisasa, mifugo na uvuvi, kuwafadhili vijana

mashamba, mitaji pamoja na kuwaunganisha kwenye fursa za masoko. Jumla ya **shilingi bilioni 100** zilitengwa kwa ajili ya wizara ya kilimo na **bilioni 29.72** kwa Wizara ya Ufugaji katika mwaka wa fedha 2022/23.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Taarifa ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo imebainisha kwamba mradi wa BBT umefikia katika hatua zifuatazo: Kubainisha, kupima na kuweka mawe ya upimaji kwa ajili ya kuyapatia hati miliki mashamba makubwa ya pamoja, kukamilika mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana 812 wa BBT katika vituo atamizi, na kulipa fidia ya shamba la Chinangali lenye ukubwa wa ekari 400, kutolewa kwa mafunzo kwa vijana 200 wanaojishughulisha na uvuvi na ukuzaji viumbe maji na ufugaji kwa vitendo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imechambua mradi huu na inapenda kutoa ushauri ufuatao:-

i. Serikali ina miliki mashamba ambayo tayari yameshapimwa na kuandaliwa lakini hayatumiki mfano, mashamba ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), mashamba ya TIC, mashamba ya magereza, na mashamba yaliyo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina (OHM) . Hivyo Kamati inaishauri Serikali kutumia mashamba hayo kwa ajili ya kutekeleza mradi huu ili ikusaidia kupungunza gharama zinazotumika kupima na kuandaa mashamba mapya.

ii. Kwa kuwa kuna vyuo vinavyotoa mafunzo ya kilimo na ufugaji nchini kama vile Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, na uwepo wa wahitimu wenye ujuzi na utaalamu wa masuala ya kilimo na mifugo ambao hawana ajira. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwiano wa walau asilimia 50 kwa 50 kwa vijana wenye ujuzi wa masuala ya kilimo, ufugaji na uvuvi, na vijana wasiokuwa na ujuzi ili kusaidia kupunguza gharama za kutoa mafunzo na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mradi huo.

## 10.14. Udhibiti wa Matumizi ya Serikali

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa miaka mitano (2018/19 – 2022/23) na kubaini kwamba kiasi cha kutokufikia malengo ya bajeti kimepungua kutoka **asilimia 16** mwaka 2018/19 hadi **asilimia 1.5** mwaka 2022/23. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa makadirio ya makusanyo ya mapato yamekuwa na uhakika na hivyo kupunguza nakisi kati ya kiasi kilichokadiriwa na makusanyo halisi. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada inazofanya katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili yakidhi mahitaji ya bajeti. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali ifanye mapitio ya matumizi ya Umma ili kuhakikisha kwamba matumizi hayo yanaenda sanjari na mapato (public expenditure review). Vilevile, kuhakikisha kwamba matumizi ya maeneo ya kipaumbele yanazingatiwa kwanza na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima.

**Jedwali Na.6 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali (Shilingi trilioni)**

| Mwaka wa Fedha | Maoteo ya Bajeti | Bajeti Halisi | Asilimia | Tofauti ya makisio na Halisi | Asilimia ya kutofikia lengo |
|---|---|---|---|---|---|
| 2018/19 | 32.50 | 27.30 | 84.0 | (5.20) | 16.0 |
| 2019/20 | 33.10 | 29.50 | 89.1 | (3.60) | 10.9 |
| 2020/21 | 34.90 | 32.30 | 92.6 | (2.60) | 7.4 |
| 2021/22 | 37.90 | 37.20 | 98.2 | (0.70) | 1.8 |
| 2022/23 | 41.50 | 40.90 | 98.5 | (0.60) | 1.5 |

***Chanzo: Hotuba za Bajeti na Sheria za Matumizi***

## 11.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba nitumie fursa hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), hakika umethibitisha uwezo wako kwa Taifa na Kimataifa katika kusimamia shughuli za Kibunge. Aidha, napenda kumshukuru Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb na Naibu Spika kwa ushirikiano wake na Kamati katika kipindi chote cha utendaji kazi wake. Vilevile nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Doto

Mashaka Biteko Naibu Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Rais Kushika wadhifa huo, Tunaamini chini ya Uongozi wa Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Mb Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mtakuwa nguzo imara katika kusimamia shughuli za Serikali.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru Mhe. Prof. Kitila Mkumbo, Mb Waziri Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Mb, Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mb Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao na Kamati. Aidha, Kamati inawashukuru Dkt. Natu Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na Ndg. Lawrence Mafuru Katibu Mtendaji Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2024/25 pamoja na Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri na ushirikiano wao katika kuchambua Mpango na Mwongozo ili kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Zainab Athumani Katimba, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb- Mjumbe

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa namna ya kipekee nimshukuru pia Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati Ndg. Lilian Masabala, Ndg. Wilfred Akasi, Ndg. Jenifer Maurice na Ndg. Trifina Karaguza, kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo,
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
06 Novemba, 2023

**MWENYEKITI:** Ahsante Makamu Mwenyekiti. Sasa tunaanza mjadala, tunaanza na Mheshimiwa Ndaisaba, jiandae Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza na mimi nianze kabisa kwa dhati ya moyo wangu kumpongeza Waziri wa Fedha, Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, pamoja na Waziri wa Mipango, Ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, kwa kweli nimesikiliza mawasilisho yao yote vizuri sana yanatia matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee niweze kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuweza kuwateua ndugu zangu hawa wawili, mmoja aweze kuendesha Wizara ya Fedha na mwingine akae kwenye Mipango, hakika mapacha wale mnavyowaona pale walivyopendeza kazi yao ni nzuri, wanaifanya vizuri na kwa kupitia mawasilisho waliyowasilisha hapo tunaona matumaini na mambo mengi yanakwenda kufanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lolote linalohitaji kuendelea kwa haraka na kwa kasi halina budi ya kuwekeza kwenye miundombinu ya ardhini, miundombinu ya usafirishaji kwenye anga na kwenye maji. Kwa kuwa Taifa letu linahitaji kuendelea kwa haraka hatuna budi nasi kama Tanzania kuweza kuwekeza kwenye miundombinu ya aina hiyo, mathalani kwa upande wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana nami pamoja na Wabunge wote, kwamba Tanzania ni lazima tuendelee kuwekeza kwenye ujenzi wa reli ya kisasa *SGR,* lazima tuendelee kuwekeza kwenye kupanua viwanja vya ndege lakini na kuweka meli za kisasa ili ziweze kusaidia Watanzania kusafirisha mizigo yao na wao wenyewe kusafiri kutoka eneo moja kwenda eneo jingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani kwa upande wa Jimbo langu la Ngara, pale Ngara kuna barabara ya kimkakati ambayo kama haitajengwa ndoto ya Tanzania ya kuvuna *nickel*, ambayo ni madini ya kimkakati yanayosubiriwa duniani ili yaende yakatengeneze betri hiyo ndoto haitatimia. Mheshimiwa Kitila Mkumbo, nataka nikupe taarifa hapa kwamba barabara ya kutoka Mlugarama kwenda Rulenge, kutoka Mlugarama – Rulenge – Kumbuga kilometa 75 na barabara ya kutoka Nyakahura – Kumbuga – Mlugarama – Mrusambaga – Gaumo kilometa 34 na barabara ya kutoka Rulenge – *Tembo Nickel* kilometa 32, jumla ni kilometa 141 kama hazitajengwa Mheshimiwa Kitila Mkumbo ile *nickel* ya Ngara haitovunwa kwa miaka 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa utaratibu wa Serikali uliopo sasa hivi wa kutoa shilingi bilioni tatu ile barabara ijengwe kilometa tatu kila mwaka na hapa tuna kilometa 141 itatuchukua miaka 47 kwa ile barabara kujengwa na ikakamilika. Kupanga ni kuchagua, tumepanga kuilisha dunia kuiuzia *nickel* iliyopo Tanzania na *nickel* hii siyo Tanzania pekee, hii *nickel* iko Tanzania lakini ndiyo *nickel* ya kipekee Afrika na pengine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kama Taifa tumeshaingia mikataba na wawekezaji. Wawekezaji wako pale kwenye *ground* lakini hawawezi kusafirisha makontena na mizigo mikubwa kutoka Dar es Salaam kuipeleka kule ili waanze kujenga ule mgodi kwa sababu ile barabara haipitiki na hakuna namna yoyote hata madaraja yale kuna mizigo ikipita pale madaraja yatadondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kupanga ni kuchagua tumeshaingia, tumeshaasaini mikataba na wawekezaji muda muafaka wa kujenga ile barabara kwa kiwango cha lami ni sasa ili zile *nickel* ziweze kutuletea tija kwa Taifa eneo la kwanza. Kwa hiyo Mheshimiwa Kitila Mkumbo, kwa kweli sitopitisha mpango huo kama tutapiga kura au hata bajeti ya mwakani kama hii barabara haijaingizwa kwa sababu nitashika shilingi mpaka hii barabara iingizwe ili zile *nickel* ziweze kuchimbwa na wananchi wangu waendelee kufanya kazi kwenye mgodi ule waendelee kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa kweli kwa unyenyekevu mkubwa sina nia ya kushika shilingi maana najua utaweka Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, kama utajisahau tunaweza tukafikia huko lakini kwa unyenyekevu mkubwa nikuombe kabisa kwenye mipango yetu hii ya maendeleo ya Taifa hasa huu wa 2024/2025 ujitahidi hii barabara iingie kwenye mpango ili uweze kupewa fedha na iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni reli ya kisasa ya *SGR* kutoka Isaka ambayo ipo Kahama mpaka Rusumo. Kupanga ni kuchagua kutoka pale Rusumo mpakani na Rwanda, ni kilometa 200 mpaka Kigali kutoka Kigali kwenda mpaka Goma ni kilometa 150, kujenga kipande cha *SGR* cha kisasa kutoka Isaka mpaka pale Rusumo ni kilometa 338, kupanga ni kuchagua

tukizubaa Watanzania soko la la Congo, Goma yote litachukuliwa na mataifa mengine ambayo yataendeleza *SGR* kutokea Kenya kuingia Uganda mpaka Rwanda na huko Goma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania Mwenyezi Mungu ametuwezesha kwamba sasa *SGR* inafika pale inakwenda mpaka kwenye kiwanda cha uchenjuaji cha *Tembo Nickel* pale Buzwagi, sasa Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, naomba tusaidie hili Taifa liweze kwenda kunufaika na masoko ya Congo na Rwanda, sisi tutajenga reli yetu mpaka pale mpakani lakini wenzetu hawatashindwa kujenga hizo kilometa 150. Ninaomba eneo hili liweze kufanyiwa kazi na liingizwe kwenye mpango wa maendeleo ya Taifa ili kama Taifa tuweze kunufaika na rasilimali ya sisi kuwa katikati ya mataifa mengine yanayotuzunguka.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kilimo. Ninapendekeza Wizara ya Kilimo ipewe fedha za kutosha ili iweze kuwekeza kwenye kilimo kwa sababu mpaka dakika hii kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Tanzania na Watanzania wanasubiria kilimo ili waweze kuishi. Taasisi za kilimo kama vile *TARI* na Bodi ya Kahawa bila kuweka kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa na kuhakikisha wanapata fedha ili waweze kuzalisha miche ya kutosha, nataka nikuambie tutakuwa hatuwasaidii Watanzania, namna pekee ya kuwasaidia Watanzania ni kuwawezesha kupata mbegu na pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameweka mazingira mazuri kwa Watanzania kuweza kupata mbolea za ruzuku. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri Bashe, ameweka utaratibu mzuri sasa Watanzania wanapata mbolea za ruzuku, lakini sasa twende mbele tuwasaidie Watanzania kupata miche. Kwa mfano, upande wa Wilaya ya Ngara, mahitaji yetu ya miche ya kahawa 2024/2025 ni miche milioni tatu ya kahawa. Kwa mfano ukitupatia miche ya Robusta, tutaweza kupanda hekta 3,000, kwenye hekta hizo tutaweza kuvuna kilo za kahawa ambayo ni safi 3,300,000 ukizidisha mara mbili kwa maana ya kahawa yenye maganda tutapata kahawa yenye maganda zaidi ya 6,600,000 tukiuza kwa bei ya juzi ya shilingi 3,040

Wanangara tutaweza kutengeneza fedha zaidi ya bilioni 18 kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama hapa kuchangia Mpango wa Maendeleo ya Taifa, hii ndiyo *vision*, huu ndiyo muonekano na mkifanya hivi nchi nzima kwa maeneo mengi, Watanzania wanakwenda kutoka kwenye dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumwa kama Mwakilishi wa Wananchi wa Ngara, nimetumwa nije hapa niwe kisemeo, nije niwatetee na kwa kuwa sasa tunakwenda kutengeneza Mpango wa Maendelea ya Taifa na kwa kuwa hakuna mradi utakaotekelezwa bila kuingia kwenye mpango wa maendeleo ya Taifa, ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa Wizara ya Kilimo tuende tuiwezeshe, iweze kuzalisha miche ya kutosha ili wananchi na Watanzania wanaohitaji kuwekeza kwenye kilimo waweze kupata miche hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa upande wa Ngara, naomba Mpango wetu uainishe miche 3,000,000 ya kahawa na miche 2,000,000 ya parachichi tumechoka kuendelea kuishi kwenye umaskini. Tunataka ifike mahali sasa na sisi tuwe matajiri tujivunie kutumia ardhi ambayo Mwenyezi Mungu, alitupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine. Kuna miradi mingi sana kwenye kilimo hasa ya masoko ya kimkakati ilishajengwa muda mrefu na kutelekezwa. Katika eneo hili naomba nisimung'unye maneno kuna watu walipiga hela lakini kwa bahati nzuri hazikupigwa katika kipindi hiki, zilipigwa kipindi mimi sijawa Mbunge, wamekwenda pale Kabanga wametengeneza soko la kimkakati la Kimataifa lakini limejengwa likaishia katikati na mradi ulikuwa unasimamiwa na Wizara ya Kilimo, moja kwa moja kutoka huku Dodoma. Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, hawakuwa na nafasi ya kuweza kusimamia ule mradi, watu wamepiga hela *document* zinaonekana mradi umekamilika, majengo yamebaki yametelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tunapotengeneza Mpango wa Maendeleo ya Taifa, tuhakikishe miradi hii

iliyosimama muda mrefu tunaijenga inakamilika, tumechoka kuona watu wanatoka Bunjumbura wanapitiliza kwenda kununua dagaa Bukoba na wanakwenda kununua vitu Dar es Salaam, soko likiwepo pale la kimkakati watu watatoka nje ya nchi watakuja Ngara kununua vitu mpakani, sasa miradi yote nchi nzima iliyotelekezwa muda mrefu, Mpango wetu wa Maendeleo ya Taifa ulenge kwenda kuhakikisha miradi hiyo inakamilika, kwanza inatuchefua, pili inatunyima kura, tatu inaonekana hatuko *serious*, ninaomba Wabunge wote wenye miradi ambayo haijakamilika huu ndiyo muda muafaka wa kuhakikisha miradi hii inaingizwa kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa na tunahakikisha tunasaidia Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele yako ya pili hiyo malizia sekunde mbili.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia na eneo la mwisho la kuwasaidia Watanzania kupata vitambulisho vya Taifa. Kuna Watanzania sasa hivi hawawezi kumiliki laini ya simu kwa sababu hana *NIDA*, kuna Watanzania wa Ngara hawawezi kwenda Vyuo Vikuu kwa sababu hawana kitambulisho, hawezi kupata *admission* ya Chuo Kikuu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwandikie Waziri.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa naunga mkono hoja lakini naomba mpango usaidie Watanzania kupata vitambulisho vyao vya utaifa ili waweze kufurahia huduma ndani ya Taifa lao na wananchi wa Ngara wapewe kipaumbele, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nyongo, Mheshimiwa Nahodha na Mheshimiwa Charles Kimei ajiandae.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nakushukuru sana wewe na nikupongeze kwa kazi yako nzuri ya kutuongoza, wewe pamoja na Mheshimiwa Spika. Nichukue fursa hii kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia

Suluhu Hassan Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya. Vile vile nawapongeza sana Mawaziri hawa wawili ambao leo wameweza kuwasilisha mpango na masuala yote na mikakati ya utekelezaji wa mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza na niendelee kupongeza kwamba Mheshimiwa Rais wetu amekuwa na maono makubwa sana kwa maana ya kujenga miundombinu kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Miundombinu inayojengwa, kwa mfano *SGR*, tunatambua kabisa ndio msingi wa kwenda kuinua uchumi wa nchi yetu; na vile vile ujenzi wa barabara pamoja na miundombinu mingine kwa mfano uboreshaji wa ujenzi wa bandari na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Mpango, Mheshimiwa Waziri kama utafikiria *SGR* na ambao utekelezaji unaendelea, tusipofikiria kujenga barabara na kuimarisha barabara kubwa, kwa mfano, barabara kutoka Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma kwenda Kanda ya Ziwa Pamoja na kwamba kuna *SGR* tunajenga mfikirie kujenga hizi barabara na kuzitanua. Haiwezekani leo tupo karne ya 21 tunapishana barabara moja, malori makubwa, mabasi, magari madogo tunapishana kwenye barabara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kwa sababu tukipata *breakdown* kidogo barabara hizi inakuwa ni *chaos,* watu wanasimama wanashindwa kutembea, barabara zetu zaina hali mbaya. Tusije tukaegemea kwenye *SGR* tukasahau barabara. Fikiria kujenga barabara nne Dar es Salaam - Morogoro, Morogoro – Dodoma, Dodoma – Singida kwenda Mwanza na upande wa Magharibi. Jengeni barabara hizi *highway* ziwe nne watu waweze kutembea, ndiyo uchumi wenyewe, siyo starehe. Barabara siyo starehe, barabara ni uchumi. Jengeni barabara watu waweze ku-*move* usiku na mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona uchumi wetu unavyokua, *trend* ya ukuaji ni mdogo. Ukiangalia mwaka 2022 ukuaji wa uchumi wetu ulikuwa ni asilimia 4.7, mwaka 2021 asilimia 4.9, ina maana kuna *difference* ya asilimia 0.2. Mwaka 2023 asilimia 5.2 na

tunategemea kuwa na asilimia 6.1 mwaka 2024. Ni lazima tuangalie uchumi wetu umekaa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitazama uchumi wetu, amezungumza Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kwenye hotuba yake kwamba sekta ya kilimo ndiyo inayoongoza kwa ukuaji kwa asilimia 15.9, ikifuatiwa na sekta ya ujenzi pamoja na uzalishaji kwa maana ya viwanda. Ukiangalia ukuaji huu wa sekta ya kilimo ni nani anayeukuza huu uchumi? Nani yupo kwenye sekta ya kilimo? Ukitazama aliyeko kwenye sekta ya kilimo ni Watanzania wa kawaida. Asilimia 80 ndio wanaolima kilimo cha kawaida. Sasa kama wewe unategemea uchumi wako kukua na unayemtegemea ni mkulima, unamfanyia nini mkulima huyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Bashe, amekuja na *BBT* na mambo mengine, lakini tuna hii *document* ambayo ameizungumza hata Mheshimiwa Mkumbo ya A*SDP (Agriculture Sector Development Program)*. Hii *program* itekelezwe kwa asilimia 100. Kwa sababu gani? Katika *SDP 2* tumeona mipango mizuri ya uzalishaji kwenye sekta ya kilimo, tumeona mipango mizuri ya uchakataji wa bidhaa za kilimo, tumeona mipango mizuri ya *packaging* kwa maana kutengeneza na kuweza kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo ikiwa ni pamoja na kufanyiwa *promotion* na masuala ya ulinzi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mpango wa *SDP* ushughulikiwe, utekelezwe ndiyo mkombozi mkubwa wa uchumi wa nchi yetu. Kwa mfano, zao la pamba. Nazungumzia pamba kwa sababu natoka kwenye kilimo cha pamba. Tunalima pamba miaka yote toka tumepata uhuru mwaka 1961, tuna-*process* asilimia 25 tu. Tunachukua pamba tunai-*gin* kwa *ginners* asilimia 75 tunaipeleka nje ya nchi. Kupeleka nje ya nchi asilimia 75 ni kupeleka ajira nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *value chain*; uchakataji wa zao la pamba uongezeke. Ule Mkoa wa Simiyu mtusaidie. Serikali lazima mwekeze kwenye ku-*add value* zao la pamba. Badala ya ku-*export* pamba *lint,* kwa maana ya nyuzi, tu-

*export* majora ya nguo, tu-*export* nguo. Bila kufanya hivyo na Serikali ku-*intervene* hatuwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimtegemea mfanyabiashara mmoja awekeze kwenye ku-*gin* pamba, atengeneze kiwanda cha kufanya *spinning*, kiwanda cha kutengeneza nguo, mfanyabiashara mmoja hawezi. Hili tunalizungumza kila siku. Katika Mpango huu tunaomba mje na mkakati na mtenge fedha tutengeneze *textile industry* kwa maana ya kuhakikisha kwamba ule mpango wa *cotton to cloth* uweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia *cotton to cloth* toka enzi zile Mzee Mwijage, mzee wa vyerehani anaongelea *cotton to cloth*. Hivi mpaka leo *cotton to cloth* iko wapi? Miaka saba sasa tunaongelea *cotton to cloth*. Bila *intervention* ya Serikali kuwekeza kwenye *textile* kuhakikisha kwamba *value chain* ya zao la pamba ina-*take place,* bila kufanya hivyo, zao la pamba litaendelea kubaki vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima wa pamba mwaka jana 2022 tuliuza pamba kwa shilingi 2,000/=. Mwaka huu 2023 tumeuza pamba kwa shilingi 1,160/=, hii inakwenda wapi? Mwakani inawezekana tukauza kwa 1,000/= au chini ya shilingi 1,000/=. Huyu mkulima wa pamba mnampeleka wapi? Mkulima wa pamba analima kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye ule mpango wa *ASDP* imeeleza namna ya ku-*increase productivity* kwenye zao la pamba mwongeze *productivity* kwa maana ya ku-*improve* mbegu za pamba; kwenye heka moja ya mtu anayelima pamba, basi mfanye namna ya kuongeza uzalishaji kwa sababu sasa hivi mtu anazalisha kwenye heka moja kilo 200 mpaka 300., wakati nchi nyingine wanazalisha mpaka kilo 1,000. Ukishaongeza *productivity* maana yake ni kwamba tayari hawa watu umeshawaongezea ajira. Ukiweka vile viwanda vya ku-*process* zao la pamba tuta-*add value* zao la pamba na tutauza nguo badala ya kuuza *lint* kama tunavyofanya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Mheshimiwa Rais wetu ni mtu msikivu, ni mtu ambaye ana upendo, tunakuomba

sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo tunaomba mfanye jambo kwenye zao la pamba. Bila hivyo hatutakuwa na maendeleo yoyote katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kengele imegonga, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyongo.

Waheshimiwa wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 86 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Ujenzi, wanaklabu ya Wapingwa Rushwa kutoka Karagwe Mkoa wa Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Priscus Tarimo, mpiga kura wake kutoka Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro; Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 90 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Sokoine Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nahodha nilishakuita, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Kandege wajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru. Naomba nitoe mchango wangu kwa kunukuu maneno ya hekima kutoka katika *Quran* Takatifu na Biblia. Katika *Quran* tunaambiwa Mwenyezi Mungu anasema, "Tutawanyanyua wale waliomwamini Mwenyezi Mungu na wale wenye elimu." Kwenye Biblia tunaelezwa, "Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa yaliyo makini na yanayotamani maendeleo ya haraka yamefanya uamuzi wa kimapinduzi kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha katika sekta ya elimu hasa elimu ya sayansi na teknolojia. Hili halishangazi, ndiyo maana nchi kama India, China, Singapore, Vietnam na Korea Kusini zimepata maendeleo ya kupigia mfano katika miaka ya karibuni kwa sababu wamewekeza sana katika sekta ya elimu hasa teknolojia na sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu kubwa ninaloliona kama Taifa, ninapoangalia mipango yetu ya maendeleo, tumeweka kiasi kikubwa sana cha fedha katika kutekeleza miundombinu. Naomba samahani sana, nadhani kwenye sekta ya elimu hasa sayansi na teknolojia hatujawekeza kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalotukwamisha kama Taifa hatuna mpango madhubuti wa usimamizi wa wafanyakazi na rasilimali watu kwa ujumla *(human resource planning and management)*. Nitalifafanua jambo hili. Kila mwaka tunatenga zaidi ya shilingi bilioni 400 na mwaka huu 2023/2024 tumetenga shilingi bilioni 731 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu. Tunatayarisha madaktari, wahandisi, walimu, lakini kwa bahati mbaya tukishawatayarisha hatuwaajiri tunawaacha wanazagaa kwenye mitaa. Haya ni matumizi mabaya sana ya rasilimali ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa kuna tatizo, ama mafunzo yanayotolewa ya shahada hayana ubora unaotakiwa wa kuwawezesha vijana wetu kujiajiri ama vijana wanalazimishwa kuchukua *course* ambazo hawana *passion* nazo, hawazipendi, ama wazazi wao wanawalazimisha, kama mzazi ni daktari anatamani na mwanaye awe daktari; kama mzazi ni mhasibu anatamani mwanaye awe daktari. Pia kuna tatizo kwenye vyuo vyenyewe. Kuna uchache wa *course* za uchaguzi. Kwa maana hiyo wanafunzi wanalazimika kuchukua na masomo ambayo pengine hawayapendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushauri wangu, nafikiri wakati umefika Serikali ingefanya maamuzi mahususi, tukafanya ukaguzi wa idadi ya wafanyakazi tunaoweza kuwaajiri, *human resource audit* ili tukawasomesha watu tunaoweza kuwaajiri na fedha zinazobaki tukazielekeza kwenye mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa mafunzo ya ufundi stadi, nilikuwa na mawazo kidogo. Kuna tatizo hapa, mafunzo yanatolewa, lakini tatizo letu kama Taifa, vijana wote wa nchi nzima kuna mtaala mmoja tu wa elimu ya ufundi stadi. Hii nadhani siyo sawa, kwa sababu mahitaji ya binadamu ni

tofauti, mazingira ya mwanadamu ni tofauti, kazi kuu inayofanyika kwenye jamii ni tofauti kati jamii moja na nyingine; hata rasilimali ni tofauti. Kwa maana hiyo, hatulazimiki kwamba lazima tuwe na mtaala mmoja. Kila wilaya iwe na mtaala unaolingana na mazingira yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, jamii ya wafugaji kwa nini hatuwafundishi ufugaji wa kisasa, ujasiriamali na namna bora ya kuzalisha mazao bora ya ufugali kama vile uzalishaji wa maziwa, utengenezaji wa jibini, utengenezaji wa samli, mtindi, nyama choma na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu wanafundishwa mambo ya jumla jumla tu. Jamii ya wavuvi tungefanya hivyo hivyo na jamii ya wafugaji nyuki tungefanya hivyo hivyo. Nadhani tukifanya hivyo bila shaka tija itaonekana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nadhani mbali nakuwa na vyuo hivi vya *VETA* kila Wilaya, Serikali inapaswa kuwa na vyuo vichache sana vunavyofundisha masomo maalumu. Kwa mfano, teknolojia ya habari, mitambo inayotumia akili za bandia, uhandisi, nishati ya jua, teknolojia ya kilimo cha umwagiliaji maji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo langu la mwisho, Mipango yetu ya Maendeleo haitafanikiwa kama tunavyotarajia kama hatujawekeza kiasi cha kutosha katika sekta ya elimu. Kwa maoni yangu, nadhani sekta ya elimu inapaswa kupewa kipaumbele cha kwanza. Kwa sababu karne zilizopita utajiri na ustawi wa mataifa ulipimwa kwa kutumia nguvu ya misuli, utajiri wa mafuta, madini na gesi. Katika karne ya 21 ustawi wa mataifa utapimwa kwa kutumia nguvu ya akili, maarifa na sayansi. Naomba nirudie katika karne ya 21 mapambano makubwa na hasa vita kati ya Taifa moja na lingine hayatapiganwa sana kwa kutumia mizinga na silaha tunazoziona, bali mapambano makubwa yatakuwa katika kutumia *cyber,* yani kutumia teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, sisi kama Taifa watu wetu tuwaelekeze huko tu. Nadhani wakati umefika sasa Vyuo vyetu Vikuu na hasa vinavyofundisha mambo ya teknolojia

na sayansi kwa ujumla, vinapaswa kuanzisha *course* maalum za teknolojia ya kidigitali, *artificial intelligence* na *data science* kama tunataka kuingia kwenye karne ya 21 kwa mbwembwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Nahodha anajenga hoja ya ku-*suppress human intelligence*. *You have to incorporate artificial intelligence* katika mipango yetu, kitu ambacho anasema labda hajaona au hajasikia. Dunia inakwenda na *AI* sasa hivi, *without that* tutakwamba. *Data analysis* itafanya *AI* na *intelligence* zote zitasaidia katika mipango ya maendeleo.

Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kimei, ajiandae Mheshimiwa Kandege. Nafikiri wawili watatosha kumalizia.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa mawasilisho mazuri na Mapendekezo mazuri ya Mpango pamoja na Mwongozo wa Bajeti kwa mwaka unaokuja. Najua kwamba hii siyo Mpango, ni mapendekezo. Kwa hiyo nitajikita zaidi kwenye yale yanayoyendana na yale yaliyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuweza hatimaye kurejesha Tume ya Mipango na Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Naamini hivi ni vyombo viwili ambavyo vilikosekana na pengine ndiyo sababu tumeshindwa kwa muda mrefu kuweza kufuatilia utekelezaji wa dira yetu, kuweza kufuatilia na kutathimini mipango ambayo tumejiwekea. Hatimaye sasa tumeipata na ninaamini huko tunakoenda tutaweza kusimamia vizuri zaidi kutathmini na kujua ni kitu gani ambacho kimekosekana kwenye mikakati yetu ili kuendelea kuboresha kila wakati yale ambayo tutakuwa tunayatekeleza kwenye mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba *institution building* ni kitu kizito sana kwenye nadharia ya uchumi. Ni kitu ambacho kinawezesha. Ukiwa na taasisi zinazostahiki, taasisi za

kijamii, taasisi za kiserikali, taasisi za sekta binafsi zikiwa zimejipanga vizuri katika kusimamia maendeleo na kushauri maendeleo, basi hapo tutaona tunapata maendeleo yale ambayo tunayategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba Wakoloni waliamua kuvunja zile taasisi zetu za kiasilia ili tusipate mahali pa kujishika. Ndiyo sababu tunapata shida sana kurejesha hizi taasisi ambazo tunaamini kwamba zingekusaidia kutekeleza. Kwa mfano, kwenye kilimo bila ushirika, *actually* huwezi kufanya mambo mengi kwenye uchumi ambao umetawaliwa na wakulima wadogo wadogo. Kwa hiyo, ni mambo ya kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimbilie kwenye moja niliyonayo kwenye mwongozo wa bajeti; katika mpango huu wa miaka mitano, tulikuwa tumejiwekea lengo kwamba matumizi ya maendeleo yawe kati ya asilimia thelathini na arobaini ya bajeti yetu, na kusema kweli Bunge hili kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba bajeti ya maendeleo inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bajeti ya maendeleo imebakia pale pale trilioni 15 na kiuwiano inazidi kupungua kwa sababu ilikuwa asilimia 34 ikaenda ikafika sasa ni asilimia 32. Hili jambo bado naamini kwamba tusilikubali sana, tujaribu kumbana Waziri wa Fedha ili atekeleze vile anavyosema kwamba atajaribu kubana matumizi yasiyo ya lazima na fedha hiyo inayokuwa *served* iende kwenye maendeleo badala ya kupunguza maendeleo. Kwa hiyo, mimi naomba kwamba wakati tunapopeleka hii tuhakikishe kwamba tunaweka ukomo, kwa mfano bajeti ya kawaida isiwe zaidi ya *inflation rate*, *something like that*, tungeweka ukomo wa namna ile ili isikue sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini ukimpa mtu fedha atatumia tu, utakuta kwamba unakaribisha Waziri aje kwenye Kamati anakuja na watu hamsini. Watu hamsini wanahitajika? Wakija watatu tu au wawili wanatosha, ukweli ni kwamba tunawapa fedha nyingi mno za matumizi ya kawaida, ndio sababu wanaweza, kama ni kuhamishia *task force* zikaenda

Arusha na nini lakini wanatumia hii fedha ya kawaida bila kujali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu cha pili, kwenye hilo ni kwamba hatujafanya *public expenditure review* kwa miaka mingi kidogo, naamini turejeshe kufanya *public expenditure review* ili tuweze kufanya *strategic resources allocation* na tuone kwamba fedha zinaenda mahali pake nani wapi ambapo tunaweza tuka-*serve* ili kuweza kuchangia zaidi kwenye maendeleo ya majimbo yetu na wananchi wetu wakafurahi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri hilo ni la msingi na nafikiri kwamba Mheshimiwa Waziri anapokuja na mpango kamili atakuwa na fedha nyingi zaidi ya hiyo fedha ili angalau twende asilimia 34 kama tulivyokuwa hapo awali ili ibaki kwenye maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya mpango hayajabadilika sana na yale ya miaka hii mitatu ya nyuma na ninajua ni kwa sababu gani? Kwa sababu pengine ni mpango ule ule wa miaka mitano ndio tunautekeleza, kwa hiyo, kuna miradi inaingiliana na kadhalika lakini pia Tume ya Mipango ilikuwa ni mpya bado haijajikita sana kufanya tafiti zinazohitajika ili waweze kuleta mpango ambao una ubunifu wa kwao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kinasikitisha ni kwamba bado hatujaona mwanga unaotupeleka kukuza kasi yetu ya ukuaji wa pato letu kufikia asilimia nane. Asilimia nane ndio ilikuwa kwenye dira na karibu tungeifikia lakini ndio tukaja tukayumbushwa na Uviko lakini bado kinachosikitisha ni kwamba mipango inayokuja haijaweza kusema ni lini tutaanza kuona uchumi unarejea asilimia saba mpaka nane. Naamini bado kuna mikakati kama hii ya sekta ya kilimo na sekta nyingine inaweza ikasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi niseme kwamba, tunafahamu kwamba Waziri wa Mipango amesema vizuri sana kwamba, kupanga ni kuchagua na amesema kwamba tutakamilisha kwanza ile miradi ambayo inaendelea kabla hatujaingiza miradi mipya mingine kwenye bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni sawa kabisa na kwa sababu inaendana na ukweli kwamba *resources* zetu ziko *limited* na ukweli kwamba, hususan kwenye sekta hii ya nje hatujawa na mikakati ambayo inaweza ikawa na uhakika wa kuongeza fedha za kigeni. Fedha za kigeni zimekuwa ni utata na sasa hivi kitakachokuwa *consumed* katika kutekeleza malengo yetu ni fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *issue* inayojitokeza ni kwamba tunasema kilimo na sekta nyingine lakini na Kamati ilisema, imeona kwamba maeneo rahisi zaidi ni kwenye eneo hili la utalii na eneo la *logistics*, usafirishaji hasa kutoka kwenye Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Bandari ya Dar es Salaam tuna bahati, Mungu ametupa bahati tumepata *DP World* imekuja wakati wake, kwa hiyo, naamini kwamba inaweza ikafungua ile *logistics* ya *hub* yenyewe tukaanza kuona kwamba hii *infrastructure* iliyojengwa, barabara na *SGR* inatumika kwa uhalisia kupeleka mizigo kwa nchi jirani na kuanza kuongeza sana pesa zetu za kigeni, kutumia *DP World*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba hili ni jambo ambalo tutaiomba Serikali ilifanyie kazi na ijaribu kumuomba Mheshimiwa Rais wetu na tumuombee ili aweze kuhamasisha hawa jamaa zetu ili waweze kuingiza ule uwekezaji ambao walikuwa wameahidi, wauingize haraka kwenye hii bandari yetu na tuweze kuona tunabadilisha kabisa suala zima la *foreign exchange* hapa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona ni kwamba, matumizi ya takwimu za sensa hayajakaa sawa kwenye mipango na kwenye miongozo. Nilifikiri kwamba Serikali na Wizara hizi zingeangalia zile *statistics* za sensa ili waone kwamba ni kitu gani wanaweza kutumia kupata mapato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna idadi za nyumba na tunajua nyumba zimeandikishwa, makazi yanajulikana, kwa hiyo kuna uwezekano wa kukusanya zaidi kwenye kodi ya majengo. Tungeweza kuona kwamba ni vitu gani tunatarajia kule,

hata huku kwenye *DP World* hajaweza kuona kwamba mapato tutakayopata yataongezeka au yatakuaje kwa sababu kusema ukweli *projected revenue* ni kubwa sana ukilinganisha na uhalisia wa 2022/2023 ni *thirty-nine trillion* halafu mwaka huu 2023/2024 tumeweka *forty-four* utaona kwamba niongezeko kubwa sana kwa hapo kama ukitumia uhalisia wa mapato tuliyopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda *forty-seven trillion* ukitumia uhalisia huu tunaona utakuta kwamba hatutafikia. *Forty-seven trillion* ni fedha nyingi sana pengine *unless* mnasema *DP World* wataanza kutuingizia fedha kwenye akaunti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kwa vile usanifu wa miradi umekuwa ni hafifu na Wizara ime-*recognize* kwamba ubora ule wa usanifu wa miradi hatuna, yaani ubora ule wa usanifu na usiposanifu vizuri huwezi kupata hata *financing cost* ya miradi ile. Kwa hiyo, ndio sababu miradi inachelewa kwa sababu haikusanifiwa kwa ubora, na unaenda sokoni ukiwa na mradi ambao umesanifiwa nusunusu, haijatathminiwa na watu wawili au watatu, halafu unaenda unapata bei kubwa unashindwa kutekeleza mkakati na unaanza kupata matatizo njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri hilo ni jambo la kuangalia na ningeomba sana wizara isiingize kwenye mpango miradi ambayo haijasanifiwa. Ifanyiwe upembuzi yakinifu mapema na isanifiwe mapema ili wakati tunaingiza kwenye mpango wetu wa mwakani basi iwe inajulikana kwamba inapoenda kutekelezwa maandiko yake yamekaa vizuri na tunaweza kuyauza kwa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu niseme, nafurahi kwamba kwenye mpango huu, mkazo unawekwa kwenye sekta binafsi kushirikishwa na hii inaenda sambamba kabisa na ile sheria ya *PPP* tuliyoipitisha ambayo sasa hivi iko vizuri na ninaamini sasa hivi tutapata wawekezaji wengi ambao wataweza kuja kuwekeza kwa mpango huu wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nirejee kuwashukuru Mawaziri, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi hii anayoifanya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango. Sasa namuita Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kutoa mapendekezo ya mpango ambao Serikali inaenda kutuandalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya njema. Kipekee naomba niwapongeze Mawaziri wote wawili, walionesha ushirikiano mkubwa sana walipokuja kwenye Kamati yetu ya Bajeti. Mengi ya mapendekezo waliweza kuchukua, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa ujumla kwa uamuzi wa busara ambao unaenda kusaidia Taifa hili na hasa kwa kuingia makataba na *DP World,* naomba nimpongeze sana. Makubaliano ambayo yamefanyika na *DP World* yatakuwa na maana pale ambapo sisi kama Taifa tunaenda kufanya kazi kwa haraka na kuhakikisha kwamba bandari yetu inakwenda kuwa na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida kwa takwimu nilizonazo za kuonesha shehena ambazo zimekuwa zikienda nchi jirani kwa mwaka 2018 mpaka 2020/2023, naomba nisome kwa mwaka 2020/2023, shehena ambayo ilienda nchini Zambia ni 1,963,718, lakini ambayo imeenda Nchini DRC - Congo ni 3,495,195, Burundi ni 487,811, Rwanda 1,550,443, Malawi 610,506, Uganda 183,280 nchi nyingine 62,768 ambazo nchi hizi zinajumuisha Mozambique, Sudan, Kenya, Comoro pamoja na Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii shehena kubwa ambayo inakwenda Congo ya DRC, kwa wastani nitakupeleka shehena kama tani laki mbili na nusu, yaani katika tani laki mbili na nusu ile ambayo inaenda *Eastern Congo* ni tani elfu 50 peke yake, kwa

hiyo *Southern Congo* ambayo ndio iko na Lubumbash ni wastani wa tani laki mbili kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unaona jinsi ambavyo ni eneo gani sisi kama Taifa, tunatakiwa tuchangamkie kama fursa ili kuhakikisha kwamba shehena kubwa ambayo inaenda huku ambayo kimsingi ndio uchumi tunatumia kama fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa malori ambayo yanapita eneo linaitwa Kasumbalesa kwa siku *on average* ukenda kila muda unakuta malori kati ya mia nane mpaka 1000, na pale lori likienda linatumia kati ya siku 21 mpaka siku 30 likiwa limepaki linasubiri kwenda upande wa pili. Kwa hiyo, ni kwamba tunafikisha malori yanakaa siku 21 mpaka 30 hayafanyi shughuli yoyote zaidi ya kulipa *parking fee* na kunakuwa na taratibu za kuvusha mpaka ambapo kunakuwa na usumbufu mkubwa sana, na nchi ambazo zinatumia eneo hili ni pamoja na Afrika Kusini, Namibia, Mozambique, Tanzania na Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hiyo hoja ili niweze kuikumbusha Serikali huu mzigo ambao tunasema laki mbili unapita kwa mwezi, njia ambayo ni rahisi kabisa tukitaka kwenda Lubumbash, naomba kipekee nipongeze Serikali imefanya uwekezaji mkubwa na imejenga barabara kiwango cha lami mpaka kufika Kasanga na tayari imejenga bandari ambayo inasubiri kuanza kutumika. Hivi tunavyoongea hakuna meli hata moja ya mizigo ambayo iko Kasanga pamoja na uwekezaji mkubwa ambao umewekwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kifanyike? Upande wa Tanzania tumefanya kazi nzuri sana, na ili tuweze kutoka *Kasanga Port* kwenda upande wa pili kuna eneo ambalo linajulikana kama Mlilo, hilo ndilo ambalo Wabelgiji walisema kuna *natural hub*, kwa hiyo, ni vizuri Serikali yetu kama kuna mahusiano mazuri sana ya kidplomasia, tuweze kutumia eneo lile kujenga bandari hata kama ni kwa kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda utakaotumika badala ya siku 21 ambayo malori yanakaa unahitaji masaa matatau hadi manne umeshaenda upande wa pili, na kama Taifa, maana yake

hata mizigo ambayo imekua ikipakuliwa pale Bandari ya Dar es Salaam kwa sababu ya *congestion*, kwa sababu *movement* iko *so slow*, ukiwepo uwezekano wa kuchachusha eneo hili likatumika vizuri zaidi, hakika kama Taifa tutaanza ku-*benefit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo Serikali iendelee kufikiria namna ya kuboresha reli yetu ya TAZARA. Ili mzigo mwingi ambao unapatikana katika Bandari ya Dar es Salaam, uchukuliwe na TAZARA na ukifika Tunduma ni rahisi kutoka Tunduma kwenda Kasanga na wakati mwingine mbele ya safari wafikirie namna gani tutaweza kuboresha ili tuwe na kipande cha reli kutoka Tunduma kwenda Kasanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uharaka kabisa**,** *low hanging fruit* ndio kama hizo ambazo nasema kama Taifa tuchangamkie fursa ya kwenda *DRC* bila kukanyaga nchi nyingine yoyote. Tutoke Tanzania twende *DRC* na twende *Southern Congo* balada ya *Eastern Congo*, mzigo wake kama nilivyosema ni elfu hamsini tu lakini laki mbili *as we speak* inaenda *Southern part of Congo. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukiwa na Mheshimiwa Rais Zambia, uliahidi kwamba utakuja ili haya ambayo ninayasema uje usadiki kwa kuona jinsi ambavyo *it's so easy* sisi kama Taifa kuweza ku-*access* kwenda upande wa pili ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,eneo lingine ambalo ninaomba kuchangia ni katika suala zima la utalii; kama Taifa, utalii unaonekana kwamba kasi yake inaongezeka lakini kasi hii inaweza ikaongezeka zaidi kwa kufungua *circuit* ya *Southern Highland* ili Mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma na Rukwa, kuna vivutio ambavyo hakika bado viko *very virgin*, watu bado wanahitaji kwenda huko. Tuna kazi moja tu ya kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu ikiwepo Maporomoko ya Kalambo, linatakiwa jambo moja tu kuwa na *airstrip* kwa sababu mtalii anakuja huku na fedha yake asingependa asafiri umbali mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kalambo tuko tayari. Wizara ya Utalii wameshatuomba tuoneshe sehemu ambayo inafaa kujenga *airstrip* na sisi tuko tayari na tulishalitenga eneo. Kwa hiyo, tunaomba tu Serikali mfanye jitihada za haraka kuhakikisha kwamba uwekezaji huo uliofanyika na hasa kwa kutumia *ECF* ambayo *for sure* nadhani mwakani pesa hii itapatikana kwa ajili ya mkopo ili tuweze kuendeleza suala zima la utalii, hakika tuifungue nchi yetu pande zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kaskazini inafanya vizuri lakini ni vizuri kukawa na sehemu nyingine ambazo itakuwa ni kama sehemu ya kupumulia ili kama Taifa tutumie nchi yetu ambayo tuna *potentials* nyingi sana ambazo hatujaweza kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya michango hiyo miwili naomba niunge mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muda bado tunao, Mheshimiwa Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa nafasi na mimi njiweze kuchangia kwenye mapendekezo haya ya mpango ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais wetu Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake chanya ya kuweza kurudisha Tume ya Mipango lakini pia kwa kuunda Wizara maalum ya Mipango na Uwekezaji kwa ajili ya kushughulikia masuala mahsusi ya mipango ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri sasa kwa kuwepo kwa Tume hii ya Mipango pamoja na Wizara hii maalum kutatua changamoto zote ambazo zilikuwepo hapo awali, changamoto ambazo tuliona kila Wizara ya kisekta inapanga mipango kivyake vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili liliweza kusababisha gharama kubwa ya utekelezaji wa miradi ya maendelep lakini pia ufanisi hafifu wa utekelezaji wa miradi. Kwa mfano, Wizara ya Maji inachimba mabwawa kwa ajili ya matumizi ya binadamu, lakini

Wizara ya Kilimo inachimba mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji, vilevile Wizara ya Mifugo na Uvuvi inachimba mabwawa kwa ajili ya ufugaji wa Samaki na kunyweshea mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote hii tungeweza kuitekeleza kwa Wizara moja tu ya Maji na hivyo kuweza kutumiwa na Wizara zingine za kisekta. Bwawa hilo moja ambalo lingeweza kutengenezwa na Wizara ya Maji lingeweza kutatua tatizo la umwagiliaji, uvuvi na kilimo na hivyo basi tungeweza kuokoa gharama kubwa ambazo tungetumia kutekeleza miradi mingi kwenye kila sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa ushirikiano kunasababisha miradi kutekelezwa kwa gharama kubwa lakini pia Serikali inatawanya fedha kwenye maeneo mbalimbali na hivyo kutokuwa na ufanisi wa miradi ambayo tunaitekeleza na miradi inakuwa haina tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati ilivyoshauri, kwa miradi inayofanana basi Wizara hizi za Kisekta ziweze kushirikiana na Wizara ya Fedha ili fedha hizi ziweze kutoka kwenye fungu moja ili kutekeleza mradi mmoja wenye tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema hapo awali, pamoja na mambo mengine ambayo mapendekezo haya ya mpango yamezingatia, pia mapendekezo haya yamezingatia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi wa 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzingatia hili tunategemea tuone kwenye mpango, mikakati ya Serikali iliyonayo katika kutekeleza malengo haya kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tu, kwenye sekta ya utalii hadi kufikia mwaka 2025 tunategemea idadi ya watalii iweze kuongezeka kufikia watalii milioni tano. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye mpango unaokuja, atuainishie hapa tutawezaje

kufikia watalii milioni tano kutoka idadi ya sasa iliyopo ya watalii milioni moja na laki nne.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto zote tulizonazo kwenye sekta hii ya utalii, changamoto ya miundombinu, changamoto ya idadi ndogo ya vyumba vya kulaza wageni wetu, changamoto ya ukosefu wa maduka ya kubadilishia fedha, changamoto tuliyonayo ya ada na tozo mbalimbali ambazo ni kubwa sana kwa watalii wetu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anahitimisha atuambie mpango unaokuja utawezaje ku-*address* changamoto hizi ili tuweze kufikia malengo yaliyopo katika Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu hapa ni mfano tu nimeutoa, kwa hiyo katika malengo yote ambayo tunayo kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi basi tuhakikishe kwamba mpango wetu unaweza ku-*address* jinsi gani tunaweza kufikia malengo haya hadi ikifika 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda ni lazima kama Taifa tuweze kuongeza tija kwenye zile sekta za uzalishaji kama sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi lakini sekta ya madini pamoja na misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuongeza uzalishaji tutakuwa na uhakika wa kulisha viwanda vyetu, pia kwenye hili, ni lazima kama Taifa tuje na mikakati ya kuweza kuhakikisha tunaongeza thamani ya mauzo, ambayo tunauza nje ya nchi. Tukiweza kufanikisha haya tutaweza kukuza uchumi wa Taifa letu kwa sababu tutauza bidhaa zetu za nje kwa bei ya juu lakini vilevile tutaweza kuongeza fedha za kigeni ambayo ni changaomoto kubwa hivi sasa kwenye sekta ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, ili kufikia malengo ya mpango wa kujenga uchumi shindani ni lazima tushirikishe sekta binafsi kwa vyovyote vile. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, hapa kwenye hotuba yake naona amekazia ushiriki wa sekta binafsi lakini ombi langu nililonalo kwa Serikali hivi leo ni kwamba,

Serikali iweze kutatua changamoto zilizopo sasa hivi ambazo zinakwamisha utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za ushiriki wa sekta binafsi kwenye miradi yetu bado ni nyingi sana. Bado kuna urasimu mkubwa lakini kuna tozo na ada mbalimbali tuweze kuziangalia kwa ukaribu, lakini mazingira ya uwekezaji kwa ujumla kushirikisha sekta binafsi bado ni magumu. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hapa aweze ku-*address* mambo yote haya ambayo yanakwamisha utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mipango yetu ni lazima tuzingatie utekelezaji wa miradi wenye tija na ufanisi. Kwenye hili naomba niongelee mradi wa *BBT* wenye lengo la kujenga kesho iliyo bora. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuja na maono haya kuanzisha miradi kama hii ambayo itatatua changamoto za ajira kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya *BBT* inatekelezwa kwa fedha za Mkopo za *ECF* kutoka *IMF*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia 2023 Wizara ya Kilimo imeshatumia zaidi ya bilioni mia moja kwenye mambo haya ya *BBT,* lakini Wizara ya Mifugo na Uvuvi wameshatumiam zaidi ya bilioni 28 kwenye utekelezaji wa miradi hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun, kengele ya pili hiyo.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kusema kwamba kupanga ni kuchagua lakini sio kuchagua tu ila kuchagua mambo yaliyo bora zaidi na yenye tija. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anahitimisha asituletee orodha ya mirdi isiyotekelezeka lakini atuletee miradi michache yenye tija na inayotekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Waheshimiwa Wabunge, jioni tutakuwa na Mheshimiwa Daniel Sillo, Mheshimiwa Oran Manase, na Mheshimiwa Aloyce Kwezi, Katibu.

**NDG. HUSSEIN ATHUMAN – KATIBU MEZANI:**

*(Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.04 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Waheshimiwa tunaendelea na Orodha yetu. tulikwishamtangaza Mheshimiwa Sillo, Mheshimiwa Njenza, jiandae na Mheshimiwa Kwezi ajiandae; Mheshimiwa Sillo.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nami niweze kutoa mchango wangu katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka huo 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya kwa Taifa letu pamoja na maono makubwa ikiwemo pia Mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaokuja wa 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Profesa Kitila, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na uwekezaji pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa taarifa nzuri ambazo wamewasilisha ndani ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nimpongeze Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Kigua pamoja na Wajumbe wa Kamati, kwa kazi kubwa waliyoifanya wakati wa uchambuzi wa Taarifa hizi ambazo leo zinawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo machache. Jambo la kwanza ni ukusanyaji wa mapato. Tathmini ya ukuaji wa mapato ya ndani kwa maana ya vyanzo vyetu vya ndani kwa miaka mitano 2017/2018 hadi 2022/2023 inaonesha kwamba, mapato ya kodi yamekua kwa asilimia 10.5. mapato yasiyo ya kodi yalikua kwa asilimia 2.5. mapayo ya halmashauri yalikua kwa asilimia 14.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini makisio ya ukuaji wa jumla ya mapato yetu ya ndani kwa vyanzo vyote kwenye mpango unaopendekezwa wa 2024/2025 unatarajiwa kuwa ni asilimia 10.5. Hili linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025 Kifungu cha 18_B(3) Chama kinaielekeza Serikali. Naomba ninukuu; 18_B(1). "Kupunguza utegemezi wa kibajeti kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwemo kuibua vyanzo vipya vya mapato, kuongeza idadi ya walipa kodi, kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara na kukusanya maduhuli yote kwa kuitumia mifumo ya kielektroniki."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufiklia malengo haya ya ukuaji wa mapato ya ndani kwa wastani wa asilimia 10.5 kwa Mwaka wa fedha 2024/2025, lakini ili mapato ya kodi yaweze kuchangia ile asilimia 12.4 kwenye mapato ya taifa kama ilivyowasilishwa kwenye mapendekezo. Vile vile, ili Pato la Taifa liweze kukua kwa asilimia 5.8 kama ambavyo imependekezwa kwenye Mpango. Pia, bajeti inayotarajiwa ya trilioni 47.4 kati ya hizo trilioni 34.4 Ikiwa ni mapato ya ndani kwa zaidi ya asilimia 70. Yako mambo ya msingi ambayo kama Taifa lazima tuyafanye: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha mifumo yote ya ukusanyaji mapato hapa nchini. Tuna mifumo mingi. Kwa mfano, Mfumo wa Kodi za Ndani ambao ni *Integrated Domestic Revenue Administration System (IDRAS)*. Mfumo wa *TRANCIS* wa ushuru wa forodha. Tuna Mfumo wa *Tausi* ambao uko kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maana ya halmashauri zetu. Vile vile, tuna Mfumo wa Bandari ambao unaitwa *Terminal operating system,* tuna *GEPG* nakadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo hii yote inafanya kazi kubwa ya kukusanya mapato ya Taifa letu. Jambo kubwa la kufanya hapa ni kuhakikisha mifumo hii yote inakuwa imara ili kufikia malengo ambayo tumejiwekea kama Taifa katika kulifikia Pato la Taifa pamoja na kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa, uimara wa mifumo hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba mifumo yote hii inasomana, kwa maana ya kwamba mifumo ya Serikali za Mitaa isomane na mfumo wa TRA, Bandari na mifumo yote. Kwa hiyo, tukiwekeza kwenye mifumo hii yote ikasomana nina imani kubwa kabisa haya yote tunayoyatarajia kama Taifa tutayafikia katika mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia ni upande wa sekta ya utalii. Sekta ya utalii inachangia takribani asilimia 14 kwenye Pato la Taifa. Vile vile, inachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa huu wa miaka mitano ambao tunao, wa

mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026, ukisoma ule ukurasa wa 102, mpango katika sekta ya utalii umeelekeza kwamba, kuendeleza mazao mapya ya utalii kwa ajili ya ukuaji wa uchumi. Pili, kuendeleza Kanda ya utalii kusini mwa Tanzania. Lengo ni kukuza sekta hii muhimu sana katika ukuaji wa uchumi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020/2025 kifungu kile cha 67 kwenye ukurasa wa 11, kimeweka malengo kwamba, kufikia wastani wa watalii milioni tano ifikapo 2025 lakini pia mapato kutokana na sekta hii ya utalii kufikia dola bilioni sita ifikapo 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya si rahisi kuyafikia bila kuwa na mipango thabiti kwenye mipango yetu ya Taifa. Mambo ya kufanya: -

(i) Kuhakikisha kwamba tunatangaza vivutio vyote ndani na nje ya nchi yetu ili kuvutia watalii wa kutosha katika Taifa letu na kuongeza Pato la Taifa. *(Makofi)*

(ii) Kushirikisha sekta binafsi katika uwekezaji hasa kwenye sekta ndogo ya malazi. Tunapozungumza kwenye sekta ya malazi katika Taifa letu kwenye sekta hii ya utalii tuna vitanda chini ya 150,000. Hivi ni vichache sana ukilinganisha na hali ya utalii pamoja na fursa zilizopo katika Taifa letu. Lakini nchi Jirani ya Kenya kuna vitanda zaidi ya milioni moja. Kwa hiyo, utaona jinsi ambavyo tuko nyuma katika kuwekeza kwenye sekta hii ya utalii, hasa hoteli zenye hadhi mbalimbali za kuhakikisha kwamba watalii wanafika kwenye nchi yetu na kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ikiwekewa mikakati mizuri katika Mpango tunaopendekeza, kwanza itachochea ukuaji wa sekta yenyewe, pili, itapunguza nakisi ya urali wa malipo ya huduma, tatu, itaongeza mchango katika Pato la Taifa, kukuza uchumi na utalii katika Bajeti yetu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana Serikali katika mpango huu tunaupendekeza, tuhakikishe tunaweka

mikakati mizuri sana katika sekta hii ya utalii ambayo ukiwekeza unapata fedha za kigeni mara moja, na haichukui muda mrefu. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Mipango mtu makini sana (Profesa) na Waziri wetu wa Fedha, mhakikishe kwamba kwenye Mpango huu unaokuja tuweke mikakati mizuri sana katika sekta hii muhimu sana ya utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni tathmini ya Mpango wa Tatu wa Maendelo ya Taifa huu wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026. Ili ujue unakokwenda ni lazima ujue ulipotoka, ulipo, ili ujipange vizuri kwa safari ya mbele. Mpango huu unaopendekezwa ni Mpango wa nne ambapo tayari tumekwishatengeneza mipango mitatu. Kwa kuwa tumekwishatekeleza mpango huu zaidi ya nusu, kwa maana tayari tumekwishatekeleza mipango miatatu, iko haja ya kufanya tathmini ya vipaumbele vyote tulivyovipanga kwa miaka mitatu katika kila sekta tumekeleza kwa kiasi gani ili tujipange kwa mipango inayokuja. Kwamba ni wapi tumefeli, wapi tumefanikiwa ili tujipange vizuri katika mipango iliyobaki, kwa maana ya mpango wa nne na mpango wa mwisho, ule wa tano, wa 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungefanya *midterm revue* ya Mpango huu itasaidia sana kuona ni nini tumefanya, nini tumekwama wapi na kwa sababu gani? Mpango huu ni wa Mwisho kwa maana ya Dira ya 2025. Kwa hiyo, tukifanya tathmini ya uhakika kwa Mpango huu unaokwisha tutakuwa tumejenga msingi imara wa kuweka dira mpya ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini kabisa kwamba tukijipanga vizuri, nchi yetu ina fursa nyingi sana na Watanzania wako tayari kufanya kazi. Kazi kubwa ni kupanga na kusimamia fedha zote za uchumi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa fursa; naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango *very professional*. Hii ndiyo michango ya mipango. Vile vile, Mheshimiwa Waziri wa

Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji ambao wote mkienda nyumbani mnapanda basi moja, mmeyasikia hayo.

Mheshimiwa Njeza, jiandae Mheshimiwa Kwezi.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kwa kupata fiursa hii ya kuchangia Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa mafanikio makubwa ambayo tumeyapata sisi Tanzania. Ukiangalia huu Mpango ni sehemu ya Mpango wetu wa Taifa wa miaka mitano. Vile vile, huu ni Mpango wa nne. Dhima ya Mpango wetu ilikuwa ni kujenga uchumi shindani, viwanda na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nimeuangalia huu Mpango wetu, kwa kweli nawashukuru sana hawa Waheshimiwa Mawazii wawili na hizi Wizara mbili pamoja na Tume ya Mipango; wamefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipouangalia huu Mpango, ukiuangalia umesheheni taarifa nyingi ambazo zinaonesha ni kiasi gani Tanzania tuko vizuri kiushindani Afrika lakini hata nje ya mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utulivu wa shilingi yetu kwa kweli tuko vizuri sana. Nilikuwa nalinganisha utulivu wa shilingi kuanzia mwaka 2015 mpaka mwaka 2023. Nimekuja kupata taarifa kwamba shilingi ya kwetu ukilinganisha na Naira ya Nigeria, shilingi ya kwetu imepanda thamani kwa zaidi ya asilimia 350. Ukiilinganisha na Kenya, shilingi ya kwetu imepanda thamani kwa zaidi ya asilimia 122. Vile vile, yote hayo ukiangalia na Afrika Kusini, shilingi ya kwetu bado imepanda thamani. Hii maana yake ni kwamba utulivu wa uchumi wetu ni kutokana na hawa wenzetu na Mheshimiwa Rais ambao kwa kweli kazi yao ilikuwa ni nzuri mno. Kwa hiyo, utulivu tunaouona na hizi taarifa tunazoziona zinadhirisha kwamba, pamoja na changamoto tulizonazo duniani Tanzania tuko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuendelee kuwa vizuri ni nini cha kuangalia? Mimi kwenye mpango huu nilijikita kwenye vihatarishi. Tusipojipanga ku-*manage* hivi vihatarishi *(risk management),* haya mafanikio yote tunayoyaona na hii mipango yetu hatuwezi kwenda. Katika Mpango wameweka vihatarishi ambavyo nilipoangalia kwenye Ripoti ya Kamati ya Bajeti, wameweza kuvijumuisha katika sehemu tatu. Kwanza ni *strategic risk* au *risk* za kimkakati, ya pili ni *operational risk* au *risk* za kiutekelezaji. Sasa nilipoangalia hizi mbili zote na ukiangalia mpango, huwezi kuona kiasi gani tutaweza kuzi-*manage* hizi *risk;* kwa sababu dunia ya leo imebadilika sana. *Management* ya leo ni tofauti na huko tulikotoka. *Management* ya leo ukiangalia majadiliano ya wiki iliyopita kwa zile Kamati tatu, ukiangalia matatizo makubwa inawezekana hatukuweza ku-*manage* hizo *risk* zetu ambazo zilikuwepo. Kwa hiyo, katika mipango hii kama hatutajipanga vizuri, inawezekana haya mafanikio yote tuliyoyapata tusiweze kwenda nayo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; kwa sababu kwenye vihatarishi vya kimkakati *(strategic risk)* hapa ndiyo unaangalia sasa kwenye ile dhima ya ushindani Tanzania tutashindana vipi na wenzetu? Kwa sababu kwenye uchumi wa leo wa dunia, hizi nchi zimebaki kama vijiji, kwa hiyo Tanzania hatuwezi kuwa kama kisiwa. Kwa hiyo, sasa ni namna gani tunapopanga mipango yetu, kama huu mpango kwa hatua alizochukua Mheshimiwa Rais za kuhakikisha kuwa tunaboresha ufanyaji kazi wa Bandari zetu ambalo ni jambo jema sana, ambalo linaweza kuwa sehemu ya kutukomboa sisi kwenye changamoto zote hizi tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeizungumzia hiyo, naangalia ya kwamba, je, tumeboresha pale, mizigo itafika vipi kwa wateja wetu hasa wa nchi za nje? Hapo inabidi mkakati uwe ni kuhakikisha kuwa reli yetu ya *SGR* kipande cha Dar es salaam mpaka Makutupola, kikamilishwe haraka na kianze kufanya kazi. Hiyo itawezesha kupunguza msongamano hasa wa mizigo na hasa hata msongamano wa magari. Kwa hiyo, presha tuliyonayo ya magari sasa hivi itapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine. Ili tuhakikishe kuwa sehemu yetu ya biashara ya bandari inafanya vizuri ukilinganisha na wezetu, inabidi Serikali ichukue hatua ngumu ya kuiboresha *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kandege, amezungumza asubuhi, nimemsikiliza kwa makini sana. Mizigo yetu ya nje inapitia ukanda au mkondo huu wa Reli ya *TAZARA* au Barabara ya *TANZAM*. Kwa hiyo, tusipoiboresha *TAZARA* inawezekana ushindani wetu usiwe mzuri kwa sababu wenzetu tayari wamekwishaanzisha *Lobito Corridor* ambayo ni kwa ajili ya kushindana na bandari ya Dar es salaam. Vile vile, kuna *Naccala Corridor.*

Mheshimiwa *Mwenyekiti*, ingawaje watu wanachukua kwa wepesi lakini mkakati uliopo ni kuua biashara yetu. Sasa, ningeiomba Serikali ifanye mkakati wa kuichukulia hii kama kihatarishi cha biashara yetu na kupoteza biashara za nje. hivyo iboreshe *TAZARA*. Pia, mimi ningependelea zaidi siyo kuboresha tu, hizi reli zetu mbili ziendeshwe na watu binafsi. Na uzuri wake katika mpango, Mawaziri wameonesha ni namna gani washirikishe sekta binafsi katika biashara za reli, bandari, na viwanja vya ndege; na huo ndiyo uwe mwendelezo. Kwa sababu Serikali isijiingize kufanya biashara sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na tatizo la Sheria ya *TAZARA*. Kwa hiyo Serikali ichukue hatua katika kuhakikisha kuwa lile tatizo linatatuliwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeoneshwa kwenye Mpango (Vipaumbele) ni madini. *Resources* hizi tulizonazo hazitakuwa na maana tukichelewa kuzitumia. Uzuri wake Serikali imeonesha kwa kiasi kikubwa kuwa itaweka nguvu kubwa kwenye madini hasa haya madini ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mgano mdogo sana. Kwa Mbeya, Songwe tuna madini hayo ya kimkakati ambayo Serikali imechelewa mno kuamua ni namna gani tuyapeleke sokoni na ni namna gani tuingie sokoni. Kwa Mbeya tuna madini yanaitwa

*Niobium***.** Nimeongea mara nyingi sana inawezekana hata jina lilibadilika nikaitwa bwana Mheshimiwa M-*niobium.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo madini ingechukuliwa 2016 mzigo wa vyuma kwa ajili ya Reli yetu ya *SGR* ambao tunalalamika sasa hivi na majengo yetu, isingekuwepo. Kwa sababu wale wawekezaji wako tayari kujenga kiwanda cha kwanza Afrika na cha nne duniani ambacho kitaleta ajira nyingi lakini na *FDI* nyingi ambazo ndiyo Serikali yetu inahitaji leo kutokana na changamoto za *forex*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea kuchelewa tunajicheleweshа wenyewe. Hayo Madini yatagunduliwa sehemu zingine na hao watu wanatafuta sehemu zingine ambazo wanaweza kufanya biashara zao vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara na reli ni muhimu sana na twende kwenye barabara ambazo zina-*impact* kubwa kwenye uchumi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ujenzi wa kuboresha barabara ya *TANZAM* na barabara ya Dar es Salaam – Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *TANZAM* inahitajika siyo leo ilikuwa inahitajika juzi. Kwa hiyo naiomba Serikali ifanye haraka kukamilisha hiyo mipango iliyopo ili faida yetu ya hawa watu ambao wanaendesha Bandari iweze kuleta matunda ikiwemo vilevile na ujenzi wa Bandari Kavu ambazo zitaleta *pressure* zitaongeza ushindani kwa hawa wenzetu ambao wanataka kupoka soko letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango mzuri. Ahsante sana maneno yako mwenyewe haya umeya-*quote* ya Mheshimiwa Kitila “*My experience in Asia has led me to a different conclusion. To get good government, you must have good men and women in charge of government.*” *(Makofi)*

Serikali yetu ina watu wazuri, Mawaziri wazuri na Watendaji wazuri, tatizo *we don't work, they talk.* Tunazungumza kila siku hayo hayo. Ahsante Mheshimiwa Njeza kwa mchango mzuri na wewe unapewa maua yako kama Mwenyekiti wako. Hii ndio michango ya mipango. Ukishaanza hapa kisima kule kwangu karibu na klabu gani sijui. *(Makofi)*

Haya, Mheshimiwa Kwezi ajiandae Mheshimiwa Jonas Mbunda na ajiandae Mheshimiwa Nicholaus Ngassa.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenichekesha, ahsante na naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kutupa wasaa huu wa jioni, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoendelea nayo ya kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Mawaziri hawa wawili. Mwigulu Nchemba pamoja na Profesa pale. Niwapongeze kwa kazi nzuri walizonazo ambazo sisi Watanzania tunaziona kwa macho na hatuna haja ya kusimuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kuhusiana na Mpango wa 2024/2025, napenda niishauri Serikali yangu mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wengi sana Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana mambo ya Barabara, lakini walipokuwa wanaendelea nilikuwa najiuliza mambo ya msingi kwamba hivi kweli tunapanga Mpango wa Maendeleo wa 2024/2025, lakini yapo mambo ya msingi, sisi kama Wabunge tumekuja Bungeni tunashauri mambo mengi sana kuhusiana na barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote tunawaambia jamani tunahitaji barabara hizi kwa kuinua mishipa ya kiuchumi ya wananchi wetu. Barabara hizo ambazo tumewaomba zitawasaidia wananchi wetu kwa mfano tuliomba Barabara ya kutokea Mpanda - Kaliua mpaka Kahama. Barabara ambayo ina-*cut across* mikoa mitatu ina umuhimu gani, kwa sababu maeneo yetu sisi kwanza tunazalisha sana tumbaku, tunalima

sana mpunga, lakini bado tunalima mazao ya mahindi na mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa barabara kama hii kiuchumi tafsiri yake ni kwamba sisi tutaweza kuuza mazao yetu kwa bei kubwa sana, lakini tafsiri yetu ya pili tutakuwa na uwezo wa kusafirisha mazao yetu mfano mchele tunauza sasa hivi Uganda, tunauza Rwanda, lakini ule mzunguko uitafute Nzega tofauti na barabara tunayowashauri unakuwa umekwenda nje ya kilomita 250. Sasa ushauri kama huu mkiwa mnauzingatia tutakuwa na mipango ambayo ni endelevu na mipango mizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii nimeanza nayo kwa sababu gani? Barabara hii kwenye Ilani ya Chama ipo, 2010 - 2015 ipo 2015 - 2020 ipo sasa tuna 2020 - 2025 ipo. Nashauri tuwe na utashi wa mambo ya msingi kwa sababu tunaweza tukawa tumeweka Mipango ambayo haitekelezeki hapa ikaishia kwenye maneno na siyo kwenye vitendo tutapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashauri haya mambo ambayo tunawashauri sisi Waheshimiwa Wabunge ndio tunajua njia sahihi na ndio tunaishi kwenye yale mazingira tunaona hali halisi ya nchi yetu inakwendaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kweli wapo wasomi wa kutosha humu lakini usomi peke yake hautoshi kwa sababu usomi ni *issue* nyigine na utendaji ni *issue* nyingine. Kwa hiyo niwaombe ndugu zangu hawa wahakikishe yale ambayo sisi tunayashauri ya Mipango ya Maendeleo wanayaingiza kwenye Mpango huo wa 2024/2025 ikiwemo hii Barabara ya Mpanda - Kaliua mpaka Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ambalo naweza kushauri, nimejiuliza hii Mipango naomba muipitie vizuri sehemu moja. Tunapopanga Mipango yetu nadhani sasa hivi tunazingatia *population*. Sasa inawezekana hatuzingatii vizuri *population* kwa sababu yapo maeneo yenye idadi kubwa sana ya watu, hatujaangalia ni miradi gani mikubwa ya kitaifa tupeleke kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni nini maana yake sasa? Utakuta maeneo yenye *population* ndogo yatapelekewa miradi mikubwa, yatapelekewa miradiya masoko na mambo mengine, wakati kuna *population* kubwa ambayo ingeweza kuzungusha fedha, ingeweza kufanya biashara, tunaacha. Kwa hiyo nashauri, jambo hili ni la msingi kulizingatia kwamba maaamuzi yenu pamoja na takwimu na sasa hivi Serikai imepata idadi ya watu, basi naomba mipango iendane na maeneo husika na historia za maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilianza kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ya miradi mikubwa inayoendelea nchini. Jambo kubwa la *SGR* jamani ninaomba kabisa tusilipige vita. Tuliunge mkono kwa sababu njia nyepesi ya usafirishaji itakazoziokoa Barabara zetu nchini ni pamoja na reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaangalia gari la mizigo moja kwa maana ya reli linabeba behewa 40 na utumiaji wa mafuti hauwezi ukawa sawa na malori ambayo yatafuatana njia nzima huku yakiharibu na mizani na kila kitu. Kwa hiyo maamuzi yake ya kujenga reli ya *SGR* hususani ya Tabora – Kigoma hususani ya Kaliua - Mpanda. Ni jambo ambalo sisi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu linakwenda kuinua mishipa yetu ya kiuchumi na wananchi wataweza kupata pato na pato na Taifa litaweza kupanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kwenye Sekta ya Utalii. Hapa naona kama vile mipango yetu mingi haijawekeza nguvu ya kutosha. Tunazo *National Parks* nyingi sana karibu 22 hivi. Sasa *National Park* zote hizi tujiulize hivi wakati wa masika zote zinafikika? Je, tutakuwa na *seasonal* utalii? Tena utalii wa kiangazi tu unasubiri mvua ikiwa imekata. Maana yake ninyi mmesoma, Maprofesa mmejaa, Ma-*doctor* mmejaa. kweli tunashindwa ku-*cover* kipindi cha mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupeleke fedha nyingi sana kwenye ujenzi wa hoteli za kutosha, *camp* za kutosha barabara za kutosha, mawasiliano ya kutosha. Sisi kule tuna *National Park* moja nzuri sana, sisi tunaona ni kama *Eden village*, Ugalla *National Park,*

lakini ukiangalia hata *advertisement* ukiangalia *TV* mipango ya kutangaza michache, sasa unajiuliza hivi hawa watu wataifahamu vipi? Hata upite barabarani kabango kake unakuta ukubwa huu hapa. Kwa nini tunashindwa kuwa wa kisasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ili tuendane na usasa, ni lazima tuhakikishe vivutio vyote kama Mheshimiwa Rais alivyokuwa *frontline* kutangaza utalii hebu na sisi tusimame naye. Bahati nzuri vivutio Mungu ametubariki jamani ni kila sehemu vipo. Ukienda Kigoma kuna Gombe, Tabora kuna Ugalla, ukienda sijui *Katavi National Park* ipo ukienda maeneo yote Nyanda za Juu Kusini zimejaa Ruaha na kila kitu mpaka kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tufungue fursa hizi siyo kwa kuangalia njia moja tu kwamba huku ndio kunawezekana watalii wengi, kumbe na kule tunaweza hata utalii wa ndani tunaweza. Sisi Kaliua idadi yetu ni 768,000, hata tukifanya utalii wa ndani tu unatutosha. Tumeuza zetu mazao vizuri, miradi imefunguka, tunatakiwa tukapumzike, sasa kipindi kama hiki huwezi ukapumzika, *Christmas* unaishia nyumbani tu. Kwa hiyo Serikali tukiishauri haya iyazingatie kwa faida ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naweza kushauri, maeneo yetu mengi naomba tuelekeze nguvu kwenye ujenzi wa maghala. Wakulima wengi wanashindwa ku-*store* na wanaibiwa sana mazao yetu nchini. Anashindwa ku-*store* mazao yake, ku-*upgrade* mazao yake ili ikifikia msimu fulani sasa nakwenda Uganda kuuza mchele wangu utakwenda, nakwenda kuuza sehemu fulani mazao yangu yatakwenda, wana-*store* wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, naomba kabisa Serikali itoe msukumo uhifadhi wa maghala. Zamani nakumbuka tulikuwa tunahifadhi kienyeji wakati wa Mwalimu Nyerere, tulipewa vile vihenge vile, lakini sasa hivi hata hawaji kushauri, tujenge hivyo vitu vya msingi ili tuhakikishe wananchi wetu wanakaa vizuri na mazao yao yale na niombe kwa hapo hata Kaliua kuna maghala yanaendelea pale, tayari maeneo yako wazi Ndugu yangu Bashe anafanya kazi nzuri sana, nimwombe

atoe msukumo tukamilishe pale maghala matatu, la Zuginole, Igwisi, Ughansa kule kuna wakulima wakubwa na wa kutosha. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri tuendelee na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata wakati mgumu wakati tunapanga hii mipango yetu. Hivi tunapanga hii mipango yetu ni kutokea Wilayani kwenye Taifani au mpaka kijijini? Kama tunapanga mpaka kijijini waelewe kwamba vipo vijiji ambavyo kipindi cha masika huwezi kufika Makao Makuu ya Kijiji kwa shida ya miundombinu. Matokeo yake ni nini? Kama ni debe la mahindi lilikuwa liuzwe Sh.2,000 matokeo yake litauzwa Sh.500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, wao wanajua jiografia yetu na wanajua watu wanavyojituma, tuangalie hii mishipa ya kiuchumi tuweze kuifungua vizuri. Nimshukuru Waziri na hili moja naleta kwake ni ombi maalum pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kusema, lakini hili ni ombi maalum mezani kwake kuna ombi la wananchi wa Kaliua. Tuna shida ya miundombinu, tulishaleta mezani kwake lina muda mrefu kama miezi sita na Kamishna anafahamu na Waziri anafahamu, wananchi kule wanateseka barabara zilikatika awamu iliyopita, tumeomba *emergence* na *special fund,* mpaka sasa sijui wanakwenda kulimaje? Kwa hiyo, niombe Waziri atusaidie ili tuweze kwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mipango tunayopanga lazima tuangalie afya za wananchi wetu, ni lazima tuhakikishe uzalishaji ni pamoja na kuwa na afya bora, wakiwa na afya mbovu, hatutarajii kabisa uzalishaji utakuwa mzuri. Sasa wakiugua kama Kituo cha Afya hakiko karibu, kama zahanati haiko karibu uzalishaji unakuwaje? Anatumia muda mwingi kusafiri kwenda kufuata kituo cha afya au zahanati. Naomba haya yote tuyaingize kwenye Mpango wetu wa 2024/2025 ili Mheshimiwa Rais kuhakikisha mambo yake yanakwenda vizuri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni jioni hii ni wageni wanne wa Mheshimiwa Jonas Zeeland, wakulima wa kilimo cha miwa kutoka Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro wakiongozwa na Mwenyekiti wao Adamu Petro, Simon Petro, Sebastian James na God Venance. Karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa, sasa namwita Mheshimiwa Jonas Mbunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicholaus Ngassa naajiandae Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/2025. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kuwepo katika Bunge hili kwa siku ya leo, lakini pia nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutekeleza mipango miwili ambayo imepita na kuna mambo mengi sana ambayo yamefanyika katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ameendelea kutekeleza miradi ya kimkakati, nikitolea mfano wa *SGR* lakini Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, lakini pia ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya barabara, mambo ya elimu, ujenzi wa miundombinu kwenye shule za msingi, elimu bila malipo, ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za mikoa lakini na Hospitali za Kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kuwapongeza sana Mawaziri wawili, Waziri wetu wa Mipango na Uwekezaji, lakini pia Waziri wa Fedha kwa kuandaa Mpango mzuri wa mwaka 2024/2025 lakini pia na Mwongozo kwa ajili ya Maandalizi ya Bajeti kwa Msimu unaokuja. Nasema kwamba ameandaa Mpango mzuri kwa sababu ukipitia hiyo rasimu imetambua uwepo wa baadhi ya miradi ambayo ilianza kutekelezwa miradi ya kimkakati. Pia ukiangalia ule Mpango umetambua uwepo wa rasilimali chache ili Mpango ule uweze kutekelezwa. Rasimu ile vile vile imetambua uwepo wa

uwezekano wa kutumia Sekta Binafsi katika kutekeleza Mpango huu unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia malengo ya Mpango wetu wa Miaka Mitano ambao unaishia 2025/2026, lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaingia kwenye Uchumi Shindani, Uchumi wa Viwanda, lakini siku ya mwisho tunatakiwa tuone kabisa kwamba katika uchumi wetu pato limeongezeka na wananchi wetu wameondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulitekeleza hilo hii Rasimu ya Mpango ukiipitia imeweka vipaumbele mbalimbali vya kuvitekeleza ili tuweze kufikia malengo. Katika vipaumbele hivi vilivyowekwa, nitajikita sana kuelezea kwenye rasilimali zilizoandaliwa kutekeleza Mpango ambao utakuwa umeandaliwa. Rasilimali hizo kwanza ni mapato ya kikodi, lakini pia kuna misaada na mikopo mbalimbali ya ndani na nje, lakini pia kuna kutumia Sekta Binafsi ili kuhakikisha kwamba Mpango huu unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiingia kwenye upande wa Kodi ya Mapato, ukiangalia Mpango wetu wa miaka mitano katika Kodi zetu mbalimbali ukizifanyia uchambuzi, kuanzia mwaka 2020/2021, 2022 hadi 2025/2026, unakuta kwamba kwa mfano kwenye kodi ya mapato, unaona kabisa makusanyo yetu ni asilimia 36 mpaka 37, lakini ukienda kwenye kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* makusanyo yetu ni asilimia 29 ya Kodi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye mapato ya forodha, makusanyo yetu ni asilimia saba kuanzia ule mwaka 2021 hadi 2026. Ukienda kwenye ushuruu makusanyo yetu ni asilimia 15 na ukienda kwenye kodi zingine, makusanyo yetu ni asilimia 13 mpaka 12. Kwa hiyo ukifanya tathmini kwenye Kodi zetu na makusanyo unakuta kabisa una udhaifu katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Ili uone kabisa kwamba kuna udhaifu hivi karibuni tulipata taarifa kwamba baadhi ya Halmashauri zetu zimekusanya mapato ya ndani lakini kwa njia ambayo siyo halali. Kwa hiyo unaona kabisa kwamba kuna udhaifu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na kodi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza sasa kudhibiti hilo na kuongeza wigo wa mapato, nilikuwa nashauri kwamba kwenye Sekta ya Madini inabidi tuongeze kodi tuangalie vyanzo mbalimbali vinavyotokana na Sekta ya Madini ili tuweze kuongeza kodi. Kwa mfano, nikichukulia kwenye Mradi wa Chuma na Makaa ya Mawe Mchuchuma na Liganga unakuta kwamba katika dunia sehemu ambayo unaweza ukapata makaa ya mawe na chuma ni Liganga peke yake katika dunia. Kwa hiyo wenzetu wanasafirisha makaa ya mawe kwenda Nje kwa ajili ya kuyeyusha chuma, lakini sisi tuna uwezo wa kuwekeza Liganga, tukayeyusha chuma na tukapata *resource* nyingi sana na fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tungeweza kujenga Reli ya kutoka Mtwara kwenda Liganga na Mchuchuma, lakini vilevile kwenda Mbamba *Bay* ili kuhakikisha kwamba tunarahisisha usafirishaji wa chuma na makaa ya mawe lakini vile vile kuhakikisha kwamba tunaweza tukasafirisha kwenda nje kupitia Bandari ya Mbamba *Bay*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lingine tunaweza tukapata kodi kupitia gesi asilia inamaana tukiweka uwekezaji mkubwa kwenye gesi asilia tutakuwa na uhakika wa kupata pato la kutosha la kuweza kuendesha shughuli zetu katika nchi hii. Pia kwenye suala la ufugaji, wenzetu wafugaji ukiangalia takwimu za ufugaji unakuta Serikali inakosa mapato mengi kupitia ufugaji kwa sababu sehemu nyingi ufugaji wetu ni holela. Kwa hiyo niiombe Serikali itengeneze mfumo unaokubalika ambao utatusaidia kukusanya mapato kupitia kwa wenzetu wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningeweza kushauri ambalo litatusaidia kupata mapato ya kutosha ili ku-*finance* mpango wetu pamoja na bajeti itakayoandaliwa, ni kwenye bidhaa za misitu. Tupo chini sana kudhibiti na kuhakikisha kwamba tunakusanya mapato kupitia bidhaa za misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mwingine ambao nataka kuchangia ni kwenye kuziba mianya kwenye mifumo mbalimbali ya kodi, kwa mfano, ukiangalia kodi zetu za mapato ya ndani, bado kuna mianya ambayo inafanya mapato haya

yasipatikane kwa wingi, lakini hata ukiangalia kwenye takwimu alizozitoa Waziri kwenye kodi ya mapato na kodi zingine unakuta kabisa kwamba ongezeko au ukuaji wa uchumi wetu hauendi sambamba na mapato tunayoyapata. Kwa hiyo, hapa ningeshauri Serikali iweke mikakati na mifumo ambayo inasomana ya kutuhakikishia kwamba tutaweza kukusanya mapato yetu bila kuwa na matobo ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, wenzetu wa Rwanda uchumi wao asilimia 31 unachangiwa na sekta binafsi, nafahamu kwamba huko nyuma tulishindwa kuitumia sekta binafsi kutokana na sheria zetu zilikuwa zinatubana lakini sasa hivi tumefanya marekebisho ya Sheria ya *PPP* kwa hiyo nina uhakika tukitumia vizuri na tukaondoa vile vikwazo ambavyo vinafanya sekta binafsi zisiwekeze, nina uhakika wawekezaji watakuwa wengi na tutapanua wigo wa mapato na tutapata mapato ya kutosha kupitia sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Sasa Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, jiandae Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2000 wakati tunaweka Dira ya Maendeleo ya Taifa kwa maana ya 2000/2025 kama Taifa tuliweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha tunapambana na umaskini na kukuza uchumi. Tulianza na Mkakati wa Kupunguza Umaskini *(Poverty Reduction Strategy Paper)* tukaja MKUKUTA I, MKUKUTA II na sasa tumeingia katika ungwe ya Mpango ya Maendeleo ambayo kwa sasa tupo Mpango wa Tatu wa 2021 mpaka 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipo hapa na niliposikia na kuchangia Mpango wa 2021 nilijipa kazi ya kufanya utafiti kidogo na kujua vitu gani vinatushika miguu kama Taifa katika kuhakikisha

mipango yetu inafanikiwa. Jambo la kwanza, nilipitia Dira ya Maendeleo ya Taifa na kuona malengo makuu matano ambayo yameenda na Dira ya Maendeleo ya Taifa. Lengo la kwanza ilikuwa ni kuboresha hali ya maisjha ya Watanzania; lengo la pili kuwepo mazingira ya amani, usalama na umoja; lengo la tatu kujenga utawala bora; na lengo la nne ilikuwa kuwepo kwa jamii iliyoelimika vema na kujifunza na lengo la tano ilikuwa ni kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani kutokana na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia hayo malengo nilikuja kubaini kuna baadhi ya mambo, nilibaini mambo mengi lakini leo nitachangia mambo kama manne ambayo yamekuwa yakituvuta miguu katika kuhakikisha Taifa letu linakimbia katika kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo Taifa lakini pia katika mipango hii ambayo tumekuwa tukijiwekea na leo tuko Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nimekuja kuligundua katika utafiti wangu mdogo ambalo linatushika miguu kwa kiwango kikubwa ni urasimu katika sekta ya umma. Serikalini bado kuna urasimu mkubwa sana jambo ambalo limekuwa likitukwamisha sana katika kukimbia. Unaenda kwenye ofisi za Umma jambo linalohitaji kufanyiwa maamuzi ndani ya siku mbili au siku tatu linakaa zaidi ya wiki mbili mezani na inatakiwa watendaji wetu wachukue mfano wa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Wabunge tutakapopitisha sheria itakapofika kwenye meza ya Mheshimiwa Rais huwa haichukui zaidi ya masaa 24 Mheshimiwa Rais ameshasaini zile sheria. Ninyi kama viongozi wetu mnatupatia taarifa Bungeni lakini bado kwenye utumishi wetu wa umma urasimu umekuwa ni mkubwa vitu vinakaa muda mrefu mezani, hata kwenye suala la uwekezaji, tunawakatisha tamaa wawekezaji kwa sababu ya urasimu ambao unaendelea. Waheshimiwa Mawaziri ambao mmewasilisha leo taarifa zenu tunaomba hili jambo mshirikiane na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma lakini na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambapo kuna asilimia

80 ya watendaji wote, urasimu upungue ili tuweze kusonga mbele na tuweze kukimbizana kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilishawahi kutoa pendekezo moja, hakikisheni kwenye kila taasisi na Idara za Serikali wana *Client Service Charter,* kwa maana ya mkataba wa huduma kwa mteja. Wapeni muda, *file* likifika mezani ndani ya masaa 48 liwe limetoka ila tukiendelea, mtu anatoka ofisini hakaimishi ofisi anaenda kwenye kazi *field* anafunga ofisi anatumia siku tatu, nne ofisi imefungwa *file* limelala. Mwisho wa siku hata wananchi wetu tutaendelea kuwakatisha tamaa. Kwa hiyo, jambo la urasimu tuliangalie sana, linatukwamisha katika maendeleo yetu na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ni jambo la muhimu sana ni miundombinu ya kiuchumi. Katika suala la miundombinu ya kiuchumi tunasema hii ndio ile mishipa ya damu katika uchumi wa Taifa letu na hapa naongelea suala la umeme, barabara, reli, mawasiliano na huduma za kifedha. Kwenye suala la umeme, tunaomba kabisa Serikali kwenye huu mpango muende mkalisimamie Bwawa la Mwalimu Nyerere likamilike tuanze kuzalisha umeme wa uhakika. Uzalishaji wa sasa kwa kutumia mafuta umekuwa na hasara kubwa sana kwa wawekezaji wa nchi hii, lakini pia katika ukuzaji wa uchumi ni jambo ambalo limekuwa likilitia hasara lakini pia na gharama ya uzalishaji imeongezeka matokeo yake tunawatia hasara wawekezaji wetu, wazalishaji na pia tunaathiri uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala la barabara kumekuwa na mkazo sana, tumejikuta tumeweka nguvu kubwa sana, tumetengeneza hizi barabara kubwa kwa maana ya *trunk roads highways*. Tunaomba sasa Serikali muweke mkazo kwenye barabara za ndani *feeder roads* ambazo ndizo zinalisha maeneo mengi zinatoa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, pale kwetu Igunga tuna barabara moja ya Igulubi – Mutu – Igunga – Mwanzugi – Itumba, haya ni maeneo makubwa sana ya uzalishaji,

tumekamilisha kufanya usanifu kupitia *TARURA* na tuliambiwa tutapewa shilingi bilioni 3 na milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha hili. Naomba Waziri wa Fedha katika bajeti ijayo jambo hili ututilie mkazo, tupatiwe fedha. Sisi tunalima pamba kwa wingi, asilimia 90 ya pamba inayotoka Mkoa wa Tabora inatoka kwenye Wilaya ya Igunga na ukanda wote wa Igulubi ndio wakulima wakubwa wa pamba. Tunaomba tupatiwe fedha tuweze kurekebisha barabara hii ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa Wilaya yetu, Mkoa wetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimekuja kugundua linatushika kamba ni suala la ushiriki wa sekta binafsi. Tumekuwa tukisema kwamba tutashirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa uchumi. Hii dhana ya sekta binafsi inaeleweka sana kwa ngazi yenu huku juu ngazi ya Mheshimiwa Rais na ninyi Mawaziri lakini kule chini bado watendaji wenu wa Serikali hawatoi ushirikiano mzuri kwa sekta binafsi. Bado kuna *harassment* kubwa sana kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wafanyabiashara wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo tunahubiri lakini katika utekelezaji linakwenda tofauti, tunaomba Waheshimiwa Mawaziri hili jambo mkalisimamie vizuri ili angalau sekta binafsi kinachohubiriwa na Mheshimiwa Rais na ndiyo maana mnaona Mheshimiwa Rais anapofanya ziara ukiacha wale watu anaoambatana nao kwa sababu za kiitifaki anaenda na wafanyabiashara, lengo ni kuhakikisha sekta binafsi inakuwa ni *engine* katika kusaidia Serikali kuendesha uchumi lakini kwa juu limekaa vizuri ukienda huko ngazi za chini kwenye Wilaya zetu, kwenye Mikoa yetu bado hali si nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia la nne katika mambo ambayo yanakwamisha sana mafanikio kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa ni suala la Utumishi wa Umma. Kwenye utumishi wa umma bado kuna changamoto kubwa, jambo mojawapo ambalo ningependa kabisa kama Serikali mlitilie mkazo ni nidhamu ya kazi, bado nidhamu ya kazi siyo nzuri huko kwenu chini katika maeneo mengi ambayo sisi tunaendelea kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kuna mabishano, Mkuu wa Mkoa anabiashana na Watendaji. Mkuu wa Mkoa anatoa maelekezo anaandikia barua Watendaji kwa mfano *TRA* au Taasisi nyingine zozote wanambishia maelekezo hawayafanyii kazi. Sasa hii ni *discipline* ya aina gani katika utumishi wa umma? Tunaomba hili mlifanyie kazi ili angalau mipango yetu inapokwenda kule na kuweza ku-*harmonize situation* ili tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulisema katika upande wa utumishi wa umma ni motisha, kuhakikisha watumishi tunaendelea kuwapa motisha na motisha siyo lazima iwe fedha kwa upande wa utumishi wa umma, hata mahusiano. Wale Watendaji Wakuu wa Taasisi mhakikishe wanaishi katika mahusiano ambayo ni mazuri na watumishi wao wanaowaongoza ili waweze kuwapa ushirikiano na tuweze kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana kwa kunipa nafas. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Mwambe, jiandae Mheshimiwa Ndingo, jiandae Mheshimiwa Kwagilwa Reuben.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Mapendekezo ya Mpango, 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejipa nafasi ya kusoma hotuba zote mbili za Waheshimiwa Mawaziri ambazo wamewasilisha hapa leo na mimi nikasema basi nijipe nafasi niweze kuchangia kwa maana ya kulishauri Taifa letu. Nilipata nafasi ya kuchangia mwaka 2016 na wakati nachangia nilionesha umuhimu wa chuma kilichopo Mchuchuma ikiunganishwa na bandari yetu ya Mtwara, nashukuru Serikali imefanya maendeleo na sasa hivi tunaambiwa kwamba kule Mchuchuma pamoja na Liganga wameanza kulipa fidia ili wale wananchi waweze kuondoka eneo lile kwa ajili ya kuendeleza huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri kwenye jambo hili kwamba mpango wa sasa wa Serikali ni kuona kwanza tunachimba makaa kadri ya taarifa ambayo iko mbele yetu, wakati ule nachangia mwaka 2016 nakumbuka, nilisema nchi yetu imekuwa inapoteza pesa nyingi sana za kigeni kwa ajili ya ku-*export* chuma ili kije kuweza kujenga na kufanya matumizi mbalimbali kwa sababu nchi yetu inakuwa kwa kasi, kwa hiyo shughuli nyingi za ujenzi zinafanyika. Kwa hiyo, tuna *import* nondo nyingi sana lakini pia karibia asilimia 90 au 85 ya chuma chote ambacho kimetumika kwenye ujenzi wa *SGR* kimekuwa *imported*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii tafsiri yake tumeiondoa *forex* nyingi sana kupeleka nje. Wakati kimsingi nchi ambazo zinaendelea au zilizoendelea, kabla ya kutekeleza miradi mikubwa ambayo kwa vyovyote vile itapoteza pesa nyingi sana za kigeni wanaanza kuangalia kwanza *resources* walizonazo wao ndani. Kwa hiyo, kwa ushauri wangu kama nchi tungeanza kwanza ku-*extract* Chuma cha Liganga ili kiweze kutusaidia kwenye kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo reli hii ya *SGR* ambayo tunaisema sasa hivi lakini pamoja na ujenzi katika maeneo mbalimbali yanayoendelea ikiwa ni pamoja na majengo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bado nasisitiza kwamba tunayo makaa ya mawe maeneo ya Ngapa kule Mbinga na maeneo mengine ambayo kwa sasa hivi yanachimbwa na hatujaweza kufikia hata asilimia kubwa kama ambavyo yanahitakija. Nashangaa kuona sasa Serikali inataka tena kuchimba makaa ya mawe Liganga badala ya kutafuta kwanza mwekezaji wa chuma ambae hatuna kabisa huo mradi hapa Tanzania ili mwisho wa siku chuma hiki ki-*support* pamoja na kupunguza *export* ya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine sijaona msisitizo mkubwa sana kwenye suala la *LNG*. Natambua kwamba Lindi tuna mradi ambao unakwenda kutekelezwa karibuni lakini ili kutekeleza huu Mradi wa *LNG* ambao na wenyewe utakwenda kutusaidia kupunguza matumizi makubwa ya *forex* kwa ajili ya kuagiza mafuta kutoka nje lakini pia sasa hivi gesi kubwa tunayotumia Tanzania tunaagiza nayo kutoka nje, wakati kimsingi

bomba letu la gesi linalotokea Lindi kwa maana ya Mkoa wa Mtwara na Lindi linatumika siyo zaidi ya asilimia 10, tena kwa kuzalisha tu umeme kwenye eneo la Kinyerezi *I* na *II* pamoja na kwamba hata sisi Watu wa Mtwara tunashida kubwa sana ya umeme, kwa hiyo tunategemea tuone Serikali inaacha kuagiza sasa gesi pamoja na mafuta kutoka nje na kuweka nguvu kubwa kwenye kuimarisha huu Mradi wa *LNG* Lindi kupitia Wizara ya Nishati. Kazi ambayo inaendelea sasa hivi lakini utekelezaji wake basi uharakishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kuhusu suala la Liganga na Mchuchuma linakwenda sambamba na kuikumbusha Serikali, kwamba Serikali hii iko kwenye *movement,* iko kwenye mwendelezo unaoendelea, sasa hivi tuko kwenye Awamu ya Sita ambayo tuko nayo sasa hivi, lakini mtakumbuka mradi mkubwa wa Mtwara *Corridor* ulipigiwa sana chepua na Mheshimiwa Hayati Mkapa wakati huo kwenye Serikali ya Awamu ya Tatu nakumbuka lakini ukija kuangalia yanayotokea sasa hivi kama Mtwara *Corridor* imekuwa *abandoned,* yaani utekelezaji wa miradi ile ambayo ilikuwa inakwneda sambamba na maboresho ya Bandari ya Mtwara, maboresho ya Uwanja wa Ndege Mtwara hayawi *serious* namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naishauri Serikali na siku moja hapa Mheshimiwa *Bishop* Gwajima alishauri kwamba tunapokuwa na nchi kama nchi yetu Tanzania, nchi inayokua lazima tuhakikishe tunapoleta hii mipango inakuwa ni ya muda mrefu, tuseme tunajadili mipango ya miaka 50, kwa hiyo, kila Rais atakayeingia kwenye uongozi wake ahakikishe kwanza anatekeleza yale tuliyokubaliana katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa, badala ya kuwa na mpango wa miaka mitano mitano ama mpango wa miaka sita sita kiasi kwamba kila Rais anapokuja basi anakuwa na vipaumbele vya kwake anavyofikiri kwamba ndiyo mambo ya msingi ya kuyafanya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida, Bandari ya Mtwara kwa mfano sasa hivi, Serikali imewekeza pale pesa nyingi sana kwa ajili ya kuona ile bandari inakua lakini matumizi makubwa ni kusafirisha makaa ya mawe kwa kiasi kidogo, makaa ya mawe haya yanaletwa na malori yanaleta athari za kuharibu

barabara zetu ambapo Serikali hivi karibuni itaingia gharama kubwa ya kufanya marekebisho ya barabara kutoka Songea mpaka Mtwara pia kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tukumbuke kwenye huu Mpango wa *Mtwara Corridor* kulikuwa kunatajwa habari ya reli ya kusini. Sasa Mheshimiwa wakati unakuja kuhitimisha kwenye jambo hili utueleze, mkakati wa kuwa na reli ya kusini bado upo ama Serikali wameamua kuuacha na unafanya mikakati mingine. Kwa sababu kuna watu wengi ambao ukitokea ukanda wa Mtwara mpaka kufika Songea eneo lile ambako inasemwa reli ya kusini itapita watu waliwekewa "*X*" mpaka Peramiho nakumbushwa hapa na Mheshimiwa Jenista. Watu waliwekewa "*X*" kwenye majumba yao, kwa maana ya kwamba nyumba hizi zitavunjwa kwa ajili ya kupitisha reli, ni zaidi ya miaka kumi, zaidi ya miaka 20 sasa hivi mradi huu hautekelezwi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka tuone Serikali itueleze kwamba mkakati ule wa kuwa na reli ya kusini inayoanzia Mchuchuma na Liganga mpaka Bandari ya Mtwara bado upo au Serikali imeuacha? Kama bado upo basi tuuone kwenye vitabu kwa sababu kimsingi tunataka tuone watu wetu ili waweze kuendeleza maeneo yao.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tupate matumizi makubwa ya Bandari yetu ya Mtwara kwa sababu sasa hivi…

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu nimpige taarifa rafiki yangu na Mbunge makini, katika suala la kuleta mapinduzi huko kusini na kwa Taifa, ujenzi wa barabara ya kiwango cha zege inayotoka Lusitu Kwenda Mawengi ambayo ilikuwa inalenga kwenda Nkomang'ombe kuliko na madini ya makaa ya mawe inaendelea kuhitaji kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo imepangiwa bajeti ya Itoni kuja Lusitu lakini kutoka Nkomang'ombe kuja Liganga kwenda Madaba kwenda Songea ambayo ingetakiwa ijengwe kwa kiwango cha zege kama ilivyoaanza kile kipande cha kwanza, kilometa zilizojengwa ni 50 tu, hatuwezi kwenda kwa kutarajia kufanya mapinduzi kwa kutumia Chuma cha Liganga kwa kwenda kwa kasi ndogo kiasi hicho, vinginevyo mradi huu utaendelea kubaki miaka mingine 20 hadi 30 ijayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe taarifa unaipokea?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana *Senior* hapa Mzee wangu kwa taarifa hii nzuri, nami niungane na wewe kwamba hicho unachokisema pia kiwe kama sehemu ya mchango wangu kwa maana ya kutaka kuboresha mchango wangu, taarifa yako nimeipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nizidi kusisitiza, kwa mfano sasa hivi sisi Wabunge wa Mtwara tunakuwa tunabishana kila mara, kuhusu matumizi sahihi ya Bandari ya Mtwara, badala ya kufikiri kuhusiana na huu mradi wa Mtwara *Corridor* ambalo ni jambo ambalo lingeweza kuongezea mapato nchi yetu, sisi tumeng'ng'ana na kufikiri kwamba kusafirisha korosho, korosho inayotoka huko Tandahimba, Masasi na maeneo mengine ili kuweza kuboresha bandari yetu kitu ambacho kinafanyika katika msimu wa miezi mitatu mpaka minne tu ambayo haiwezi kusaidia na uwekezaji mkubwa uliofanyika pale na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa katika mpango wanasema wanataka sasa kuweka taa kwenye Uwanja wa Ndege wa Mtwara, niendelee kumsisitiza Mheshimiwa Waziri hapa kwamba umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Mtwara utaonekana wakati wa utekelezaji wa Mradi wa *LNG*. Pia, tuangalie na umuhimu wa Bandari ya Mtwara kwa sababu kimsingi barabara ya kutoka Dar es Salaam, Lindi mpaka Mtwara *literally* imekufa, inahitaji matengenezo makubwa sana. Kwa hiyo, wawekezaji wengi kwa vyovyote watatumia uwanja wa ndege lakini pia watatumia Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi zinakufa kwa sababu ya matumizi makubwa ya barabara kwa sababu tunakosa njia nyingine za usafarishaji. Kwa hiyo, tulikuwa tunatumia barabara muda wote kiasi kwamba barabara zetu sasa zimekufa, zinahitaji matengenezo makubwa kwa sababu ya kupitisha malori makubwa ya sementi yaliyokuwa yanatoka Kiwanda cha Dangote na sasa hivi tunashuhudia barabara ya kutoka Songea kupitia Madaba – Tunduru – Masasi - Ndada kuelekea Mtwara na yenyewe imekufa *almost,* kwa sababu ya kupitisha magari makubwa yanayobeba mkaa kutokea Ngapa, Peramiho na maeneo mengine ambako wanachimba madini haya ya makaa ya mawe. Hii ni pamoja na uchafuzi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa vyovyote kama tutakuwa tume-*concentrate* kwenye ujenzi wa reli ya kusini inayoanzia hayo maeneo niliyoyataja kufika Mtwara bandarani, kwanza tutajitahidi kulinda mazingira yetu kwa sababu reli itakuja moja kwa moja mpaka bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu nitaleta mchango mwingine wa maandishi ambao uko *more detailed* lakini ninaomba haya ya sasa myachukue na kuona namna ya kuboresha kwenye taarifa yako. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Ndingo jiandae Mheshimiwa Reuben.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kupata fursa, nami nianze kwa shukrani kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza tangu niingie hapa Bungeni nikiwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukishukuru Chama changu, ninashukuru Halmashauri Kuu ya Chama changu na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa waliyonayo na kurejesha jina langu ili nikawanie kiti hiki kwa kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Pia ninawashukuru sana wana CCM wenzangu wa Jimbo la Mbarali kwa imani yao kwangu na ninawashukuru sana wananchi wa Mbarali kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa mwakilishi wao Bungeni. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa uwakilishi baadhi ya Wabunge walifika Mbarali kusaka ushindi wa Chama cha Mapinduzi, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu niishukuru familia yangu inayoongozwa na mume wangu kipenzi kwa mapenzi, umoja na mshikamano wao, kwa niaba yao ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa mchango wangu, msingi wa maendeleo duniani ni watu, msingi wowote wa utawala duniani ni watu na maendeleo yoyote ambayo yanaweza yakafanyika yakaacha uchungu na maumivu kwa wanadamu au wananchi, hayo maendeleo si yenye tija. Ili maendeleo yawe yenye tija ni lazima yawe yanafurahiwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wowote ili utekelezeke, lazima uwe mpango shirikishi, ushirikishe wananchi. Vilevile ili mpango uweze kupangika na ukatekelezeka ni lazima mpango huo sekta zote zichukuliwe kwa uzito unaostahili. Nikianza kwa sisi Mbarali, mfano mwaka 2006 Mpango wa Serikali ulikuwa ni kutanua Hifadhi ya Ruaha. Utanuzi wa Hifadhi ile ulienda kuhamisha vijiji 10 na kata moja nzima ya kule kwetu Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ule lengo lake, pamoja na kwamba mpango ulikuwa ni kuhakikisha mnaweka uhifadhi

kwenye Bonde la Ihefu na mtiririko wa maji kwenda kwenye Mto Ruaha, mpango ule haukufanikiwa. Kwa sababu gani? Ni kwa sababu hamkushirikisha watu. Badala yake, mpaka sasa uharibifu kwenye Bonde la Ihefu umeongezeka kwa kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suluhu ya wataalam wa Taifa hili, wanataka tena kuwahamisha wana-Mbarali kwenye maeneo yale. Hili jambo likanifanya niwe msomaji sana wa matatizo kama haya kwenye mataifa mengine. Ni lazima tukubaliane, sekta na mchango wa chakula kwenye Taifa hili na kwenye Bonde la Mbarali siyo jambo la kupuuzwa hata kidogo, pia sekta ya uhifadhi siyo jambo la kupuuzwa; sekta ya utiririshaji maji kwenye Mto Ruaha pia siyo jambo la kupuuzwa. Mambo haya yote matatu yana uzito sawa. Kwa hiyo, wataalam wa Taifa hili na ninyi mliopata fursa ya kumshauri Mheshimiwa Rais, ni lazima msiwe wavivu wa kufikiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma ripoti, mnamo mwezi wa Pili mwaka huu nchi sita zilienda kupeleka Umoja wa Mataifa mipango yao ya kurejesha maeneo oevu. Mheshimiwa Prof. Kitila hapo unapenda sana kusoma vitabu, sasa nami nakuomba ukasome ili mkashauriane vizuri kuhusiana na Mbarali. Nenda kasome mpango wa Zambia walivyofanya kurejesha maeneo oevu, kasome mpango wa Gabon, kasomeni mpango wa DRC Congo, kasomeni mpango wa Mexico, walifanya yafuatayo, na Mbarali inawezekana kufanyika ili wananchi waendelee kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, walivyofanya na nilivyosoma ripoti kwa udogo kabisa, na ni mambo ya kawaida, gharama ndogo kabisa kuliko gharama za kuhamisha watu kila baada ya muda fulani. Kwanza, walianza kujenga miundombinu ya umwagiliaji. Hiyo kazi Mheshimiwa Rais ameshaifanya Mbarali na anaendelea kuifanya. Leo Waziri wa Kilimo yuko pale, kaka yangu Mheshimiwa Bashe, tuna miradi sita ya umwagiliaji inaendelea, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta shilingi bilioni 78. Mnatuhamisha twende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hivyo, juzi nilikuwa namwuliza hapa kaka yangu Mheshimiwa Bashe, mna mpango

gani wa kutujengea mabwawa? Akaniambia wanakuja Mbarali kujenga mabwawa ya umwagiliaji. Sasa mnawapeleka wapi hawa watu wakati Mheshimiwa Rais ameshaanza mipango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wenzenu walichofanya, tunajua sheria za kufanya kazi pembezoni ya mito ni mita 60. Twendeni tukapande miti pembeni ya hizo mita. Nasi wana-Mbarali tuko tayari kuongoza zoezi hilo, lakini siyo kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, wenzetu wanachofanya ili kurejesha maeneo hayo wanasema wanalima kwa msimu mmoja wa mvua. Wakulima wadogo wa Mbarali ndicho wanachofanya, wanalima msimu mmoja wakati wa mvua peke yake. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokizungumza Mbunge wa Mbarali, nami ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, uvivu wa wataalam wetu Mheshimiwa Waziri Mchengerwa tulivyoenda kule, anawauliza kwa nini hapa mnawahamisha na hawa mnawaacha? Mtaalam anasema hawa hawana miundombinu mizuri ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge ni sahihi, wataalam wetu ni wavivu wa kufikiri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la Mbarali kama mlivyotuhamisha mwaka 2008, uharibifu uliongezeka zaidi. Leo

ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja ni zaidi ya 170,000. Upi mkakati wa ku-*recover* hizo ajira? Eti tunaenda kupoteza ajira 170,000 kwa ajili ya kuhamisha watu. Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nakuomba, ungesitisha hata zile fedha zile za tathmini, mgeendelea kutujengea miundombinu Mbarali ili tuendelee kuwa salama. Tathmini hizo za nini wakati utaalam unajulikana? Kasomeni ripoti, wenzenu wa nchi hizi wamefanya haya na yamewezekana. Leo wananchi wa Mbarali wamesimamishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais, alimtuma Makamu Mwenyekiti wa Chama hiki awaambie wananchi wa Mbarali walime, lakini yako maeneo ambayo walikatazwa kulima. Leo hii ugonjwa wa sukari na Mheshimiwa dada yangu Mheshimiwa Ummy ungepeleka vipimo kule. Katika Wilaya ambayo watu wanaumwa sukari na *pressure,* Mbarali inaweza ikaongoza. Kwa hiyo, naomba sana, jambo hili hebu wataalam wa Taifa hili msiwe wavivu kufikiri. Yanapokuja masuala magumu ya wananchi, twendeni tukahakikishe wananchi wanafurahia maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utiririshaji wa maji ni muhimu. Nimezunguka Mbarali wakati wa kampeni, hata kabla ya hapo tumezunguka maeneo mbalimbali. Tumewashauri watu wa mazingira, Mbarali inapokea maji kutoka maeneo tofauti tofauti, ina vijito; mito ile imeziba. Mnasema utiririshaji wa maji kwenda Ruaha ni mbaya, tumewaambia nendeni mkachimbue ile mito vizuri ili mtiririko wa maji uende vizuri. Leo hii tunakwenda kuwaadhibu masikini wenye heka mbili, tatu, nne. Ina maana kweli sisi hatuwajui watumiaji wa maji wakubwa Mbarali? Hapana, siyo sawa. Ni lazima ifikie wakati tumshauri Mheshimiwa Rais kwa kuangalia maslahi mapana ya wana-Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili inawezekana labda wenzetu, sijui, mnaogopa kuliwasilisha. Mimi binafsi nimemwandika barua Mheshimiwa Rais nikamwone kuhusiana na hili ili nikamweleze kama ninyi mnashindwa kutusaidia wataalam wa Taifa hili kupeleka maoni ya wana-Mbarali na utaalam halisi unaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemeandikia nimwone. Naamini Mheshimiwa Rais atanipa fursa nimwone, nimwelezee nini wana-Mbarali wanataka? Naamini kwa usikivu wake, kwa upendo wake wana-Mbarali atatupa fursa tutaliangalia upya suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashukuru sana kwa kupata fursa hii. Nawaomba sana wataalam na mnaoweza kumshauri Mheshimiwa Rais, mkiwa mnakaa, suala la Mbarali siyo la kujadiliana kwenye karatasi kirahisi, siyo suala la kukaa na kujadiliana kwenye makaratasi. Chama cha Mapinduzi chenye Serikali hii, kiko na wananchi kwenye suala hili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliokuja Mbarali wako na wananchi, lakini Wabunge waliofika Mbarali kwenye kampeni ni mashahidi. Wameona hali halisi ya wana-Mbarali. Vilevile CCM, mimi Mbunge wao tuko na wananchi na suala la kuhamisha siyo suala jema na wanaofikiria kumshauri Mheshimiwa Rais hivyo hawawatendei haki wana-Mbarali na hawamtendei haki Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, tushauri vitu ambavyo vitakwenda kujenga hata *morally* ya wananchi. Twendeni mkamshauri vitu vya msingi Mheshimiwa Rais. Fikirieni wataalam wa Taifa hili, nendeni mkaanzishe vituo vya kufuatilia uhifadhi. Niwaambie kabisa, katika mpango wenu Waheshimiwa sijaona mkakati madhubuti wa mambo ya uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapenda kufanya vitu *simple,* yaani tunafanya tu uhifadhi kwa maneno. Uhifadhi unataka *investment*. Wekezeni kwenye uhifadhi. Kuhamisha watu siyo suluhu la uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashukuru sana kwa kupata fursa hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Reuben Kwagilwa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimepitia vyema taarifa ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2024/2025. Vilevile nimepitia vyema Taarifa iliyosomwa na Waziri wa Fedha, Taarifa ya Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali 2024/2025; na vilevile nimeshiriki katika maandalizi ya Taarifa yetu ya Kamati ambayo imewasilishwa na Makamu Mwenyekiti kwa niaba ya Mwenyekiti wetu, na nimemsikiliza vyema pia alipokuwa anaisoma hapa mbele ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana tunapojadili mapendekezo ya mpango, tukaifahamu historia kidogo ya chombo ambacho kimekuwa kikipanga mipango toka tumepata uhuru. Ni muhimu kujua historia hii kwa sababu lipo jambo ambalo mimi nafikiri na ninaamini hatulifanyi kwa usahihi, tunalikosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1961 mpaka 1964 mipango yetu imekuwa ikipangwa na Tume ya Maendeleo ya Uchumi, tukaona haifai, tukabadilisha. Mwaka 1965, mwaka mmoja tu mipango yetu tukaipeleka Ofisi ya Rais, Idara ya Mipango na Maendeleo; tukaona haifai tukahama. Mwaka 1965 mpaka 1975, miaka 10 hapo tukakaa, mipango yetu ikawa inapangwa na Wizara ya Uchumi na Mipango ya Maendeleo; tukaona haifai tukahama. Mwaka 1975 mpaka 1980, miaka mitano mipango yetu ikawa inapangwa na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango; tukaona haifai, tukahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 1980 mpaka 1985, 1985 mpaka 1989 tukarudi kwenye Wizara ya Fedha, Mipango na Uchumi, tukaona haifai tukahama. Mwaka 1989 mpaka 2000 mipango yetu ikawa inapangwa na Tume ya Mipango, tukaona haifai tukahama tena. Mwaka 2000 mpaka 2005 tukaenda Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, haikutosha, tukaona haifai tukahama. Mwaka 2008 mpaka 2016 mipango yetu ikawa inapangwa na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, tukaona haifai, tukahama. Mwaka 2016 mpaka 2023 mipango yetu ikawa inapangwa na Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwa historia hiyo ya kuonesha namna ambavyo Taifa limehangaika kupata wapi mipango ipangwe, nani asimamie mipango; nimesimama hapa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Maeneo yote haya ambayo nimeyataja na kuhamishwa kwa Idara hii ya Mipango imekuwa ikifanyika tu kwa *Presidential Decree*. Rais anakuja anatoa tamko, mipango ihamie sehemu fulani kama ambavyo nimeonesha. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mzungumzaji kwamba *confusion* kubwa ilitokea mwaka 2001 wakati ambapo Idara ya Kuondoa Umaskini ilipelekwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais nayo ikawa inapanga mipango. Hiyo ni taarifa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo, na pana *story* ndefu sana kwenye hili ambalo amelisema Mheshimiwa Kakunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimempongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu mwaka 2023 amerejesha Tume ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais na siyo tu *by Presidential Decree,* ameirejesha kwa sheria. Kwa hiyo, hivi sasa tunayo Sheria ya Bunge tuliyoitunga hapa juzi ya kuanzishwa Tume ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya sheria ile inasema, Tume ya Mipango, Kuanzishwa kwa Tume; kipengele cha 4(1) na (2) kinasema; "inaanzishwa Tume itakayojulikana kama Tume ya Mipango. Tume itakuwa Idara itakayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais." Sasa nimepongeza hatua hii ya kurejeshwa Tume ya Mipango na kutungiwa sheria ya uwepo wake, lakini kuna jambo moja ambalo nataka nilishauri na Serikali mlichukue. Hili litatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usipokuwa na chombo imara cha kupanga mipango, *definitely* huwezi ukaisimamia mipango hiyo. Huwezi kuifanyia tathmini mipango hiyo. Kwenye hili siyo, tu kwamba nashauri kama Mbunge wa Handeni Mjini, lakini nashauri kama mtu aliyesoma Mipango. Hapa tuliposema tume itakuwa Idara itakayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais, natamani sana Serikali na Bunge tukafanya marekebisho. Tume hii ili tuwe na mipango mizuri na tuweze kuisimamia, twendeni tukaifanye kuwa taasisi *(an institution)*. Ikiwa ni taasisi itatusaidia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, itatusaidia kuandaa wataalamu watakaopata uzoefu wa muda mrefu, lakini kutakuwa na urahisi wa kufanya *transitions* kutoka kizazi na kizazi, pia kutakuwa na mwendelezo hata wa mipango yenyewe kwa sababu ni taasisi. Hivi sasa kwenye hii Tume ambayo ipo chini ya Mheshimiwa Prof. Kitila kwenye Wizara yake, hii Tume inayojitegemea, ukiuliza leo wafanyakazi wa Tume hii, atakwambia anaokotaokota kutoka idara nyingine za Serikali. Haipaswi kuwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalieni maeneo ambayo tumetumia taasisi kufanya jambo na mwone ambavyo tumefanikiwa. Angalia leo *TRA* kama taasisi, angalia leo *NBS* kama taasisi. Ni muhimu Tume hii ya Mipango ikawa ni taasisi wala siyo Idara chini ya Ofisi ya Rais. Ikiwa taasisi, hatuiondoi pale kwa Rais. Inakuwa ni taasisi inayojitegemea ambayo iko chini ya Rais kwa sababu mipango ni *instrument* ya Rais katika kuleta maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawapeni mfano wa wenzetu ambao wamefanikiwa sana. Mfano nchi ya India, Mheshimiwa Rais alikwenda kule na bahati nzuri niliona Mheshimiwa Prof. Kitila aliambatana na Mheshimiwa Rais kule. Nina imani kwamba yapo ambayo mmejifunza. Pale India wana Tume ya Mipango *(Planning Commissioner)* ambaye leo hivi nilivyosimama imetimiza miaka 73. Ipo toka mwaka 1950 ipo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi miaka yote 62 ambayo nimeitaja kwenye ule mlolongo toka mwaka 1961 mpaka leo tunatangatanga wapi pa kuiweka Tume ya Mipango, halafu

wakati mwingine inakuwepo, wakati mwingine haipo. Sasa unaandaa *vision* ya miaka zaidi ya 20 halafu msimamizi ndani ya miaka mitano amefutwa! Unaandaa Mpango wa miaka mitano mitano ili kutekeleza *vision* ndefu ya miaka mingi, halafu Tume ya Mipango haipo, imefutwa. *Definitely* mpango wako huwezi kuusimamia. Ninatoa mifano michache hapa kuonesha namna gani tumeshindwa kuusimamia mpango kwa sababu ya *structure* yenyewe ya wapi chombo cha mipango kikae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna madini. Ameongea Mheshimiwa Mzee Njeza, tuna madini tusiyoweza kuyachimba miaka 62. Hii ni mifano michache sana natoa ili tuone kwamba tusipokuwa na chombo madhubuti, taasisi ya kusimamia na kuandaa mipango tutakuwa tuna-*miss target* na *indicators* nyingi ambazo tunakuwa tumejiwekea wenyewe. Tuna madini tusiyoweza kuyachimba, tuna samaki tusioweza kuwavua. Kwenye hili nimpongeze Mheshimiwa Rais. *Just imagine* kwa mara ya kwanza ndiyo Serikali imenunua vyombo vya uvuvi na kuvigawa nchi nzima. Yaani Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kana kwamba tumetoka msituni au tumepata uhuru leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliongea Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais kule Singida, hata yale yanayofanyika kwenye Afya, yote yanafanyika kana kwamba tumetoka msituni na tumepta uhuru leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa ambavyo Mheshimiwa Rais anapeleka, zahanati na vituo vya afya vinavyojengwa, lakini vyote hivi tungekuwa na Tume ya Mipango ambayo ni taasisi tungekuwa tumeshajenga uwezo wa kusimamia na kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalieni mambo ambayo tume-*miss target*. Tuna hekta milioni 29.4 ambazo zinafaa kwa umwagiliaji, lakini muulize Waziri wa Kilimo tumeweza kumwagilia ngapi kwenye hizo hekta milioni 29? Tumeweza kumwagilia hekta 822,000. Tuna-*miss target* kwa sababu ya kukosa mipango mizuri na taasisi ya kusimamia mipango hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vivutio vya utalii vingi sana, na tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa ile *Royal Tour* ambayo imetusaidia kuongeza watalii, lakini angalia; tuna vivutio vya utalii vingi sana ambavyo malengo yetu tulitaka tufikie watalii milioni tano na tupate fedha za kigeni *six billion USD* na tutengeneze ajira 1,750,000. Fanya tathmini leo, tuko mbali mno ya malengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa mwisho, tuna Gridi ya Taifa ambayo haijakamilisha urefu wa 9,351 kilometa na tuna uzalishaji wa umeme ambao haujafika megawati 4,915. Tusipokuwa na taasisi na tusipoifanya Tume hii kuwa taasisi tutaendelea kuya-*miss* malengo na tutashindwa kuyasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningependa kwenye mpango huu lijitokeze ukiacha huu ushauri wa kuifanya Tume kuwa taasisi huru, taasisi inayojitegemea, taasisi inayoripoti kwa Mheshimiwa Rais, taasisi ambayo ni *instrument* ya Mheshimiwa Rais, jambo lingine kwenye mpango huu ambao tulitaraji kuliona lakini halija-*surface* ni tathmini ya mpango wenyewe. Tunafunga *vision 2025* na ni miaka miwili tu baadaye, ni mwaka mmoja baada ya mpango huu kupita mwezi wa tatu, lakini hatujapata kufanya tathmini ya ule mpango. Kwa kweli siyo tu tathmini ya miaka mitano hii ya mwisho, tunataka tuone tathmini ya jumla ya miaka yote hii ambayo tumei-*practice vision* 2025. Hii tathmini inatakiwa ifanyike mapema ili ituwezeshe kuandaa *vision* nyingine ya mbele. *(Makofi)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taarifa.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba tunashindwa kufanya tathmini hiyo Mheshimiwa Kwagilwa kwa sababu hatuna taasisi inayojitegemea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii. Unajua ukiwa unaongea hapa Bungeni, unamuambukiza mwenzako umeme hapa. Kwa hiyo, ameelewa kabisa nilichokuwa nakisema kwamba ni muhimu tukawa na taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa taasisi kumefanya hata mpango wetu tukiuandaa, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Ilani ya chama changu mimi ndiyo imekuwa kiongozi wa mipango ya nchi hii. Ndiyo Ilani ya Chama, wakati kumbe *it was supposed to be the opposite*. Inatakiwa Ilani zote za vyama zi-*refer* kwenye mpango, yaani chama A kituambie tu wanafanyaje kufikia mpango wetu wa Taifa kuukamilisha, chama B watuambie hivyo. Hata ukisoma mpango leo watakwambia rejea yao walitumia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Vyama vingine ndiyo kabisa hata rejea hazipo, maana ni vyama hata Ilani havina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Bunge linarejea

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Kicheko)*

*(Saa 12.21 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 7 Novemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*